We would like to thank the Kiswahili team who contributed to this Terminology Bulletin, which is the outcome of a project which started in 2007, namely the translation of the Rome Statute into Kiswahili. Primarily devised as a working tool for interpreters and translators, this project was completed with the help of experts who thoroughly revised the document. Given that legal and judicial terminology is not fully standardised in Kiswahili, it is important to stress that this is a groundbreaking work as far as terminology is concerned.
This document is not an official version of the Rome Statute of the International Criminal Court.

If you have any comments on the bulletin or any questions on terminology matters, please do not hesitate to contact the Terminology and Reference Unit at: **terminology.terminology@icc-cpi.int**.

Copyright © STIC 2010

Nous remercions l'équipe swahili qui a travaillé à la réalisation du présent bulletin de terminologie. Ce bulletin est le produit d'un projet, commencé en 2007 : la traduction du Statut de Rome en swahili. Conçu d'abord comme un outil de travail destiné aux interprètes et aux traducteurs, il a été finalisé grâce à l'aide d'experts qui ont révisé le document de manière approfondie. Étant donné que la terminologie juridique et judiciaire n'est pas complètement normalisée en swahili, il y a lieu de souligner l'aspect novateur de ce travail du point de vue terminologique.
Le présent document ne peut être considéré comme une version officielle du Statut de Rome de la Cour pénale internationale.

Pour toute remarque sur le bulletin ou toute question portant sur un point de terminologie, n'hésitez pas à contacter l'Unité de la terminologie et des références en envoyant un courriel à l'adresse suivante : **terminology.terminology@icc-cpi.int**.

Copyright © STIC 2010

Mkataba wa Roma
wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai

Copyright © STIC 2010

Copyright © STIC 2010

Yaliyomo

Dibaji 1

Sehemu I Uanzishaji wa Mahakama 3

Ibara 1	Mahakama	3
Ibara 2	Uhusiano kati ya Mahakama na Umoja wa Mataifa	3
Ibara 3	Makao makuu ya Mahakama	3
Ibara 4	Hadhi ya kisheria na madaraka ya Mahakama	3

Sehemu II Uwezo wa kisheria, kukubalika, na sheria inayotumika 5

Ibara 5	Makosa ya jinai ambayo yapo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama	5
Ibara 6	Mauaji ya kimbari	5
Ibara 7	Makosa ya jinai dhidi ya ubinadamu	6
Ibara 8	Makosa ya jinai ya kivita	9
Ibara 9	Viambato vya makosa ya jinai	16
Ibara 10		16
Ibara 11	Uwezo wa kisheria *ratione temporis*	17
Ibara 12	Masharti ya kutumia uwezo wa kisheria	17
Ibara 13	Matumizi ya uwezo wa kisheria	18
Ibara 14	Ombi la kuanzisha upelelezi kutoka kwa Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama	18
Ibara 15	Mwendesha Mashtaka	19
Ibara 16	Kuahirisha upelelezi au mashtaka	20
Ibara 17	Masuala yanayohusu kukubalika	20
Ibara 18	Uamuzi wa awali kuhusu kukubalika	21
Ibara 19	Kupinga uwezo wa kisheria wa Mahakama au kukubalika kwa kesi	23
Ibara 20	*Ne bis in idem*	25
Ibara 21	Sheria inayotumika	25

Sehemu III Misingi ya jumla ya sheria za makosa ya jinai 27

Ibara 22	*Nullum crimen sine lege*	27
Ibara 23	*Nulla poena sine lege*	27
Ibara 24	Kutorudi nyuma *ratione personae*	27
Ibara 25	Dhima binafsi ya kosa la jinai	28
Ibara 26	Kutokuwa na uwezo wa kisheria kwa watu wenye umri chini ya miaka kumi na nane	29
Ibara 27	Kutojali madaraka yanayoambatana na cheo	29

Copyright © STIC 2010

Ibara 28 Dhima ya makamanda wa kijeshi au wakuu wengine 30
Ibara 29 Kutotumika kwa sheria inayoweka kikomo cha muda ambao kesi inaweza kufikishwa kwenye Mahakama 31
Ibara 30 Kiambato cha kisaikolojia 31
Ibara 31 Sababu za kusamehewa dhima ya kosa la jinai 32
Ibara 32 Kosa la ukweli au kosa la kisheria 33
Ibara 33 Amri kutoka ngazi za juu na maagizo ya sheria 34

Sehemu IV Muundo na utawala wa Mahakama 35

Ibara 34 Vyombo vya Mahakama 35
Ibara 35 Kazi za majaji 35
Ibara 36 Sifa, uteuzi na uchaguzi wa majaji 35
Ibara 37 Nafasi za Mahakama zilizo wazi 40
Ibara 38 Ofisi ya Rais 40
Ibara 39 Vyumba 41
Ibara 40 Uhuru wa majaji 42
Ibara 41 Kujiondoa na kukataliwa kwa majaji 42
Ibara 42 Ofisi ya Mwendesha Mashtaka 43
Ibara 43 Ofisi ya Msajili 45
Ibara 44 Watumishi 46
Ibara 45 Kiapo rasmi 47
Ibara 46 Kuondolewa kazini 47
Ibara 47 Hatua za kinidhamu 48
Ibara 48 Haki na kinga 48
Ibara 49 Mishahara, posho na gharama za matumizi 49
Ibara 50 Lugha rasmi na lugha za kazi 49
Ibara 51 Kanuni za Utaratibu na Ushahidi 50
Ibara 52 Kanuni za Mahakama 51

Sehemu V Upelelezi na mashtaka 52

Ibara 53 Uanzishaji wa upelelezi 52
Ibara 54 Kazi na madaraka ya Mwendesha Mashtaka kuhusiana na upelelezi 53
Ibara 55 Haki za watu wakati wa upelelezi 55
Ibara 56 Wajibu wa Chumba cha Utangulizi kuhusiana na fursa ya pekee ya kufanya upelelezi 56
Ibara 57 Shughuli na madaraka ya Chumba cha Utangulizi 57
Ibara 58 Kutolewa hati ya kukamata au samansi na Chumba cha Utangulizi 59
Ibara 59 Utaratibu wa kukamata katika Nchi ambamo mtu anazuiliwa 61
Ibara 60 Utaratibu wa awali mbele ya Mahakama 62

Copyright © STIC 2010

Ibara 61 Kuthibitisha mashtaka kabla ya kesi 63

Sehemu VI Kesi 67

Ibara 62 Mahali pa kesi 67
Ibara 63 Kesi mbele ya mshtakiwa 67
Ibara 64 Shughuli na madaraka ya Chumba cha Kesi 67
Ibara 65 Utaratibu baada ya kukiri kosa 69
Ibara 66 Kudhaniwa kutokuwa na hatia 71
Ibara 67 Haki za mshtakiwa 71
Ibara 68 Kuwahami waathiriwa na mashahidi na kushiriki kwao kwenye kesi 73
Ibara 69 Ushahidi 74
Ibara 70 Makosa dhidi ya utoaji wa haki 75
Ibara 71 Adhabu kwa utovu wa nidhamu kwenye Mahakama 77
Ibara 72 Kulinda habari zinazohusiana na usalama wa taifa 77
Ibara 73 Habari au nyaraka kutoka kwa mtu wa tatu 80
Ibara 74 Mahitaji ya kufikia uamuzi 80
Ibara 75 Malipo kwa waathiriwa 81
Ibara 76 Kutoa adhabu 82

Sehemu VII Adhabu 83

Ibara 77 Adhabu zinazoweza kutolewa 83
Ibara 78 Kuamua adhabu 83
Ibara 79 Mfuko wa Dhamana 84
Ibara 80 Kutozuia kutumika kwa adhabu na sheria za kitaifa 84

Sehemu VIII Rufaa na marudio 85

Ibara 81 Rufaa dhidi ya uamuzi wa kuachia au kutia hatiani au dhidi ya hukumu 85
Ibara 82 Rufaa dhidi ya maamuzi mengine 87
Ibara 83 Taratibu za kukata rufaa 88
Ibara 84 Marudio ya kutiwa hatiani au adhabu 89
Ibara 85 Fidia kwa mtu aliyekamatwa au aliyepatikana na hatia 90

Sehemu IX Ushirikiano wa kimataifa na msaada wa kisheria 91

Ibara 86 Wajibu wa jumla wa kushirikiana 91
Ibara 87 Maombi ya ushirikiano : vipengele vya jumla 91
Ibara 88 Kuwepo kwa taratibu zilizo chini ya sheria za kitaifa 93
Ibara 89 Kuwawasilisha watu kwenye Mahakama 93

Copyright © STIC 2010

Ibara 90	Maombi shindani	94
Ibara 91	Yaliyomo kwenye ombi la kukamata na kuwasilisha	97
Ibara 92	Kukamatwa kwa muda	98
Ibara 93	Aina nyingine za ushirikiano	99
Ibara 94	Kuahirisha utekelezaji wa ombi kuhusiana na upelelezi au mashtaka yanayoendelea	103
Ibara 95	Kuahirisha utekelezaji wa ombi kuhusiana na pingamizi la kukubalika	103
Ibara 96	Yaliyomo katika ombi la misaada ya aina nyingine chini ya ibara 93	104
Ibara 97	Mashauriano	105
Ibara 98	Ushirikiano kuhusiana na kumwondolea mtu kinga ya kisheria na kuridhia kumwasilisha	105
Ibara 99	Utekelezaji wa maombi yaliyotolewa chini ya ibara 93 na 96	106
Ibara 100	Gharama	107
Ibara 101	Kanuni ya shtaka maalumu	108
Ibara 102	Matumizi ya istilahi	108

Sehemu X Utekelezaji 109

Ibara 103	Wajibu wa Nchi katika utekelezaji wa adhabu za kifungo	109
Ibara 104	Mabadiliko katika uteuzi wa Nchi ya utekelezaji	110
Ibara 105	Utekelezaji wa adhabu	110
Ibara 106	Usimamizi wa utekelezaji wa adhabu na wa hali ya kifungo	111
Ibara 107	Kuhamisha mtu aliyehukumiwa baada ya kumaliza adhabu yake	111
Ibara 108	Kikomo cha mashtaka au adhabu ya makosa mengine	112
Ibara 109	Utekelezaji wa hatua ya kupiga faini au kunyang’anywa mali	112
Ibara 110	Mahakama kufanya marudio ya hukumu kuhusiana na upunguzaji wa adhabu	113
Ibara 111	Kutoroka	114

Sehemu XI Baraza la Nchi zinazounda Mahakama 115

Ibara 112	Baraza la Nchi zinazounda Mahakama	115

Sehemu XII Mambo ya fedha 118

Ibara 113	Kanuni za fedha	118
Ibara 114	Ulipaji wa gharama	118
Ibara 115	Fedha za Mahakama na za Baraza la Nchi zinazounda Mahakama	118

Copyright © STIC 2010

Ibara 116 Michango ya hiari 118
Ibara 117 Ukadiriaji wa michango 119
Ibara 118 Ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 119

Sehemu XIII Vifungu vya mwisho 120

Ibara 119 Usuluhishi wa migogoro 120
Ibara 120 Tamko linalolenga kutoa au kubadili matokeo ya kisheria 120
Ibara 121 Marekebisho 120
Ibara 122 Marekebisho ya vipengele vya kiasasi 121
Ibara 123 Mapitio ya Mkataba 122
Ibara 124 Vipengele vya mpito 123
Ibara 125 Saini, ridhaa, kukubali, idhini au kujiunga 123
Ibara 126 Kuanza kutumika 123
Ibara 127 Kujitoa 124
Ibara 128 Makala halisi 124

Copyright © STIC 2010

Copyright © STIC 2010

Dibaji

Nchi zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu,

Zikifahamu kwamba watu wote wanaunganishwa na matakwa ya namna moja na kwamba utamaduni wao unaunda urithi wa pamoja, na zikiwa na wasiwasi kwamba mchanganyiko huu dhaifu wa mambo mbalimbali unaweza kuvunjika wakati wowote**,**

Zikizingatia kwamba katika karne hii mamilioni ya watoto, wanawake na wanaume wameathiriwa na ukatili wa kutisha ambao unashtusha sana hisia za ubinadamu,

Zikitambua kwamba makosa ya jinai makubwa kiasi hicho yanatishia amani, usalama na ustawi wa dunia,

Zikithibitisha kwamba makosa ya jinai makubwa kuliko yote yanayohusu jumuiya ya kimataifa kwa jumla hayawezi kuachiliwa yatendeke bila adhabu na lazima ihakikishwe kwamba yanafunguliwa mashtaka kwa kuchukuliwa hatua katika ngazi ya kitaifa na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa,

Copyright © STIC 2010

Zikiwa zimedhamiria kukomesha kutoadhibiwa kwa wahalifu na hivyo kutoa mchango katika kuzuia makosa mapya ya jinai ya aina hiyo,

Zikikumbuka kwamba ni wajibu wa kila Nchi kutumia uwezo wake wa kisheria dhidi ya wale wanaohusika na makosa ya jinai ya kimataifa,

Zikitilia mkazo Madhumuni na Kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa na, hususan kwamba Nchi zote zitajizuia kutoa vitisho au kutumia nguvu dhidi ya umoja na utawala wa Nchi au uhuru wa kisiasa wa Nchi yoyote ile au kwa namna nyingine yoyote ile iliyo kinyume na Madhumuni ya Umoja wa Mataifa,

Zikitilia mkazo kwamba Mkataba huu hautachukuliwa kuwa ni kibali cha kuiruhusu Nchi yoyote mojawapo ya zile zinazounda Mahakama kuingilia kati kwenye mgogoro wa kivita au katika mambo ya ndani ya Nchi nyingine,

Zikikusudia, kwa madhumuni yote haya na kwa maslahi ya vizazi vilivyopo na vitakavyokuja baadaye, kuunda Mahakama ya Jinai ya kudumu ya Kimataifa ambayo ni huru na yenye kushirikiana na Umoja wa Mataifa, na yenye uwezo wa kisheria juu ya makosa ya jinai makubwa kuliko yote yanayohusiana na jumuiya ya kimataifa kwa jumla,

Zikitilia mkazo kwamba Mahakama ya Kimataifa ya Jinai iliyoundwa chini ya Mkataba huu ina madhumuni ya kusaidia tu mahakama za kitaifa za jinai,

Zikiazimia kuhakikisha kuwepo kwa heshima ya kudumu kwa ajili ya utekelezaji wa haki ya kimataifa,

Zilikubaliana yafuatayo :

Copyright © STIC 2010

Sehemu I Uanzishaji wa Mahakama

Ibara 1
Mahakama

Kumeundwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ("Mahakama"). Ni asasi ya kudumu ambayo itakuwa na mamlaka dhidi ya watu wanaotenda makosa makubwa ya jinai yanayohusu mataifa yote, kama yanavyotajwa katika Mkataba huu, na itakuwa kwa ajili ya kusaidia mahakama za kitaifa za jinai. Uwezo wa kisheria na shughuli za Mahakama vitatawaliwa na vipengele vya Mkataba huu.

Ibara 2
Uhusiano kati ya Mahakama na Umoja wa Mataifa

Mahakama itawezeshwa kuwa na uhusiano na Umoja wa Mataifa kupitia mkataba utakaoidhinishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama na kusainiwa na Rais wa Mahakama kwa niaba ya Mahakama.

Copyright © STIC 2010

Ibara 3
Makao makuu ya Mahakama

1. Makao makuu ya Mahakama yatakuwa mjini The Hague nchini Uholanzi ("Nchi mwenyeji").

2. Mahakama na Nchi mwenyeji watatiliana saini mkataba unaohusu makao makuu na mkataba huo utaidhinishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama na baadaye kusainiwa na Rais wa Mahakama kwa niaba ya Mahakama.

3. Kama inaona ni muhimu, Mahakama inaweza kuwa na kikao chake mahali pengine, kulingana na vipengele vya Mkataba huu.

Ibara 4
Hadhi ya kisheria na madaraka ya Mahakama

1. Mahakama itakuwa na hadhi ya kisheria za kimataifa. Pia itakuwa na uwezo wa kisheria kama itakavyohitajika wa kuiwezesha kuendesha shughuli zake na kutekeleza madhumuni yake.

2. Mahakama inaweza kuendesha shughuli zake na kutumia madaraka yake kama ilivyo kwenye Mkataba huu, kwa makubaliano maalumu, kwenye eneo la Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama.

Copyright © STIC 2010

Sehemu II Uwezo wa kisheria, kukubalika, na sheria inayotumika

Ibara 5
Makosa ya jinai ambayo yapo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama

1. Uwezo wa kisheria wa Mahakama utaishia kwenye makosa makubwa ya jinai tu yanayohusu jumuiya ya kimataifa kwa jumla. Kwa mujibu wa Mkataba huu, Mahakama ina uwezo wa kisheria kwa makosa ya jinai yafuatayo :

   (a) Kosa la jinai la mauaji ya kimbari ;

   (b) Makosa ya jinai dhidi ya ubinadamu ;

   (c) Makosa ya jinai ya kivita ;

   (d) Kosa la jinai la uvamizi ;

Copyright © STIC 2010

2. Mahakama itatumia uwezo wake wa kisheria kuhusiana na kosa la jinai la uvamizi baada ya kipengele kuidhinishwa kwa mujibu wa ibara 121 na 123 zinazofafanua kosa husika la jinai na kutoa masharti ambayo Mahakama itatekeleza uwezo wake wa kisheria kuhusiana na kosa hili la jinai. Kipengele hicho kitalingana na vipengelele husika vya Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Ibara 6
Mauaji ya kimbari

Kwa madhumuni ya Mkataba huu, "mauaji ya kimbari" yanamaanisha kitendo chochote kati ya vitendo vifuatavyo, kilichotendwa kwa nia ya kuangamiza kwa jumla au sehemu, kikundi cha taifa, cha kabila, cha jamii au cha dini, kinachotambuliwa kama hivyo :

   (a) Mauaji ya jamii ya kikundi fulani ;

   (b) Kusababisha madhara makubwa ya kimwili au ya kiakili kwa jamii ya kikundi fulani ;

(c) Kusababisha kwa makusudi, hali ya maisha ambayo inaweza kusababisha kuangamia kwa kikundi kizima au sehemu ya kikundi cha jamii fulani ;

(d) Kulazimisha taratibu zenye nia ya kuzuia uzazi miongoni mwa kikundi ;

(e) Kuhamisha kwa nguvu watoto kutoka kwenye kikundi kimoja kwenda kwenye kikundi kingine.

Ibara 7
Makosa ya jinai dhidi ya ubinadamu

1. Kwa madhumuni ya Mkataba huu, "kosa la jinai dhidi ya ubinadamu" linamaanisha kitendo chochote kati ya vitendo vifuatavyo, kinapotendwa kama sehemu ya mpango ulioathiri watu wengi au mpango ulioandaliwa kwa makusudi wa kufanya mashambulio dhidi ya raia :

Copyright © STIC 2010

(a) Mauaji ;

(b) Maangamizi ;

(c) Kutia utumwani ;

(d) Kuondosha nchini au kuhamisha watu kwa nguvu nchini ;

(e) Kufunga gerezani au kunyima kwa kiwango kikubwa uhuru wa mtu kinyume na kanuni za msingi za sheria za kimataifa ;

(f) Mateso ;

(g) Ubakaji, utumwa wa ngono, ukahaba wa kulazimisha, mimba ya kulazimishwa, kuhasi kwa nguvu, au aina yoyote ya ukatili wa kingono ambao athari zake zinaweza kulinganishwa na hayo ;

(h) Utesaji dhidi ya kikundi au jamii iliyoainishwa kwa misingi ya kisiasa, rangi, kitaifa, kikabila, kiutamaduni,

kidini, kijinsia kama inavyofafanuliwa katika aya 3, au kwa sababu nyingine ambazo hazikubaliki kimataifa chini ya sheria za kimataifa, kuhusiana na kitendo chochote kinachotajwa ndani ya aya hii au kosa lolote la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ;

(i) Upotezaji wa watu wa kulazimisha ;

(j) Kosa la jinai la ubaguzi wa rangi ;

(k) Matendo mengine ya kinyama ya aina kama hii ambayo kwa makusudi yanasababisha madhila makubwa au madhila makubwa ya kimwili, ya kiakili au ya kiafya.

2. Kwa madhumuni ya aya 1 :

(a) "Shambulio dhidi ya raia wowote "inamaanisha mwenendo unaohusu utendaji wa matendo kadhaa yanayotajwa katika aya 1, dhidi ya raia wowote, katika kutekeleza au kuendeleza sera ya serikali au ya shirika ya kufanya shambulio kama hilo ;

Copyright © STIC 2010

(b) "Maangamizi" ni pamoja na kusababisha kwa makusudi hali fulani ya maisha, kama vile kuwanyima watu chakula na dawa kwa madhumuni ya kuangamiza sehemu fulani ya raia ;

(c) "Kutia utumwani" inamaanisha kutumia madaraka fulani au madaraka yote yanayohusu haki ya kummiliki mtu, pia kuyatumia madaraka hayo kwa kufanya biashara ya kuuza watu, hususan wanawake na watoto ;

(d) "Kuondosha nchini au kuhamisha kwa nguvu nchini" inamaanisha kuhamisha kwa nguvu watu wanaohusika, kwa kuwafukuza au kwa kutumia matendo mengine ya kushurutisha, kutoka sehemu wanapoishi kisheria, bila sababu zinazokubaliwa chini ya sheria za kimataifa ;

(e) "Mateso" inamaanisha kusababisha kwa makusudi uchungu au maumivu makali, ya kimwili au ya kiakili, kwa mtu aliye chini ya ulinzi au mamlaka ambayo

mshtakiwa yupo chini yake ; isipokuwa kama mateso hayo hayatajumuisha maumivu au madhila yanayotokana na adhabu za kisheria au kusababishwa nazo ;

(f) "Mimba ya kulazimishwa" inamaanisha kumweka kizuizini kinyume cha sheria mwanamke aliyetiwa mimba kwa nguvu, kwa nia ya kuathiri muundo wa kabila la raia fulani au kuendeleza vitendo vingine viovu vya ukiukaji mkubwa wa sheria za kimataifa. Ufafanuzi huu usichukuliwe kuwa unaathiri kwa namna yoyote ile sheria za kitaifa zinazohusiana na mimba ;

(g) "Utesaji" inamaanisha kunyima kabisa kwa makusudi haki za msingi kinyume cha sheria za kimataifa, kwa sababu zinazoambatana na utambulisho wa kikundi au jamii fulani ;

(h) "Kosa la jinai la ubaguzi wa rangi" inamaanisha vitendo vya kinyama vinavyofanana na vile vinavyotajwa kwenye aya 1, vilivyotendwa na asasi ya kiutawala inayoendesha sera za makusudi za kikundi kimoja cha kikabila kukikandamiza kikundi au vikundi vingine vya kikabila kwa madhumuni ya kuiwezesha asasi hiyo kudumisha utawala wake ;

(i) "Upotezaji watu kwa lazima" inamaanisha kuwakamata, kuwaweka kizuizini au kuwateka watu nyara kwa kibali, msaada au ridhaa ya serikali au chama cha siasa ikifuatiwa na kukataa kukiri kuwanyima wahusika uhuru huo na kutoa taarifa juu ya mustakabali wao au mahali walipo watu hao kwa nia ya kuwazuia wasilindwe na sheria kwa muda mrefu.

3. Kwa madhumuni ya Mkataba huu, ieleweke kuwa neno "jinsia" linamaanisha jinsia zote mbili, ya kiume na ya kike, kufuatana na muktadha wa kijamii. Neno hilo halina maana nyingine yoyote tofauti na hii.

Copyright © STIC 2010

Ibara 8
Makosa ya jinai ya kivita

1. Mahakama ina uwezo wa kisheria kuhusu makosa ya jinai ya kivita, hasa pale yanapotendwa kama sehemu ya mpango au sera au kama sehemu ya mpango mkubwa wa kutenda makosa hayo ya jinai.

2. Kwa madhumuni ya Mkataba huu, "makosa ya jinai ya kivita" inamaanisha :

(a) Ukiukaji mkubwa wa Mikataba ya Geneva ya tarehe 12 Agosti 1949, yaani mojawapo ya vitendo vifuatavyo dhidi ya watu au mali zinazolindwa chini ya vipengele vya Mikataba husika ya Geneva :

(i) Mauaji ya kukusudia ;

(ii) Mateso au utendeaji wa kinyama, ikiwa ni pamoja na majaribio ya kibiolojia ;

(iii) Kelo Kusababisha kwa makusudi madhila makubwa, au madhara makubwa ya kimwili au kiafya ;

(iv) Uharibifu mkubwa na kutwaa mali pasipokuwa na sababu zozote za kijeshi na vitendo hivyo kutendwa kinyume cha sheria na kiholela ;

(v) Kulazimisha mfungwa wa kivita au mtu yeyote anayekingwa kutumikia majeshi au utawala wa adui ;

(vi) Kumnyima kwa makusudi mfungwa wa kivita au mtu yeyote anayelindwa haki ya kesi ya haki na ya kutopendelea ;

(vii) Kuondosha nchini au kuhamisha au kuweka kizuizini isivyo halali ;

(viii) Kuteka nyara ;

Copyright © STIC 2010

(b) Ukiukaji mwingine mkubwa wa sheria na desturi vinavyotumiwa wakati wa migogoro ya kivita vya kimataifa, ndani ya mfumo wa sheria za kimataifa ambazo ni chochote cha vitendo vifuatavyo :

(i) Kuelekeza mashambulio kwa makusudi dhidi ya raia au dhidi ya raia mmoja mmoja wasiohusika moja kwa moja na uhasama ;

(ii) Kuelekeza mashambulio kwa makusudi dhidi ya rasilimali za raia, yaani, rasilimali ambazo si malengo ya kijeshi ;

(iii) Kuelekeza mashambulio kwa makusudi dhidi ya watumishi, majengo, vifaa, vitengo au magari yanayotumiwa kwa huduma na msaada wa kibinadamu au kikosi cha kulinda amani, kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ilimradi tu wanastahili ulinzi wanaopewa raia au vitu vya kiraia chini ya sheria za kimataifa zinazohusiana na mgogoro wa kivita ;

(iv) Kushambulia kwa makusudi, kwa kujua kwamba shambulio hilo litasababisha vifo visivyotegemewa au kujeruhi raia au kuharibu rasimali za raia au kuleta madhara ambayo yatakuwa na athari kubwa na ya muda mrefu na itakayochafua sana mazingira, ambayo haitalingana kwa ukubwa wake na maslahi yaliyo dhahiri ya jumla ya kivita yaliyotarajiwa ;

(v) Kushambulia au kupiga mabomu kwa namna yoyote ile miji, vijiji, makazi au majengo ambayo hayalindwi na ambayo si malengo ya kijeshi ;

(vi) Kuua au kujeruhi mpiganaji ambaye aliweka silaha zake chini au ambaye hana tena namna yoyote ya kujikinga, na amejisalimisha kwa hiari yake ;

Copyright © STIC 2010

(vii) Kutumia vibaya bendera ya kusalimu amri, bendera au alama ya kijeshi na sare ya adui au ya Umoja wa Mataifa, pamoja na nembo zenye kutambulika za Mikataba ya Geneva, na kusababisha vifo au majeraha makubwa kwa mtu ;

(viii) Serikali iliyovamia eneo, kuhamishia raia wa eneo hilo moja kwa moja au kinyemela katika eneo inalolimiliki au kuondosha nchini au kuhamisha raia wote au baadhi ya raia wa Nchi iliyovamiwa ndani au nje ya Nchi hiyo ;

(ix) Kuelekeza kwa makusudi mashambulio dhidi ya majengo ya kidini, ya elimu, sanaa, sayansi au ya kutoa misaada, minara ya kihistoria, hospitali na mahali wanamokusanywa wagonjwa na majeruhi, ilimradi tu si malengo ya kijeshi ;

Copyright © STIC 2010

(x) Kukatakata viungo vya miili ya watu walio chini ya utawala wa upande wa upinzani au kuwafanyia majaribio ya tiba au ya kisayansi ya namna yoyote ambayo hayahusiani na matibabu, tiba ya meno au ya kihospitali ya mtu anayehusika wala hayafanywi kwa maslahi yake na yenye kusababisha kifo au kuhatarisha sana afya ya mtu au watu hao ;

(xi) Kuua au kujeruhi kwa kiusaliti watu kutoka taifa au jeshi la adui ;

(xii) Kutangaza kuuliwa kila mtu ;

(xiii) Kuharibu au kuteka rasilimali za adui, isipokuwa kama uharibifu au utekaji huo unalazimishwa na mahitaji yanayotokana na vita ;

(xiv) Kutangaza kufutwa, kuahirishwa au kutokubalika mbele ya mahakama haki na madai ya raia wa upande wa adui ;

(xv) Kulazimisha raia wa upande wa adui kuhusika kwenye operesheni za kivita dhidi ya Nchi yao, hata kama walikuwa wakimtumikia mpiganaji vita huyo kabla ya vita kuanza ;

(xvi) Uporaji wa mji au eneo, hata kama panashambuliwa ;

(xvii) Kutia sumu au silaha za sumu ;

(xviii) Kutumia gesi ya kuziba pumzi, yenye sumu au gesi za aina nyingine, na viowevu, vitu au zana nyingine zote za aina hiyo ;

(xix) Utumiaji wa risasi zenye kupanuka au kujisambaza kwa urahisi ndani ya mwili, kama vile risasi ambayo ganda lake gumu halifuniki kiini chote au limetiwa mitai ;

Copyright © STIC 2010

(xx) Utumiaji wa silaha, vitupo, vitu au mbinu za vita ambazo zinasababisha maumivu yasiyohitajika au yasiyo ya lazima, au kupiga bila kuchagua kinyume cha sheria za kimataifa zinazohusu migogoro ya kivita, ilimradi tu silaha hizo, vitupo hivyo, vitu hivyo au mbinu hizo za vita ziwe zimekatazwa kwa jumla na kuandikwa kwenye kiambatisho cha Mkataba huu, kwa kufanyiwa marekebisho kwa mujibu wa vipengele husika vilivyoainishwa katika ibara 121 na 123 ;

(xxi) Kumfanyia mtu kitendo cha kikatili cha kumvunjia heshima, hasa kitendo cha kumdhalilisha na kumshushia hadhi yake ;

(xxii) Ubakaji, utumwa wa ngono, ukahaba wa kulazimishwa, mimba ya kulazimishwa, kama inavyofafanuliwa katika ibara 7, aya 2 (f), kuhasi kwa nguvu au aina nyingine yoyote ya ukatili wa kingono ambao pia ni ukiukaji mkubwa wa Mikataba ya Geneva ;

(xxiii) Kutumia kuwepo kwa raia au mtu yeyote anayelindwa, ili kufanya baadhi ya vituo, maeneo au vikosi vya kijeshi visiathirike na operesheni za kijeshi ;

(xxiv) Kuelekeza kwa makusudi mashambulio dhidi ya majengo, vifaa, vituo vya matibabu na magari ya usafirishaji, wafanyakazi wanaotumia nembo zinazotambulika za Mikataba ya Geneva kwa kulingana na sheria za kimataifa ;

(xxv) Kunyima raia chakula kwa makusudi, ikiwa ni mbinu ya kivita, kwa kuwanyima bidhaa za lazima za maisha, ikiwa ni pamoja na kuzuia kwa makusudi misaada ya kuwapunguzia watu dhiki inayotajwa chini ya Mikataba ya Geneva ;

(xxvi) Kuingiza kwa nguvu au kuandikisha kwenye jeshi la taifa watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 au kuwatumia kikamilifu kwenye uhasama ;

Copyright © STIC 2010

(c) Unapotokea mgogoro wa kivita ambao hauna sura ya kimataifa, ukiukaji mkubwa wa ibara 3 inayohusu Mikataba yote minne ya Geneva ya tarehe 12 Agosti 1949, ambayo ni chochote cha vitendo vifuatavyo kilichofanywa dhidi ya watu wasioshiriki kikamilifu katika uhasama, ikiwa ni pamoja na wanajeshi walioweka silaha zao chini na wale wasioweza kupigana tena kwa sababu ya maradhi, majeraha, kuwekwa kizuizini au sababu nyingine yoyote :

(i) Ukatili dhidi ya maisha na mtu, hususan mauaji ya aina zote, kukata kiungo cha mwili, utendeaji wa kikatili na mateso ;

(ii) Kumfanyia mtu kitendo cha kikatili cha kumvunjia heshima, hasa kitendo cha kumdhalilisha na kumshushia hadhi yake ;

(iii) Kuteka watu nyara ;

(iv) Utoaji wa adhabu na unyongaji bila hukumu iliyotolewa na mahakama iliyoundwa kihalali, yenye kutoa haki zote za kimahakama ambazo zinatambulika kuwa ni za lazima.

(d) Aya 2 (c) inahusu migogoro ya kivita ambayo haina sura ya kimataifa na kwa hivyo haihusiani na vurugu za ndani ya Nchi kama vile ghasia, vitendo vya vurugu vya hapa na pale au vitendo vya aina kama hiyo ;

(e) Ukiukaji mwingine mkubwa wa sheria na desturi zinazohusiana na migogoro ya kivita ambayo haina sura ya kimataifa, kwa mfumo wenye kutambulika kwa sheria za kimataifa, yaani mojawapo ya vitendo vifuatavyo :

(i) Kuelekeza kwa makusudi mashambulio dhidi ya raia kwa kuwa raia tu, au dhidi ya raia mmoja mmoja wasioshiriki moja kwa moja kwenye uhasama ;

Copyright © STIC 2010

(ii) Kuelekeza kwa makusudi mashambulio dhidi ya majengo, vifaa, vituo vya matibabu na magari ya usafirishaji, wafanyakazi wanaotumia nembo zinazotambulika za Mikataba ya Geneva kwa kulingana na sheria za kimataifa ;

(iii) Kuelekeza mashambulio kwa makusudi dhidi ya watumishi, majengo, vifaa, vitengo au magari yanayotumiwa kwa huduma na msaada wa kibinadamu au kikosi cha kulinda amani, kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ilimradi tu wanastahili ulinzi wanaopewa raia au vitu vya kiraia chini ya sheria za kimataifa zinazohusiana na mgogoro wa kivita ;

(iv) Kuelekeza kwa makusudi mashambulio dhidi ya majengo ya kidini, ya elimu, sanaa, sayansi au ya kutoa misaada, minara ya kihistoria, hospitali na mahali wanamokusanywa wagonjwa na majeruhi, ilimradi tu si malengo ya kijeshi ;

(v) Uporaji wa mji au eneo, hata kama panashambuliwa ;

(vi) Ubakaji, utumwa wa ngono, ukahaba wa kulazimishwa, mimba ya kulazimishwa, kama inavyofafanuliwa katika ibara 7, aya 2 (f), kuhasi kwa nguvu, ukatili wa kingono ambao ni ukiukaji mkubwa wa ibara 3 inayohusu Mikataba yote minne ya Geneva ;

(vii) Kuingiza kwa nguvu au kuandikisha kwenye jeshi au vikundi vyenye silaha watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 au kuwashirikisha kikamilifu kwenye uhasama ;

(viii) Kuamuru kuhamishwa kwa raia kwa sababu zinazohusiana na mgogoro huo, isipokuwa kama usalama wa raia hao au sababu za kijeshi zinalazimisha kitendo hicho ;

Copyright © STIC 2010

(ix) Kuua au kujeruhi kiusaliti mpiganaji wa upande wa upinzani ;

(x) Kutangaza kuuliwa kila mtu ;

(xi) Kukatakata viungo vya miili ya watu walio chini ya utawala wa upande wa upinzani au kuwafanyia majaribio ya tiba au ya kisayansi ya namna yoyote ambayo hayahusiani na matibabu, tiba ya meno au ya kihospitali ya mtu anayehusika wala hayafanywi kwa maslahi yake na yenye kusababisha kifo au kuhatarisha sana afya ya mtu au watu hao ;

(xii) Kuharibu au kuteka rasilimali za adui, isipokuwa kama uharibifu au utekaji huo unalazimishwa na mahitaji yanayotokana na mgogoro ;

(f) Aya ya 2 (c) inahusu migogoro ya kivita ambayo haina sura ya kimataifa na kwa hivyo haihusiani na vurugu za ndani

ya Nchi kama vile ghasia, vitendo vya vurugu vya hapa na pale au vitendo vya aina kama hiyo. Inahusiana na migogoro ya kivita inayotokea katika eneo la Nchi lenye mgogoro wa muda mrefu wa kutumia silaha kati ya serikali na makundi yenye silaha yaliyojiandaa au kati ya makundi kama hayo.

3. Hakuna chochote katika aya 2 (c) na (e) ambacho kitaathiri jukumu la serikali kudhibiti au kurejesha sheria na utulivu ndani ya Nchi, au kulinda umoja na hadhi ya eneo la Nchi hiyo kwa kutumia njia zote halali.

Ibara 9
Viambato vya makosa ya jinai

1. Viambato vya makosa ya jinai vitasaidia Mahakama kufasiri na kutumia ibara 6, 7 na 8. Vitathibitishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

2. Marekebisho ya viambato vya makosa ya jinai yanaweza kupendekezwa na :

    (a) Nchi yoyote kati ya zile zinazounda Mahakama ;

    (b) Majaji, wakifanya hivyo kwa wingi ulio dhahiri ;

    (c) Mwendesha Mashtaka.

Marekebisho hayo yatathibitishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

3. Viambato vya makosa ya jinai pamoja na marekebisho yake vitalingana na Mkataba huu.

Ibara 10

Hakuna chochote katika Sehemu hii kitakachofasiriwa kwa namna ya kupunguza au kuathiri kwa namna yoyote kanuni za sheria za kimataifa zilizopo au zilizo njiani kuundwa kwa madhumuni yaliyo nje ya Mkataba huu.

Copyright © STIC 2010

Ibara 11
Uwezo wa kisheria *ratione temporis*

1. Mahakama ina uwezo wa kisheria kwa yale makosa ya jinai yaliyotendwa baada ya kuanza kutumika kwa Mkataba huu tu.

2. Nchi inapokuwa mojawapo ya zile zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu baada ya kuanza kutumika kwake, Mahakama inaweza kutumia uwezo wake wa kisheria kwa yale makosa ya jinai yaliyotendwa baada ya kuanza kutumika kwa Mkataba huu tu, isipokuwa kama serikali hiyo imetoa tamko kulingana na ibara 12, aya 3.

Ibara 12
Masharti ya kutumia uwezo wa kisheria

1. Nchi inayokuwa mojawapo ya zile zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu inakubali uwezo wa kisheria wa Mahakama kuhusiana na makosa ya jinai yaliyotajwa katika ibara 5.

Copyright © STIC 2010

2. Kuhusiana na ibara 13, aya (a) au (c), Mahakama inaweza kutumia uwezo wake wa kisheria ikiwa moja au zaidi ya Nchi zifuatazo ni mojawapo ya zile zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu au zikiwa zinaukubali uwezo wa kisheria wa Mahakama kwa mujibu wa aya 3 :

    (a) Nchi ambamo jambo linalochunguzwa lilitendwa, au kama kosa hilo la jinai lilitendwa kwenye chombo cha majini au ndani ya ndege, Nchi ambamo chombo hicho cha majini au ndege imesajiliwa ;

    (b) Nchi ya uraia wa mtu anayeshtakiwa kwa kutenda kosa la jinai.

3. Kama Nchi ambayo si mojawapo ya zile zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu inatakiwa kuukubali uwezo wa kisheria wa Mahakama chini ya aya 2, Nchi hiyo inaweza kukubali uwezo wa kisheria wa Mahakama kuhusiana na kosa husika la jinai kwa kutoa tamko litakalowasilishwa kwa Msajili wa Mahakama. Nchi iliyoukubali uwezo wa kisheria wa Mahakama itashirikiana na

Mahakama bila kukawia wala kuleta kipingamizi kwa mujibu wa Sehemu ya 9.

Ibara 13
Matumizi ya uwezo wa kisheria

Mahakama inaweza kutumia uwezo wake wa kisheria kuhusiana na kosa la jinai lililotajwa katika ibara 5, kwa mujibu wa vipengele vya Mkataba huu ikiwa :

(a) Hali ambamo kosa moja la jinai au zaidi linaonekana kuwa limetendwa inawasilishwa kwa Mwendesha Mashtaka na Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu, kwa mujibu wa ibara 14 ;

(b) Hali ambamo kosa moja la jinai au zaidi linaonekana kuwa limetendwa, inawasilishwa kwa Mwendesha Mashtaka na Baraza la Usalama likifanya chini ya Sura VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa ; au

Copyright © STIC 2010

(c) Mwendesha Mashtaka ameanzisha upelelezi kuhusiana na kosa hilo la jinai kwa mujibu wa ibara 15.

Ibara 14
Ombi la kuanzisha upelelezi kutoka kwa Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama

1. Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inaweza kupeleka kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka hali ambayo kosa moja la jinai au zaidi lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama linaonekana kuwa limetendwa, ili kuitaka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka kufanya upelelezi juu ya hali hiyo kwa madhumuni ya kuamua kama mtu mmoja mahususi au zaidi ya mmoja washtakiwe kwa kutenda makosa hayo ya jinai.

2. Kama itakavyoyumkinika, ombi litaelezea juu ya hali husika na kuambatishwa na nyaraka muhimu kama zitakavyoweza kupatikana na Nchi inayoomba kupelelezwa kwa hali hiyo.

Ibara 15
Mwendesha Mashtaka

1. Mwendesha Mashtaka anaweza kuanzisha upelelezi kwa hiari yake kufuatana na habari kuhusu makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama.

2. Mwendesha Mashtaka atachambua uzito wa habari alizopata. Kwa madhumuni hayo, anaweza kutafuta habari za ziada kutoka Nchi, vyombo vya Umoja wa Mataifa, mashirika baina ya serikali mbalimbali au yale yasiyokuwa ya kiserikali, au vyanzo vingine vya kuaminika ambavyo Mwendesha Mashtaka anaviona vinafaa, na anaweza kupokea maelezo ya maandishi au ya mdomo kwenye makao makuu ya Mahakama.

3. Ikiwa Mwendesha Mashtaka ataona kuwa kuna sababu za kutosha za kuanzisha upelelezi, atawasilisha kwenye Chumba cha Utangulizi ombi la kumruhusu kufanya upelelezi pamoja na vitu vingine vyovyote vya uthibitisho vilivyokusanywa. Waathiriwa wanaweza kutoa malalamiko yao mbele ya Chumba cha Utangulizi, kufuatana na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Copyright © STIC 2010

4. Ikiwa Chumba cha Utangulizi kitaamua kwamba kuna sababu za kutosha za kuanzisha upelelezi baada ya kuchunguza ombi na vitu vya kuthibitisha na kwamba kesi hiyo inaonekana kuwa ipo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, kitaidhinisha kuanza kwa upelelezi bila kuathiriwa na maamuzi yaliyopita ya Mahakama kuhusiana na kupelekwa kwenye Mahakama kwa kesi hiyo na kukubalika kwake.

5. Kukataa kwa Chumba cha Utangulizi kuidhinisha upelelezi hakutamzuia Mwendesha Mashtaka kutoa ombi jipya baadaye, kufuatana na habari au ushahidi mpya kuhusiana na hali hiyohiyo.

6. Ikiwa baada ya uchunguzi wa mwanzo unaotajwa katika aya 1 na 2, Mwendesha Mashtaka ataona kuwa habari zilizotolewa hazina sababu za kutosha za kuanzisha upelelezi, atawaarifu wale waliotoa habari hizo. Hii haitamzuia Mwendesha Mashtaka kupokea habari zaidi zitakazowasilishwa kwake kuhusiana na hali hiyo kutokana na habari au ushahidi mpya.

Ibara 16
Kuahirisha upelelezi au mashtaka

Hakuna upelelezi wowote au mashtaka yanayoweza kuanzishwa chini ya Mkataba huu mnamo kipindi cha miezi 12 inayofuata baada ya Baraza la Usalama kupitisha azimio chini ya Sura VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuiomba Mahakama kufanya hivyo ; ombi hilo linaweza kuletwa upya na Baraza katika hali hiyo hiyo.

Ibara 17
Masuala yanayohusu kukubalika

1. Kufuatana na aya 10 ya Dibaji na ibara 1, Mahakama itaamua kama kesi haikubaliki pale ambapo :

   (a) Kesi inafanyiwa upelelezi au mashtaka yake yanaendeshwa na Nchi ambayo ina uwezo wa kisheria kwa kesi hiyo, isipokuwa kama Nchi hiyo haitaki au haiwezi kikweli kweli kufanya upelelezi au kuendesha mashtaka ;

Copyright © STIC 2010

   (b) Kesi ilikwishawahi kufanyiwa upelelezi na Nchi ambayo ina uwezo nayo wa kisheria na Nchi hiyo imeamua kutomshtaki mhusika, isipokuwa kama uamuzi huo umetokana na Nchi kukataa au kutoweza kuendesha mashtaka kikweli kweli ;

   (c) Mhusika tayari alikwishahukumiwa kuhusu mwenendo uliosababisha malalamiko, na haruhusiwi kuhukumiwa na Mahakama chini ya ibara 20, aya 3 ;

   (d) Kesi haina uzito wa kutosha kiasi cha kuifanya Mahakama ichukue hatua za ziada.

2. Ili kuamua juu ya kukataa kwa Nchi kuhusu kesi fulani, Mahakama itazingatia, ikitilia maanani misingi ya utaratibu wa hivi sasa unaotambuliwa na sheria za kimataifa, ikiwapo moja au zaidi ya hali zifuatazo kama inavyofaa :

   (a) Kesi iliendeshwa au inaendeshwa au uamuzi wa kitaifa umetolewa kwa madhumuni ya kumlinda mhusika dhidi

ya dhima ya jinai kwa makosa ya jinai ambayo yapo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ulioelezwa katika ibara 5 ;

(b) Pamekuwepo na ucheleweshaji usiokubalika wa kuendesha kesi ambao katika hali kama hiyo haukubaliani na nia ya kumfikisha mhusika mbele ya sheria ;

(c) Kesi haikuendeshwa au haiendeshwi kwa uhuru au kwa kutopendelea upande wowote na inaendeshwa kwa namna ambayo haikubaliani na nia ya kumfikisha mhusika mbele ya sheria.

3. Ili kuamua kuwa Nchi haina uwezo wa kuendesha kesi fulani, Mahakama itafikiria kama ni kwa sababu ya kuvurugika kabisa au kutokuwepo kwa mfumo wa kitaifa wa kimahakama, Nchi haiwezi kumpata mshtakiwa au haiwezi kupata ushahidi na maelezo ya lazima au haina uwezo wa kuendesha kesi hiyo.

Copyright © STIC 2010

Ibara 18
Uamuzi wa awali kuhusu kukubalika

1. Wakati hali ikishaletwa mbele ya Mahakama kufuatana na ibara 13, (a), na Mwendesha Mashtaka akawa ameamua kwamba kuna sababu za kutosha za kuanzisha upelelezi, na wakati Mwendesha Mashtaka akianzisha upelelezi kufuatana na ibara 13 (c) na 15, Mwendesha Mashtaka atazijulisha Nchi zote zinazounda Mahakama pamoja na Nchi ambazo, kwa kutilia maanani taarifa zilizopo, zingeweza kutumia uwezo wao wa kisheria dhidi ya makosa ya jinai yanayohusika. Mwendesha Mashtaka anaweza kuziarifu Nchi hizo kwa siri, na akiona umuhimu wa kuwalinda watu, kuzuia kuharibu ushahidi au kuzuia kutoroka kwa watu, anaweza kubana kiasi fulani cha taarifa inayotolewa kwa Nchi.

2. Mnamo mwezi mmoja wa kupokea taarifa hiyo, Nchi inaweza kuiarifu Mahakama kwamba imeanzisha au ilianzisha upelelezi dhidi ya raia wake au watu wengine walio ndani ya uwezo wake wa kisheria kuhusiana na vitendo vya makosa ya jinai ambavyo vinaweza kuunda makosa ya jinai yanayotajwa katika ibara 5 ambayo yanahusiana na taarifa iliyopewa Nchi. Kwa ombi la Nchi, Mwendesha Mashtaka, anaweza kukubali Nchi hiyo ifanye

shughuli ya kuendesha upelelezi dhidi ya watu hao, isipokuwa pale Chumba cha Utangulizi, kwa ombi la Mwendesha Mashtaka, kinaamua kuidhinisha kufanyika kwa upelelezi huo.

3. Kuahirishwa huko kwa Mwendesha Mashtaka kwa Nchi kuendesha upelelezi kunaweza kutazamwa upya na Mwendesha Mashtaka miezi sita baada ya uamuzi huo, au wakati wowote yanapotokea mabadiliko ya kimsingi ya hali ya mambo kutokana na Nchi kukataa au kutokuwa na uwezo kikweli kweli wa kuendesha upelelezi huo.

4. Nchi inayohusika au Mwendesha Mashtaka wanaweza kukata rufaa kwa Chumba cha Rufaa dhidi ya uamuzi wa Chumba cha Utangulizi, kwa mujibu wa ibara 82. Rufaa hiyo inaweza kusikilizwa kwa haraka.

5. Mwendesha Mashtaka anapokubali kuahirisha upelelezi kwa mujibu wa aya 2, anaweza kuiomba Nchi inayohusika kumjulisha baada ya kila kipindi maalumu maendeleo ya upelelezi wake, na mashtaka mengine yoyote yatakayojitokeza baadaye. Nchi zinazounda Mahakama zitatakiwa kutoa majibu kuhusiana na maombi hayo bila ya kuchelewa.

Copyright © STIC 2010

6. Wakati akingojea uamuzi wa Chumba cha Utangulizi, au wakati wowote ambao Mwendesha Mashtaka ameahirisha upelelezi chini ya ibara hii, Mwendesha Mashtaka anaweza, katika hali ya kipekee, kuomba kibali kutoka Chumba cha Utangulizi ili kufuatilia hatua muhimu za upelelezi kwa madhumuni ya kuhifadhi ushahidi, mahali ambapo pana fursa ya kipekee ya kupata ushahidi muhimu au kama kuna hatari kubwa ya kuwa ushahidi huo hautapatikana baadaye.

7. Nchi ambayo iliweka pingamizi kuhusiana na uamuzi wa Chumba cha Utangulizi chini ya ibara hii inaweza kukataa kukubalika kwa kesi chini ya ibara 19, kwa misingi ya kupatikana kwa taarifa muhimu za ziada au mabadiliko makubwa ya hali ya mambo.

Ibara 19
Kupinga uwezo wa kisheria wa Mahakama au kukubalika kwa kesi

1. Mahakama itahakikisha kwamba ina uwezo wa kisheria wa kusikiliza kila kesi ambayo inaletwa mbele yake. Mahakama inaweza kwa hiari yake yenyewe kuamua kuhusu kukubalika kwa kesi kwa mujibu wa ibara 17.

2. Pingamizi kuhusiana na kukubalika kwa kesi kufuatana na sababu zilizotajwa katika ibara 17 au pingamizi kuhusu uwezo wa kisheria wa Mahakana kunaweza kufanywa na :

   (a) Mshtakiwa au mtu ambaye hati ya kukamata au samansi imetolewa kwa mujibu wa ibara 58 ;

   (b) Nchi ambayo ina uwezo wa kisheria juu ya kesi, kutokana na kwamba inafanya upelelezi au inaendesha kesi hiyo, au ilifanya upelelezi au iliendesha kesi hiyo ; au

   (c) Nchi ambayo inahitaji kuukubali uwezo wa kisheria wa Mahakama chini ya ibara 12.

3. Mwendesha Mashtaka anaweza kuomba Mahakama kuamua kuhusu suala la uwezo wa kisheria au kukubalika. Katika taratibu zinazohusu uwezo wa kisheria au kukubalika, wale waliopeleka maelezo ya hali husika chini ya ibara 13, na waathiriwa, wanaweza pia kutoa maoni yao kwa Mahakama.

4. Kukubalika kwa kesi au uwezo wa kisheria wa Mahakama vinaweza kupingwa mara moja tu na Nchi au mtu yeyote aliyetajwa katika aya 2. Kupinga kunapaswa kufanyike kabla au wakati wa kuanzisha kesi. Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Mahakama inaweza kuruhusu ombi la kupinga liwasilishwe zaidi ya mara moja au baada ya kuanza kesi. Maombi ya kupinga kukubalika kwa kesi yanayowasilishwa wakati wa kuanza kesi, au baadaye kwa kupata ruhusa ya Mahakama, yatategemezwa kwenye ibara 17, aya 1 (c) tu.

Copyright © SFIC 2010

5. Nchi zilizotajwa katika aya 2 (b) na (c), zitaweka pingamizi mapema iwezekanavyo.

6. Kabla ya kuthibitishwa kwa mashtaka, maombi ya pingamizi dhidi ya kukubalika kwa kesi au dhidi ya uwezo wa kisheria yatatumwa Chumba cha Utangulizi. Baada ya kuthibitishwa kwa mashtaka, yatatumwa Chumba cha Kesi. Maamuzi kuhusu uwezo wa kisheria na kukubalika kwa kesi yanaweza kukatiwa rufaa kwenye Chumba cha Rufaa kwa mujibu wa ibara 82.

7. Kama ombi la kuweka pingamizi linatolewa na Nchi inayotajwa na aya 2, (b) au (c), Mwendesha Mashtaka atasimamisha upelelezi hadi hapo Mahakama itakapoamua kwa mujibu wa ibara 17.

8. Wakati akisubiri uamuzi wa Mahakama, Mwendesha Mashtaka anaweza kuomba kibali cha Mahakama :

   (a) Kufuatilia hatua muhimu za upelelezi kama zile zilizotajwa na ibara 18, aya 6 ;

   (b) Kuchukua taarifa au maelezo kutoka kwa shahidi au kukamilisha ukusanyaji na uchunguzi wa ushahidi ulioanza kabla ya kuwekwa kwa pingamizi ; na

   (c) Kwa kushirikiana na Nchi husika, kuzuia kutoroka kwa watu ambao Mwendesha Mashtaka amekwishaomba kutolewa hati ya kukamata chini ya ibara 58.

9. Pingamizi lolote halitaathiri kutambulika kwa kitendo chochote cha Mwendesha Mashtaka au agizo lolote au hati yoyote ya kukamata iliyotolewa na Mahakama kabla ya kuwekwa kwa pingamizi.

10. Ikiwa Mahakama imeamua kuwa kesi haikubaliki chini ya ibara 17, Mwendesha Mashtaka anaweza kuiomba Mahakama kuutazama upya uamuzi wake, kama zimepatikana taarifa zaidi ambazo zinakanusha sababu zilizoifanya kesi isikubalike hapo awali chini ya ibara 17.

11. Kufuatana na masuala yanayotajwa katika ibara 17, kama Mwendesha Mashtaka anahairisha upelelezi, anaweza kuiomba Nchi inayohusika kumpatia taarifa zinazohusu uendeshaji wa kesi

Copyright © STIC 2010

hiyo. Taarifa hizo zinakuwa ni siri kwa maombi ya Nchi husika. Ikiwa Mwendesha Mashtaka baada ya hapo ataamua kuanza upelelezi, ataiarifu Nchi ambayo iliomba kuahirishwa huko.

Ibara 20
Ne bis in idem

1. Isipokuwa kama ilivyoonyeshwa katika Mkataba huu, hakuna mtu anayeweza kuhukumiwa na Mahakama kwa vitendo vinavyounda makosa ya jinai ambayo alikwisha kupatikana na hatia au kukutwa hana hatia na Mahakama.

2. Hakuna mtu atakayehukumiwa na mahakama nyingine kwa kosa la jinai lililotajwa katika ibara 5, kosa ambalo mtu huyo amekwisha kupatikana na hatia au kukutwa hana hatia na Mahakama.

3. Mtu yeyote aliyehukumiwa na mahakama nyingine kwa mwenendo unaohusiana na ibara 6, 7 au 8 anaweza tu kuhukumiwa na Mahakama kwa mwenendo huo huo, isipokuwa kama uendeshaji wa kesi hiyo katika Mahakama nyingine :

   (a) Ulilenga kumlinda mhusika asiwajibike kwa makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ; au

   (b) Haukufanywa katika hali ya kuwa huru au bila upendeleo kwa mujibu wa maadili ya utaratibu unaokubalika na sheria za kimataifa, na kuendeshwa kwa namna ambayo, katika hali hiyo, ulikuwa kinyume na nia ya kumfikisha mtu huyo mahakamani.

Copyright © STTC 2010

Ibara 21
Sheria inayotumika

1. Mahakama itatumia :

   (a) Kwanza, Mkataba huu, Viambato vya Makosa ya Jinai na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi ;

   (b) Pili, panapofaa, mikataba inayotumika na misingi na kanuni ya sheria za kimataifa, ikiwa ni pamoja na misingi ya sheria za kimataifa zinazohusu migogoro ya kivita ;

(c) Kama si hivyo, misingi ya jumla ya sheria ambazo zimechukuliwa na Mahakama kutoka kwenye sheria za kitaifa zenye kufuata mifumo ya sheria za ulimwengu, ikiwa ni pamoja na, panapofaa, sheria za kitaifa za Nchi ambazo zina uwezo wa kisheria kwa kosa hilo la jinai, ilimradi tu misingi hiyo haipingani na Mkataba huu na sheria za kimataifa, na kaida na viwango vinavyotambulika kimataifa.

2. Mahakama inaweza kutumia misingi na kanuni za sheria kama zilivyofasiriwa katika maamuzi yaliyotangulia.

3. Matumizi na fasiri ya sheria kufuatana na ibara hii vinapaswa kuwiana na haki za binadamu zinazokubalika kimataifa, na zisiwe na ubaguzi wowote unaotokana na sababu za kijinsia kama inavyofafanuliwa katika ibara 7, aya 3, umri, kabila, rangi, lugha, dini au imani, mawazo ya kisiasa au mawazo mengine, utaifa, asili ya kikabila au kijamii, mali, kuzaliwa au hadhi nyingine yoyote.

Copyright © STIC 2010

Sehemu III Misingi ya jumla ya sheria za makosa ya jinai

Ibara 22
Nullum crimen sine lege

1. Chini ya Mkatabu huu, mtu anakuwa tu na dhima ya kosa la jinai kama kitendo kinachotiliwa shaka wakati wa kukitenda, kitakuwa kimeshaainishwa kuwa ni kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama.

2. Ufafanuzi wa kosa la jinai utafasiriwa kama ulivyo na hauwezi kunyumbuliwa kwa mfanano. Endapo kutakuwa na utata, ufafanuzi huo utafasiriwa kwa maslahi ya mtu ambaye anafanyiwa upelelezi, anayeshtakiwa au aliyepatika na hatia.

3. Ibara hii haitaathiri ubainishaji wa mwenendo wowote kuwa kosa la jinai chini ya sheria za kimataifa, bila kutegemea Mkataba huu.

Copyright © STIC 2010

Ibara 23
Nulla poena sine lege

Mtu alipatika na hatia na Mahakama anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa Mkataba huu tu.

Ibara 24
Kutorudi nyuma *ratione personae*

1. Chini ya Mkataba huu, hapana mtu atakayekuwa na dhima ya kosa la jinai kwa kitendo kilichofanywa kabla ya Mkataba huu kuanza kutumika.

2. Kama sheria inayotumika katika kesi fulani imebadilishwa kabla ya hukumu ya mwisho, sheria yenye maslahi kwa mtu ambaye anafanyiwa upelelezi, anayeshtakiwa au anayepatikana na hatia ndiyo itakayotumika.

Ibara 25
Dhima binafsi ya kosa la jinai

1. Mahakama itakuwa na uwezo wa kisheria kwa watu kufuatana na Mkataba huu.

2. Mtu anayetenda kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama yeye binafsi ndiye atakayekuwa na dhima ya kosa la jinai na atastahili kuadhibiwa kwa mujibu wa Mkataba huu.

3. Kwa mujibu wa Mkataba huu, mtu atakuwa na dhima ya kosa la jinai na atastahili kuadhibiwa kwa kosa hilo la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama kama mtu huyo :

   (a) Anatenda kosa la jinai kama hilo, akiwa yeye binafsi, au kwa kushirikiana na mtu mwingine au kwa kupitia mtu mwingine bila ya kujali kama mtu huyo mwingine ana dhima ya kosa la jinai ;

   Copyright © SIIC 2010

   (b) Anaamuru, anashauri au anachochea utendaji wa kosa la jinai kama hilo, ambalo limetendwa kweli kweli au linajaribiwa kutendwa ;

   (c) Kwa madhumuni ya kuwezesha kutendwa kwa kosa la jinai kama hilo, kusaidia na kuhamasisha au kusaidia katika kutendwa kosa hilo au kujaribu kulitenda, ikiwa ni pamoja na kutoa nyenzo za kutendea kosa hilo ;

   (d) Anachangia kwa njia yoyote nyingine katika kutenda au kujaribu kutenda kosa la jinai kama hilo linalofanywa na kikundi cha watu wenye dhamira moja. Mchango huo unapaswa kuwa wa makusudi na utafanywa ama :

      (i) Kwa nia ya kuendeleza kitendo hicho cha uhalifu au kwa madhumuni ya kihalifu ya kikundi hicho pale ambapo kitendo hicho au madhumuni hayo yanajumuisha kutendwa kwa kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ; au

(ii) Kufanywa kwa kuelewa nia ya kikundi hicho ya kutenda kosa hilo la jinai ;

(e) Kuhusiana na kosa la jinai la mauaji ya kimbari, kuwachochea watu wengine moja kwa moja na waziwazi kufanya mauaji ya kimbari ;

(f) Anajaribu kutenda kosa la jinai kama hilo ambalo utendaji wake unaanza kwa kuchukua hatua kubwa lakini kosa lenyewe la jinai halitokei kwa sababu ya mazingira yaliyo nje ya uwezo wa matakwa ya mtu huyo. Hata hivyo mtu anayeghairi nia yake ya kutenda kosa la jinai au kuzuia kukamilika kwa kosa hilo hatastahili kuadhibiwa chini ya Mkataba huu kwa jaribio lake la kutaka kutenda kosa la jinai ikiwa mtu huyo, kwa hiari yake, aliacha kabisa utendaji wa kosa hilo la jinai.

4. Hakuna kipengele hata kimoja cha Mkataba huu kinachohusu dhima binafsi ya kutenda kosa la jinai ambacho kitaathiri jukumu la Nchi chini ya sheria za kimataifa.

Copyright © STIC 2010

Ibara 26
Kutokuwa na uwezo wa kisheria kwa watu wenye umri chini ya miaka kumi na nane

Mahakama haitakuwa na uwezo wa kisheria kwa mtu yeyote aliyekuwa na umri wa chini ya miaka 18 wakati wa kutenda kosa la jinai analodaiwa kutenda.

Ibara 27
Kutojali madaraka yanayoambatana na cheo

1. Mkataba huu utahusu watu wote bila kujali tofauti za madaraka yao rasmi. Zaidi hasa madaraka rasmi kama vile Mkuu wa Nchi au serikali, Mtendaji Mkuu wa serikali au mbunge, mwakilishi aliyechaguliwa au mtumishi wa serikali hautamsamehe mtu kwa namna yoyote ile dhima ya kosa la jinai chini ya Mkataba huu, wala wadhifa huo hautakuwa ndiyo sababu ya kumpunguzia adhabu.

2. Kinga au kanuni za utaratibu maalumu zinazoambatana na wadhifa rasmi wa mtu, zikiwa ama chini ya sheria za kitaifa au za kimataifa, hazitaizuia Mahakama kutekeleza wajibu wake wa kisheria kwa mtu huyo.

Ibara 28
Dhima ya makamanda wa kijeshi au wakuu wengine

Zaidi ya sababu nyingine za dhima ya kosa la jinai chini ya Mkataba huu kwa makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama :

(a) Kamanda wa kijeshi au mtu anayekaimu nafasi ya kamanda wa kijeshi atakuwa na dhima ya kosa la jinai kwa makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ambayo yametendwa na vikosi vilivyo chini ya uongozi wake, au chini ya uongozi na udhibiti wake vyovyote itakavyokuwa ; kutokana na kushindwa kwake kudhibiti vikosi hivyo vilivyo, pale :

(i) Kamanda wa kijeshi au mtu anayekaimu nafasi hiyo ama alijua, au, mintarafu ya mazingira yaliyokuwepo wakati huo alipaswa ajue kuwa vikosi hivyo vilikuwa vinatenda au vinakaribia kutenda kosa hilo la jinai ; na

(ii) Kamanda wa kijeshi au mtu anayekaimu ameshindwa kuchukua hatua zinazofaa zilizo ndani ya uwezo wake kuzuia au kukomesha utendaji wa makosa ya jinai au kuwajulisha jambo hilo wakuu wanaohusika ili waanzishe upelelezi na kufungua mashtaka.

(b) Kuhusu uhusiano kati ya mkubwa na wasaidizi usioelezwa katika aya (a), mkubwa atakuwa na dhima ya makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama yaliyotendwa na wasaidizi wake walio chini ya uwezo na udhibiti wake kutokana na kushindwa kwake kutumia madaraka aliyonayo ya kuwadhibiti sawasawa wasaidizi wake hao, pale :

Copyright © STIC 2010

(i) Mkubwa huyo ama alijua au kwa makusudi alidharau taarifa ilizoashiria waziwazi kwamba wasaidizi wake wamekuwa wakitenda au wanakaribia kutenda makosa hayo ya jinai ;

(ii) Makosa hayo ya jinai yalihusu shughuli ambazo zilikuwa chini ya madaraka na udhibiti wa mkubwa huyo ; na

(iii) Mkubwa huyo ameshindwa kuchukua hatua za lazima na za kufaa zilizo ndani ya uwezo wake kuzuia au kukomesha utendaji wa vitendo hivyo au ameshindwa kuwajulisha wakubwa wanaohusika ili ufanywe upelelezi na kufungua mashtaka.

Ibara 29
Kutotumika kwa sheria inayoweka kikomo cha muda ambao kesi inaweza kufikishwa kwenye Mahakama

Copyright © STIC 2010

Makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama hayatahusishwa na sheria inayoweka kikomo cha muda ambao kesi inaweza kufikishwa kwenye Mahakama.

Ibara 30
Kiambato cha kisaikolojia

1. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, mtu atakuwa na dhima ya kosa la jinai na atastahili kuadhibiwa kwa kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama pale tu vitendo hivyo vinapokuwa vimetendwa kwa kudhamiria na kwa kujua.

2. Kwa madhumuni ya ibara hii, mtu anakuwa amedhamiria pale :

    (a) Kuhusiana na mwenendo fulani, mtu amedhamiria kuwa katika mwenendo huo ;

    (b) Kuhusiana na matokeo, mtu anadhamiria kusababisha matokeo hayo au anajua kuwa yatatokea kutokana na hali ya kawaida ya matukio.

3. Kwa madhumuni ya ibara hii, "kujua" inamaanisha kuelewa kuwa hali fulani ipo au matokeo fulani yatatokea katika hali ya kawaida ya matukio. "Kujua" na "kwa kujua" yatatafsiriwa vile itakavyoonekana inafaa.

Ibara 31
Sababu za kusamehewa dhima ya kosa la jinai

1. Zaidi ya sababu nyingine za kusamehewa dhima ya kosa la jinai zilizotajwa katika Mkataba huu, mtu hatakuwa na dhima ya kosa la jinai endapo wakati wa mwenendo :

    (a) Mtu huyo anaumwa maradhi ya akili au ana upungufu wa akili ambao unaharibu uwezo wake wa kubaini uvunjaji wake wa sheria au tabia ya mwenendo wake au uwezo wake wa kujizuia ili mwenendo wake ulingane na matakwa ya sheria ;

    (b) Mtu huyo yupo katika hali ya kulewa ambayo inaharibu uwezo wake wa kubaini uvunjaji wake wa sheria au tabia ya mwenendo wake au uwezo wake wa kujizuia ili mwenendo wake ulingane na matakwa ya sheria, isipokuwa kama mtu huyo amelewa kwa makusudi katika hali hiyo akijua, au amedharau ukweli kuwa, kutokana na kulewa kwake, ulikuwepo uwezekano wa kujiingiza katika mwenendo wa kutenda kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ;

    (c) Mtu huyo anatenda hivyo kwa kuelewa, kwa madhumuni ya kujilinda au kumlinda mtu mwingine, na kwa makosa ya jinai ya kivita, rasilimali ambayo ni muhimu kwa maisha ya mtu huyo au mtu mwingine au rasilimali iliyo muhimu katika kutekeleza shughuli ya kijeshi dhidi ya matumizi haramu, ya nguvu, yanayotarajiwa katika muda mfupi ujao, kwa namna inayolingana na ukubwa wa hatari inayomkabili mtu huyo au mtu mwingine au mali inayolindwa. Ukweli kuwa mtu huyo alikuwa katika kitendo cha kujilinda kilichofanywa kwa kutumia majeshi, haitakuwa ndiyo sababu ya kumsamehe dhima ya kosa la jinai chini ya aya hii ndogo ;

Copyright © STIC 2010

(d) Mwenendo ambao unadaiwa kuwa ni kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama umesababishwa na tishio la kifo kinachotarajiwa katika muda mfupi ujao au maumivu makubwa ya mwili ya kuendelea yanayotarajiwa katika muda mfupi ujao dhidi ya mtu huyo au mtu mwingine, na mtu huyo anachukua hatua zinazohitajika na zinazofaa ili kuepuka tishio hilo, ilimradi tu mtu huyo hadhamirii kusababisha madhara makubwa kuliko yale anayotaka kuyaepuka. Tishio kama hilo linaweza kuwa ama :

(i) Limetendwa na watu wengine ; au

(ii) Limeundwa na hali nyingine ambazo zipo nje ya uwezo wa mtu kujizuia.

2. Mahakama itaamua kuhusu kukubalika kwa sababu za kusamehewa dhima ya kosa la jinai kama ilivyoelezwa katika Mkataba huu kwa kesi iliyo mbele yake.

Copyright © STIC 2010

3. Wakati wa kesi, Mahakama inaweza kuzingatia sababu za kusamehe dhima ya kosa la jinai mbali na zile zilizotajwa katika aya 1, ikiwa sababu hiyo itatokana na sheria inayotumika kama ilivyotajwa katika ibara 21. Utaratibu unaohusiana na kufikiria sababu hiyo utatokana na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Ibara 32
Kosa la ukweli au kosa la kisheria

1. Kosa la ukweli litakuwa ni sababu ya kusamehe dhima ya kosa la jinai pale tu linapotangua kiambato cha kisaikolojia kinachohitajika kwa kosa la jinai.

2. Kosa la kisheria ikiwa mwenendo fulani ni kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama hakutakuwa na sababu ya kusamehe dhima ya kosa la jinai. Hata hivyo, kosa la kisheria linaweza kuwa ni sababu ya kusamehe dhima ya kosa la jinai ikiwa linatangua kiambato cha kisaikolojia kinachohitajika kwa kosa la jinai kama hilo, au kama ilivyoelezwa katika ibara 33.

Ibara 33
Amri kutoka ngazi za juu na maagizo ya sheria

1. Ile kwamba kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama lilitendwa na mtu kufuatana na amri ya serikali au ya mkuu, awe wa kijeshi au wa kiraia, haimwondolei mtu huyo dhima ya kosa la jinai, isipokuwa kama :

   (a) Mtu huyo alikuwa na wajibu wa kisheria kutii amri za serikali au za mkuu anayehusika ;

   (b) Mtu huyo hakujua kuwa amri hiyo ilikuwa kinyume cha sheria ; na

   (c) Amri hiyo haikuonekana wazi kabisa kuwa ni kinyume cha sheria.

2. Kwa madhumuni ya ibara hii, amri ya kutekeleza mauaji ya kimbari au makosa ya jinai dhidi ya ubinadamu ni wazi kabisa kuwa ni kinyume cha sheria.

Copyright © SliC 2010

Sehemu IV Muundo na utawala wa Mahakama

Ibara 34
Vyombo vya Mahakama

Mahakama itaundwa na vyombo vifuatavyo :

(a) Ofisi ya Rais ;

(b) Tawi la Rufaa, Tawi la Kesi na Tawi la Utangulizi ;

(c) Ofisi ya Mwendesha Mashtaka ;

(d) Ofisi ya Msajili.

Ibara 35
Kazi za majaji

Copyright © STIC 2010

1. Majaji wote watachaguliwa kuwa wafanyakazi wa muda wote wa Mahakama na watakuwepo kwa kufanya kazi hiyo mara baada ya kuanza kufanya kazi.

2. Majaji wanaounda Ofisi ya Rais watafanya kazi kwa muda wote mara baada ya kuchaguliwa.

3. Kutokana na uzito wa kazi na kwa kujadiliana na majaji wengine, Ofisi ya Rais inaweza mara kwa mara kuamua ni kwa muda gani majaji waliobakia watatakiwa kufanya kazi kwa muda wote. Utaratibu wowote wa namna hiyo hautaathiri ibara 40.

4. Utaratibu wa fedha kwa majaji ambao hawatatakiwa kufanya kazi kwa muda wote utakuwa ni kwa mujibu wa ibara 49.

Ibara 36
Sifa, uteuzi na uchaguzi wa majaji

1. Kwa kutegemea vipengele vya aya 2, Mahakama itakuwa na majaji 18.

2. (a) Ikitenda kwa niaba ya Mahakama, Ofisi ya Rais inaweza kupendekeza kuongeza idadi ya majaji iliyoainishwa

katika aya 1, ikifafanua sababu kwa nini kuongezwa huko ni lazima na kunafaa. Msajili atasambaza haraka sana pendekezo lolote la aina hiyo kwa Nchi zote zinazounda Mahakama.

(b) Pendekezo lolote la aina hiyo litajadiliwa katika mkutano wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama utakaoitishwa kwa mujibu wa ibara 112. Pendekezo hilo litachukuliwa kuwa limeidhinishwa ikiwa litakubaliwa katika mkutano huo kwa wingi wa theluthi mbili ya kura za wajumbe wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Litaanza kutumika muda ambao utaamuliwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

(c) (i) Mara tu pendekezo la kuongeza idadi ya majaji likishakubaliwa chini ya aya ndogo (b), uchaguzi wa majaji wa ziada utafanywa kwenye mkutano unaofuata wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, kwa mujibu wa aya 3 hadi 8, na ibara 37, aya 2 ;

Copyright © STIC 2010

(ii) Mara baada ya pendekezo la kuongeza idadi ya majaji kukubaliwa na kutekelezwa chini ya aya ndogo (b) na (c) (i), Ofisi ya Rais itapendekeza baadaye wakati wowote, ikiwa kazi ya Mahakama itaonyesha haja ya kupunguza idadi ya majaji, ilimradi tu idadi hiyo haitakuwa chini ya idadi iliyoelezewa katika aya 1. Pendekezo litachunguzwa kwa mujibu wa utaratibu uliotajwa katika aya ndogo (a) na (b). Ikiwa litakubaliwa, idadi ya majaji itapunguzwa kila muda wa jaji unapomalizika, hadi pale idadi inayohitajika inapofikiwa.

3. (a) Majaji watachaguliwa miongoni mwa watu wenye maadili mema, wasiokuwa na upendeleo, na wenye hadhi na sifa zinazohitajika katika Nchi zao ili kuteuliwa katika ngazi za juu za utumishi wa kimahakama.

(b) Kila mgombea uchaguzi kwenye Mahakama anapaswa :

(i) Kuwa na ustadi katika sheria za makosa ya jinai na utaratibu wa kesi za mokosa ya jinai, pia uzoefu unaohitajika wa kuwa jaji, Mwendesha Mashtaka au wakili, au uwezo mwingine wowote kama huo, katika taratibu za kuendesha kesi za makosa ya jinai ; au

(ii) Kuwa na ustadi mkubwa katika nyanja za sheria za kimataifa, kama vile sheria ya kimataifa ya ubinadamu na sheria ya haki za binadamu, pia kuwa na uzoefu mkubwa katika fani ya taaluma ya kisheria ambayo inahusiana na kazi za kimahakama za Mahakama ;

(c) Kila mgombea uchaguzi kwenye Mahakama atapaswa kujua na kutumia vizuri angalau moja kati ya lugha za kazi za Mahakama.

Copyright © STIC 2010

4. (a) Uteuzi wa wagombea uchaguzi kwenye Mahakama unaweza kufanywa na Nchi yoyote kati ya zile zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu na utafanywa ama :

(i) Kufuatana na utaratibu wa uteuzi wa wagombea kwa ajili ya kuajiri watumishi wa ngazi za juu za kimahakama katika Nchi husika ; au

(ii) Kufuatana na utaratibu wa uteuzi wa wagombea wa Mahakama ya Haki ya Kimataifa unaotajwa katika Mkataba wa Mahakama hiyo.

Uteuzi utaambatanishwa na maelezo muhimu juu ya namna mgombea atakavyotekeleza mahitaji yaliyoainishwa katika aya 3.

(b) Kila Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inaweza kupendekeza jina moja la mgombea kwa uchaguzi fulani ambaye si lazima awe raia wa Nchi inayompendekeza lakini anapaswa kuwa raia wa Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama.

(c) Baraza la Nchi zinazounda Mahakama linaweza kuamua kuunda, kama kuna umuhimu wa kufanya hivyo, Kamati

ya Ushauri juu ya uteuzi. Katika hali hiyo, muundo na madaraka ya Kamati vitatengenezwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

5. Kwa madhumuni ya uchaguzi, zitakuwepo orodha mbili za wagombea :
Orodha A itakuwa na majina ya wagombea na sifa zao kama zilivyoainishwa katika aya 3 (b) (i) ; na
Orodha B itakuwa na majina ya wagombea na sifa zao kama zilivyoainishwa katika aya 3 (b) (ii).
Mgombea mwenye sifa za kutosha zenye kukidhi orodha zote mbili atachagua anataka kuwemo katika orodha ipi. Katika uchaguzi wa awali wa Mahakama, kwa uchache watachaguliwa majaji tisa kutoka orodha A na majaji watano kutoka orodha B. Chaguzi zifuatazo zitaendeshwa kwa namna ambayo zitadumisha uwiano wa majaji walioteuliwa kwenye orodha hizo mbili.

6. (a) Majaji watachaguliwa kwa kura ya siri kwenye mkutano wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama ulioitishwa kwa madhumuni ya shughuli hiyo chini ya hiyo ibara 112. Kwa kutegemea masharti ya aya 7, watu watakaochaguliwa kujiunga na Mahakama watakuwa 18 waliopata kura nyingi zaidi na theluthi mbili ya wingi wa kura za Nchi zinazounda Mahakama zilizohudhuria na kupiga kura.

(b) Ikiwa idadi ya majaji waliochaguliwa katika duru ya kwanza haitoshi, utafanyika uchaguzi mwingine kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa katika aya ndogo (a) mpaka hapo nafasi zilizo wazi zitakapojazwa.

7. Majaji wawili hawawezi kuwa raia wa Nchi moja. Mtu ambaye, kwa madhumuni ya uanachama wa Mahakama, anaweza kuchukulia kuwa ni raia wa zaidi ya Nchi moja atahesabiwa kuwa ni raia wa Nchi ile ambayo kwa kawaida mtu huyo anatumia haki zake za kiraia na za kisiasa.

8. (a) Katika kuchagua majaji, Nchi zinazounda Mahakama zitazingatia umuhimu wa kuhakikisha kuwa muundo wa Mahakama una :

Copyright © STIC 2010

(i) Uwakilishi wa mifumo mikuu ya kisheria ulimwenguni ;

(ii) Uwakilishi wa uwiano wa kijiografia ; na

(iii) Uwakilishi wa uwiano wa majaji wanawake na wanaume ;

(b) Nchi zinazounda Mahakama zitazingatia pia umuhimu wa kuwepo kwa majaji waliobobea katika masuala maalumu, ikiwa ni pamoja, bila kukomea hapo, na masuala yanayohusu ukatili dhidi ya wanawake au watoto.

9. (a) Kwa kutegemea aya ndogo (b), majaji watashika nyadhifa zao kwa kipindi cha miaka tisa na, kwa kutegemea aya ndogo (c) na ibara 37, aya 2, hawataweza kuchaguliwa tena.

(b) Katika uchaguzi wa awali, theluthi moja ya majaji waliochaguliwa watateuliwa kwa kura kufanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu ; theluthi moja ya majaji waliochaguliwa watateuliwa kwa kura kufanya kazi kwa kipindi cha miaka sita ; na waliobakia watafanya kazi kwa kipindi cha miaka tisa.

Copyright © STIC 2010

(c) Jaji aliyeteuliwa kufanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu chini ya aya ndogo (b) anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kamili.

10. Bila kuathiri aya 9, jaji aliyepangiwa Chumba cha Kesi au Chumba cha Rufaa kwa mujibu wa ibara 39 atabakia kazini ili kumaliza kesi au rufaa ambayo itakuwa imeshaanza kusikilizwa mbele ya Chumba husika.

Ibara 37
Nafasi za Mahakama zilizo wazi

1. Panapokuwepo na nafasi iliyo wazi katika Mahakama kutafanyika uchaguzi kwa mujibu wa ibara 36 ili kujaza nafasi hiyo.

2. Jaji aliyechaguliwa kujaza nafasi iliyo wazi, atafanya kazi kwa muda uliobaki wa kipindi cha yule aliyemchukulia nafasi yake, na ikiwa kipindi hicho ni miaka mitatu au chini ya hapo, ataweza kuchaguliwa tena kwa muda kamili chini ya ibara 36.

Ibara 38
Ofisi ya Rais

1. Rais na Makamu wa Kwanza na wa Pili wa Rais watachaguliwa kwa kura nyingi za majaji. Kila mmoja wao atafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu, au mpaka mwisho wa kipindi chake cha ujaji, chochote kitakachomalizika mwanzo. Wanaweza kuchaguliwa tena mara moja.

Copyright © SFIC 2010

2. Makamu wa Kwanza wa Rais atakaimu nafasi ya Rais pale Rais atakapokuwa hawezi kupatikana au amekataliwa. Makamu wa Pili wa Rais atakaimu nafasi ya Rais pale wote wawili, Rais na Makamu wa Kwanza wa Rais watakapokuwa hawawezi kupatikana au wamekataliwa.

3. Rais pamoja na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais ndiyo watakaounda Ofisi ya Rais ambayo itawajibika na :

   (a) Uendeshaji mzuri wa utawala wa Mahakama, isipokuwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka ; na

   (b) Kazi nyingine ilizokabidhiwa kwa mujibu wa Mkataba huu.

4. Katika kutekeleza wajibu wake chini ya aya 3 (a), Ofisi ya Rais itaratibu na kujaribu kuleta makubaliano ya Mwendesha Mashtaka, na mambo yote yanayohusu pande zote mbili.

Ibara 39
Vyumba

1. Mara baada ya uchaguzi wa majaji, Mahakama itaunda matawi yaliyoainishwa katika ibara 34, aya (b). Tawi la Rufaa litaundwa na Rais, na majaji wengine wanne, Tawi la Kesi litaundwa na majaji wasiopungua sita na Tawi la Utangulizi litaundwa na majaji wasiopungua sita. Upangaji wa majaji kwenye matawi utajikita kwenye shughuli zinazotakiwa kufanywa na kila tawi, na sifa na uzoefu wa majaji waliochaguliwa kujiunga na Mahakama kwa namna ambayo kila tawi litakuwa na mchanganyiko wa utaalamu unaofaa wa sheria za makosa ya jinai na taratibu zake na sheria za kimataifa. Matawi ya Kesi na Utangulizi yataundwa kwa kiwango kikubwa na majaji wenye uzoefu wa kesi za makosa ya jinai.

2. (a) Katika kila tawi, shughuli za kimahakama za Mahakama zitaendeshwa na Vyumba.

   (b) (i) Chumba cha Rufaa kitaundwa na majaji wote wa Tawi la Rufaa ;

   (ii) Shughuli za Chumba cha Kesi zitaendeshwa na majaji watatu wa Tawi la Kesi ;

   (iii) Shughuli za Chumba cha Utangulizi zitaendeshwa ama na majaji watatu wa Tawi la Utangulizi au jaji mmoja wa tawi hilo kwa mujibu wa Mkataba huu na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi ;

   (c) Hakuna chochote katika aya hii kitakachozuia uundaji sawia wa Chumba cha Kesi au Chumba cha Utangulizi zaidi ya kimoja pale uzito wa kazi za Mahakama utakapohitaji ifanyike hivyo ili kuleta ufanisi.

3. (a) Majaji waliopangwa kufanya kazi katika Matawi ya Kesi na Utangulizi watafanya kazi katika matawi hayo kwa kipindi cha miaka mitatu ; na baada ya hapo, mpaka hapo itakapomalizika kesi ambayo imeshaanza kusikilizwa katika tawi linalohusika.

Copyright © STIC 2010

(b) Majaji waliopangwa kwenye Tawi la Rufaa watafanya kazi katika tawi hilo kwa muda wote ambao wameajiriwa katika Mahakama.

4. Majaji waliopangwa katika Tawi la Rufaa watafanya kazi katika tawi hilo tu. Hakuna chochote katika ibara hii kitakachozuia kuwahamisha kwa muda majaji kutoka Tawi la Kesi kwenda kwenye Tawi la Utangulizi, au kinyume chake, ikiwa Ofisi ya Rais inaona kwamba uzito wa kazi za Mahakama utahitaji ifanyike hivyo ili kuleta ufanisi, ilimradi tu katika hali yoyote ile jaji ambaye ameshiriki katika kipindi cha utangulizi cha kesi hatatakiwa kukaa kwenye Chumba cha Kesi kusikiliza kesi hiyo.

Ibara 40
Uhuru wa majaji

1. Majaji watakuwa huru watakapokuwa wanaendesha shughuli zao.

2. Majaji hawatajihusisha na shughuli yoyote itakayoweza kuingilia kati shughuli zao za kimahakama au kuathiri imani katika uhuru wao.

Copyright © STIC 2010

3. Majaji wanaotakiwa kufanya kazi kwa muda wote kwenye makao makuu ya Mahakama hawatajihusisha na kazi nyingine yoyote yenye hadhi ya kitaalamu.

4. Suala lolote linalohusiana na utekelezaji wa aya 2 na 3 litaamuliwa kwa wingi ulio dhahiri wa kura za majaji. Pale ambapo suala hilo linamhusu jaji mmoja, jaji huyo hatashiriki katika kufanya uamuzi.

Ibara 41
Kujiondoa na kukataliwa kwa majaji

1. Ofisi ya Rais, kwa ombi la jaji, inaweza kumkubalia jaji kujiondoa katika kufanya shughuli fulani chini ya Mkataba huu kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

2. (a) Jaji hawezi kushiriki katika kesi yoyote ambayo sifa yake ya kutokuwa na upendeleo inaweza kuwa na sababu yoyote ya kutiliwa shaka. Jaji anaweza kukataliwa katika kuendesha kesi kwa mujibu wa aya hii kama, pamoja na

mambo mengine, jaji huyo hapo awali alifanya kazi yoyote katika taratibu za kesi hiyo mbele ya Mahakama au katika kesi ya kitaifa ya makosa ya jinai inayohusiana nayo ambamo mtu anayelengwa na upelelezi au na mashtaka alihusika. Jaji anaweza pia kukataliwa kutokana na sababu nyingine zitakazotajwa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

(b) Mwendesha Mashtaka au mtu anayelengwa na upelelezi au na mashtaka anaweza kuomba kumkataa jaji chini ya aya hii.

(c) Suala lolote kuhusiana na kukataliwa kwa jaji litaamuliwa kwa wingi ulio dhahiri wa kura za majaji. Jaji anayepingwa atakuwa na haki ya kutoa maoni yake juu ya suala hilo lakini hatashiriki katika kufanya uamuzi.

Ibara 42
Ofisi ya Mwendesha Mashtaka

Copyright © STIC 2010

1. Ofisi ya Mwendesha Mashtaka itaendesha shughuli zake kwa kujitegemea kama chombo huru cha Mahakama. Itakuwa na wajibu wa kupokea rufaa na habari zote zenye kuthibitishwa juu ya makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, ili kuzichunguza, kufanya upelelezi na kufungua mashtaka mbele ya Mahakama. Mtumishi wa ofisi hiyo hatatafuta, au hatatenda kwa kufuata maagizo yoyote kutoka vyanzo vya nje.

2. Ofisi hiyo itaongozwa na Mwendesha Mashtaka. Mwendesha Mashtaka atakuwa na madaraka kamili juu ya usimamizi na uendeshaji wa Ofisi hiyo, ikiwa ni pamoja na watumishi, nyenzo na rasilimali nyingine. Mwendesha Mashtaka atasaidiwa na Naibu mmoja au zaidi, ambaye atawajibika kufanya shughuli nyingine zozote zile za Mwendesha Mashtaka chini ya Mkataba huu. Mwendesha Mashtaka na Manaibu Waendesha Mashtaka watakuwa ni raia kutoka mataifa tofauti. Watafanya kazi kwa muda wote.

3. Mwendesha Mashtaka na Manaibu Waendesha Mashtaka watakuwa ni watu wenye uadilifu mkubwa na wenye ustadi mkubwa na uzoefu mkubwa katika utendaji wa kuendesha

mashtaka au kesi za makosa ya jinai. Watakuwa mahiri katika ujuzi wa lugha na ufasaha wa angalau lugha mojawapo ya lugha za kazi za Mahakama.

4. Mwendesha Mashtaka atachaguliwa kwa kura ya siri na kwa wingi ulio dhahiri wa wajumbe wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Manaibu Waendesha Mashtaka watachaguliwa kwa namna hiyo hiyo kutoka katika orodha ya wagombea iliyowasilishwa na Mwendesha Mashtaka. Mwendesha Mashtaka atateua wagombea watatu kwa kila nafasi ya Naibu Mwendesha Mashtaka inayotakiwa kujazwa. Isipokuwa kama umeamuliwa muda mfupi zaidi wakati wanapochaguliwa, Mwendesha Mashtaka na Manaibu Waendesha mashtaka watashika nyadhifa zao kwa muda wa miaka tisa na hawataweza kuchaguliwa tena.

5. Mwendesha Mashtaka au Naibu Mwendesha Mashtaka hawatajihusisha na shughuli yoyote ile ambayo inaweza kuingilia kati shughuli zao za kuendesha mashtaka au kuathiri imani katika uhuru wao. Hawatajihusisha na kazi nyingine yoyote yenye hadhi ya kitaalamu.

Copyright © STTC 2010

6. Ofisi ya Rais inaweza kumkubalia Mwendesha Mashtaka au Naibu Mwendesha Mashtaka, kujiondoa kwa ombi lake mwenyewe, kushughulikia kesi fulani.

7. Mwendesha Mashtaka au Naibu Mwendesha Mashtaka hatashiriki katika kesi yoyote ambayo sifa yake ya kutokuwa na upendeleo inaweza kuwa na sababu za kutiliwa shaka. Wanaweza kukataliwa katika kesi kwa mujibu wa aya hii kama, pamoja na mambo mengine, hapo awali walifanya kazi yoyote katika taratibu za kesi hiyo mbele ya Mahakama au katika kesi ya kitaifa ya makosa ya jinai inayohusiana na mtu anayelengwa na upelelezi au na mashtaka.

8. Suala lolote linalohusiana na kukataliwa kwa Mwendesha Mashtaka au Naibu Mwendesha Mashtaka litaamuliwa na Chumba cha Rufaa.

   (a) Mtu anayelengwa na upelelezi au na mashtaka anaweza, wakati wowote, kuomba kumkataa Mwendesha Mashtaka

au Naibu Mwendesha Mashtaka kutokana na sababu zilizotajwa katika ibara hii ;

(b) Mwendesha Mashtaka au Naibu Mwendesha Mashtaka, kama inafaa, atakuwa na haki ya kutoa maoni yake kuhusu suala hilo.

9. Mwendesha Mashtaka atateua washauri ambao ni wataalamu wa sheria inayohusiana na masuala fulani, ikiwa ni pamoja na, lakini yasiyoishia, kwenye ukatili wa kingono, ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Ibara 43
Ofisi ya Msajili

1. Ofisi ya Msajili itashughulikia mambo yasiyokuwa ya kimahakama, ambayo ni ya kiutawala na ya kutoa hudumu kwa Mahakama bila ya kuathiri shughuli na madaraka ya Mwendesha Mashtaka kwa mujibu wa ibara 42.

Copyright © STIC 2010

2. Ofisi ya Msajili itaongozwa na Msajili, ambaye atakuwa afisa mkuu tawala wa Mahakama. Msajili atafanya shughuli zake chini ya mamlaka ya Rais wa Mahakama.

3. Msajili na Naibu Msajili watakuwa ni watu wenye uadilifu mkubwa na wenye ustadi mkubwa na umahiri mkubwa wa lugha na ufasaha wa angalau lugha mojawapo ya lugha za kazi za Mahakama.

4. Majaji watamchagua Msajili kwa wingi ulio dhahiri wa kura za siri, kwa kutilia maanani mapendekezo yoyote ya Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Kama kuna haja, na kufuatia mapendekezo ya Msajili, majaji watamchagua Naibu Msajili kwa namna hiyo hiyo.

5. Msajili atashika madaraka hayo kwa kipindi cha miaka mitano, na ataweza kuchaguliwa tena mara moja tu na atafanya kazi kwa muda wote. Naibu Msajili atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano au kwa muda mfupi zaidi, kama itakavyoamuliwa kwa wingi ulio dhahiri wa kura za majaji, na ataweza kuchaguliwa

kwa msingi kwamba Naibu Msajili atatakiwa kufanya kazi kama inavyohitajika.

6. Msajili ataanzisha, katika Ofisi ya Msajili, Kitengo cha Msaada kwa Waathiriwa na Mashahidi. Kwa kushauriana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Kitengo hicho kitachukua hatua za kulinda, taratibu za kiusalama, ushauri nasaha na msaada mwingine unaofaa kwa mashahidi, waathiriwa wanaokuja mbele ya Mahakama na watu wengine ambao wamo hatarini kwa sababu ya maelezo yaliyotolewa na mashahidi hao. Kitengo hicho kitajumuisha wataalamu wa maradhi ya kupatwa na kiwewe, ikiwa ni pamoja na kiwewe kinachohusiana na ukatili wa kingono.

Ibara 44
Watumishi

1. Mwendesha Mashtaka na Msajili wataajiri watumishi wenye sifa kama zinavyohitajika katika ofisi zao. Kwa Mwendesha Mashtaka, watumishi hao ni pamoja na kuajiri wapelelezi.

Copyright © STIC 2010

2. Katika kuajiri watumishi, Mwendesha Mashtaka na Msajili watahakikisha kuwepo kwa kiwango cha juu cha ufanisi, cha ustadi na uadilifu, wakizingatia, mutatis mutandis, vigezo vilivyotajwa katika ibara 36, aya 8.

3. Msajili, kwa kukubaliana na Ofisi ya Rais na Mwendesha Mashtaka, atapendekeza Kanuni za Utumishi ambazo zitajumuisha masharti na maslahi ya watumishi wa Mahakama watakaoajiriwa, mishahara yao na kuachishwa kwao kazi. Kanuni hizo za Utumishi zitaidhinishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

4. Mahakama inaweza, katika hali isiyokuwa ya kawaida, kuajiri watu wa kujitolea, watakaoletwa na Nchi zinazounda Mahakama, mashirika baina ya serikali mbalimbali, au mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ili kusaidia kazi za chombo chochote cha Mahakama. Mwendesha Mashtaka anaweza kukubali watu kama hao kwa niaba ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Watumishi hao wa kujitolea wataajiriwa kwa mujibu wa mwongozo utakaotayarishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

Ibara 45
Kiapo rasmi

Kabla ya kuanza kazi zao zilizotajwa katika Mkataba huu, majaji, Mwendesha Mashtaka, Manaibu Waendesha Mashtaka, Msajili na Naibu Msajili, kila mmoja atakula kiapo katika mahakama ya wazi, kuwa watafanya shughuli zao bila upendeleo na kwa makini kabisa.

Ibara 46
Kuondolewa kazini

1. Jaji, Mwendesha Mashtaka, Naibu Mwendesha Mashtaka, Msajili au Naibu Msajili wataondolewa kazini kama uamuzi wa kufanya hivyo umechukuliwa kwa mujibu wa aya 2, endapo mtu huyo :

   (a) Ameonekana kuwa na tabia mbaya sana au uvunjaji mkubwa wa maadili ya kazi zake chini ya Mkataba huu, kama ilivyo katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi ; au

   (b) Anashindwa kutekeleza shughuli zake kama ilivyofafanuliwa katika Mkataba huu.

Copyright © STIC 2010

2. Uamuzi wa kumwondoa kazini jaji, Mwendesha Mashtaka au Naibu Mwendesha Mashtaka, chini ya aya 1, utachukuliwa na Nchi zinazounda Mahakama kwa kura ya siri :

   (a) Kama ni jaji, kwa wingi wa theluthi mbili ya Nchi zinazounda Mahakama kufuatana na pendekezo lililoidhinishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya majaji wengine ;

   (b) Kama ni Mwendesha Mashtaka, kwa wingi ulio dhahiri wa Nchi zinazounda Mahakama ;

   (c) Kama ni Naibu Mwendesha Mashtaka, kwa wingi ulio dhahiri wa Nchi zinazounda Mahakama kufuatana na pendekezo la Mwendesha Mashtaka.

3. Uamuzi wa kumwondoa kazini Msajili au Naibu Msajili utafanywa na majaji, kwa wingi ulio dhahiri.

4. Jaji, Mwendesha Mashtaka, Naibu Mwendesha Mashtaka, Msajili au Naibu Msajili ambaye tabia au uwezo wa kutekeleza kazi zake kama inavyotakiwa na Mkataba huu, unatiliwa shaka, chini ya ibara hii, atakuwa na fursa kamili ya kuwasilisha na kupokea ushahidi na kutoa maoni kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi. Mtu huyo hatashiriki katika kulijadili jambo hilo.

Ibara 47
Hatua za kinidhamu

Jaji, Mwendesha Mashtaka, Naibu Mwendesha Mashtaka, Msajili au Naibu Msajili, aliyetenda kosa dogo kuliko lile linalotajwa katika ibara 46, aya 1, atakachukuliwa hatua za kinidhamu kufuatana na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Ibara 48
Haki na kinga

Copyright © STIC 2010

1. Mahakama itakuwa na haki na kinga, ambazo itazihitaji katika kutekeleza madhumuni yake katika Nchi zote zinazounda Mahakama.

2. Majaji, Mwendesha Mashtaka, Manaibu Waendesha Mashtaka na Msajili, wanapokuwa katika kazi za Mahakama watakuwa na haki na kinga kama zile walizonazo wakuu wa ofisi za ubalozi, na baada ya kumalizika muda wao wa utumishi, wataendelea kuwa na kinga ya hatua zozote za kisheria kutokana na maneno waliyoyasema au kuyaandika na vitendo walivyovifanya katika nyadhifa zao rasmi.

3. Naibu Msajili, watumishi wa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na watumishi wa Ofisi ya Msajili watakuwa na haki na kinga na nyenzo zinazohitajika katika kufanya kazi zao, kwa mujibu wa makubaliano kuhusu haki na kinga za Mahakama.

4. Mawakili, wataalamu, mashahidi au watu wengine wowote wanaohitajika kwenye makao makuu ya Mahakama watatendewa kama inavyohitajika katika uendeshaji wa shughuli za Mahakama, kulingana na makubaliano kuhusu haki na kinga za Mahakama.

5. Haki na kinga za :

(a) Jaji au Mwendesha Mashtaka zinaweza kuondolewa kwa wingi ulio dhahiri wa majaji ;

(b) Msajili zinaweza kuondolewa na Ofisi ya Rais ;

(c) Manaibu Waendesha Mashtaka na watumishi wa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka zinaweza kuondolewa na Mwendesha Mashtaka ;

(d) Naibu Msajili na watumishi wa Ofisi ya Msajili zinaweza kuondolewa na Msajili.

Ibara 49
Mishahara, posho na gharama za matumizi

Majaji, Mwendesha Mashtaka, Manaibu waendesha mashtaka, Msajili na Naibu Msajili watapokea mishahara, posho na gharama za matumizi kama itakavyoamuliwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Mishahara na posho hizo havitapunguzwa wakati wa kipindi chao cha utumishi.

Copyright © STIC 2010

Ibara 50
Lugha rasmi na lugha za kazi

1. Lugha rasmi za Mahakama zitakuwa Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania. Hukumu za Mahakama pamoja na maamuzi mengine ya kusuluhisha masuala ya msingi yanayoletwa kwenye Mahakama yatachapishwa katika lugha rasmi. Ofisi ya Rais, kwa mujibu wa vigezo vilivyo katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, itaamua ni maamuzi gani yatachukuliwa kuwa yamesuluhisha masuala ya msingi kwa madhumuni ya aya hii.

2. Lugha za kazi za Mahakama zitakuwa Kiingereza na Kifaransa. Kanuni za Utaratibu na Ushahidi zitaamua hali ambamo lugha nyingine rasmi zinaweza kutumiwa kama lugha za kazi.

3. Kwa ombi la upande wowote unaoshiriki katika kesi au Nchi iliyoruhusiwa kuingilia kati katika kesi hiyo, Mahakama, itaidhinisha lugha ambayo si Kiingereza wala Kifaransa itumiwe na upande au Nchi hiyo, ilimradi tu Mahakama inaona kuwa idhini hiyo ni mwafaka.

Ibara 51
Kanuni za Utaratibu na Ushahidi

1. Kanuni za Utaratibu na Ushahidi zitaanza kutumika mara tu baada ya kupitishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

2. Marekebisho ya Kanuni za Utaratibu na Ushahidi yanaweza kupendekezwa na :

   (a) Nchi yoyote mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ;

   (b) Majaji kwa wingi ulio dhahiri ; au

   (c) Mwendesha Mashtaka.

   Marekebisho hayo yataanza kutumika baada ya kupitishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

Copyright © STIC 2010

3. Baada ya kupitishwa kwa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, katika hali za dharura, ambapo kanuni hazitoshelezi katika hali ya namna ya pekee mbele ya Mahakama, majaji kwa wingi wa theluthi mbili, wanaweza kutengeneza kanuni za dharura, ili zitumike mpaka hapo zitakapopitishwa, kufanyiwa marekebisho au kukataliwa katika mkutano mwingine wa kawaida, au mkutano maalumu wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

4. Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, marekebisho yake na kanuni nyingine za dharura zitakubaliana na Mkataba huu. Marekebisho ya Kanuni za Utaratibu na Ushahidi pamoja na kanuni za dharura hazitatumiwa kwa kurudi nyuma kwa namna itakayomsababishia madhara mlengwa wa upelelezi au wa mashtaka au aliyekwisha kupatikana na hatia.

5. Pale panapotokea mgogoro kati ya Mkataba na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, Mkataba ndio utakaotawala.

Ibara 52
Kanuni za Mahakama

1. Majaji, kwa mujibu wa Mkataba huu na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, watapitisha kwa wingi ulio dhahiri, Kanuni za Mahakama zilizo za lazima katika kutenda shughuli zake za kawaida.

2. Mwendesha Mashtaka na Msajili wataombwa ushauri wao wakati wa kutunga Kanuni za Mahakama na marekebisho yoyote yanayohusiana na kanuni hizo.

3. Kanuni na marekebisho yake yoyote vitaanza kutumika baada ya kupitishwa, ila kama itaamuliwa vinginevyo na majaji. Mara baada ya kupitishwa zitasambazwa kwa Nchi zinazounda Mahakama ili zitoe maoni yao. Kama hapatakuwa na pingamizi katika kipindi cha miezi sita kutoka kwa Nchi nyingi zinazounda Mahakama, kanuni hizo zitaanza kutumika.

Copyright © SIIC 2010

Sehemu V Upelelezi na mashtaka

Ibara 53
Uanzishaji wa upelelezi

1. Mwendesha Mashtaka baada ya kutathmini taarifa aliyopewa ataanzisha upelelezi, isipokuwa kama ameamua kwamba hakuna sababu za kutosha kuendelea na upelelezi chini ya Mkataba huu. Katika kuamua kuanzisha upelelezi, Mwendesha Mashtaka ataangalia kama :

   (a) Taarifa alizopewa Mwendesha Mashtaka zina sababu za msingi za kuamini kwamba kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama limetendwa au linatendwa ;

   (b) Kesi husika inakubalika au inaweza kukubalika chini ya ibara 17 ; na

   (c) Kwa kutilia maanani uzito wa kosa la jinai na maslahi ya waathiriwa, kuna kila sababu za kuamini kuwa upelelezi hautakidhi maslahi ya sheria.

   Ikiwa Mwendesha Mashtaka ameamua kuwa hakuna haja ya kushtaki, na uamuzi wake unatokana na aya ndogo (c) tu ya hapo juu, atakiarifu Chumba cha Utangulizi.

2. Ikiwa kufuatia upelelezi,Mwendesha Mashtaka ataona kuwa hakuna sababu za kutosha kufungua mashtaka kwa sababu :

   (a) Hakuna sababu za kutosha za kisheria au za kimatukio za kutaka itolewe hati, au samansi chini ya ibara 58 ;

   (b) Kesi hiyo haikubaliki chini ya ibara 17 ; au

   (c) Kufungua mashtaka hakutakuwa na faida kwa maslahi ya haki, ikitiliwa maanani hali zote, ikiwa ni pamoja na uzito wa kosa la jinai, maslahi ya waathiriwa, umri, au udhaifu wa mtuhumiwa na ushiriki wake katika kosa la jinai analotuhumiwa ; Mwendesha Mashtaka atakiarifu

Copyright © SIIC 2010

Chumba cha Utangulizi na Nchi inayowasilisha hali chini ya ibara 14, au Baraza la Usalama kwa hali iliyo chini ya ibara 13, aya (b) juu ya uamuzi wake na sababu za kufikia uamuzi huo.

3. (a) Kwa ombi la Nchi inayowasilisha rufaa chini ya ibara 14, au la Baraza la Usalama kwa hali iliyo chini ya ibara 13, aya (b), Chumba cha Utangulizi kinaweza kupitia upya uamuzi wa Mwendesha Mashtaka wa kutofungua mashtaka chini ya aya 1 au 2 na kinaweza kumwomba Mwendesha Mashtaka kufikiria upya uamuzi wake.

(b) Zaidi ya hayo, Chumba cha Utangulizi kinaweza, kwa hiari yake, kupitia upya uamuzi wa Mwendesha Mashtaka wa kutofungua mashtaka kama hatua hiyo inategemea sababu zinazotajwa katika aya 1 (c) na aya 2 (c) tu. Katika hali hiyo, uamuzi wa Mwendesha Mashtaka utaanza kutumika tu endapo utathibitishwa na Chumba cha Utangulizi.

Copyright © STIC 2010

4. Mwendesha Mashtaka anaweza, wakati wowote, kubadili uamuzi wake ama kuanzisha upelelezi, au kufungua mashtaka, kufuatana na mambo au taarifa mpya.

Ibara 54
Kazi na madaraka ya Mwendesha Mashtaka kuhusiana na upelelezi

1. Mwendesha Mashtaka :

(a) Ili kuthibitisha ukweli, atapanua upelelezi kuhusiana na mambo yote na ushahidi wote unaohusika katika kuamua ikiwa kuna dhima ya kosa la jinai chini ya Mkataba huu, na katika kufanya hivyo, kupeleleza hali ya kutia au kutoa hatiani kwa uwiano ;

(b) Atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha kuwa unafanyika upelelezi mzuri na kufungua mashtaka ya makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, na katika kufanya hivyo, kuheshimu maslahi na hali binafsi ya waathiriwa na mashahidi, ikiwa ni pamoja na umri, jinsia, kama ilivyofafanuliwa katika ibara 7, aya 3, na afya, na

kutilia maanani hali ya kosa lenyewe la jinai, hususan pale linapohusiana na ukatili wa kingono, ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto ; na

(c) Ataheshimu kikamilifu haki za watu zinazojitokeza chini ya Mkataba huu.

2. Mwendesha Mashtaka anaweza kufanya upelelezi katika eneo la Nchi :

(a) Kwa mujibu wa vipengele vya sehemu 9 ; au

(b) Kama ilivyoidhinishwa na Chumba cha Utangulizi, chini ya ibara 57, aya 3 (d).

3. Mwendesha Mashtaka ataweza :

(a) Kukusanya na kuchunguza ushahidi ;

(b) Kuita na kuhoji watu wanaopelelezwa, waathiriwa na mashahidi ;

(c) Kuomba ushirikiano wa Nchi yoyote au shirika lolote baina ya serikali mbalimbali au mipango yoyote ya kiserikali kwa mujibu wa mamlaka na/au madaraka yake ;

(d) Kuingia katika mipango au makubaliano yasiyopingana na Mkataba huu, kama itakavyokuwa lazima ili kuleta ushirikiano na Nchi, shirika baina ya serikali mbali mbali au mtu ;

(e) Kukubali kutotoa, katika hatua yoyote ile ya kesi, siri kuhusiana na nyaraka au taarifa ambazo Mwendesha Mashtaka amezipata kwa masharti ya kutunza siri na kwa madhumuni ya kutafuta ushahidi mpya tu, isipokuwa kama mwenye kutoa habari hizo amekubali ; na

(f) Kuchukua hatua za lazima au kuomba zichukuliwe hatua za lazima ili kuhakikisha kutunzwa kwa siri ya taarifa, ulinzi wa mtu yeyote au utunzaji wa ushahidi.

Copyright © STIC 2010

Ibara 55
Haki za watu wakati wa upelelezi

1. Kuhusiana na upelelezi unaoanzishwa chini ya Mkataba huu, mtu :

   (a) Hatalazimishwa kujitia mwenyewe hatiani au kukiri kosa ;

   (b) Hatatendewa tendo lolote la kulazimishwa, kutishwa au kuogopeshwa, kuteswa au kufanyiwa aina yoyote ya ukatili, kudhalilishwa au kupewa adhabu ;

   (c) Akihojiwa katika lugha nyingine ambayo si lugha anayoielewa na kuizungumza vizuri, apate huduma ya bure ya msaada wa mkalimani hodari na tafsiri zilizo za lazima zitakazokidhi mahitaji ya kupatiwa haki ; na

   (d) Hatakamatwa au kuwekwa kuzuizini kiholela ; na hatanyimwa uhuru wake isipokuwa kwa sababu na kwa kufuata taratibu zilizotajwa na Mkataba huu.

Copyright © STIC 2010

2. Zinapokuwepo sababu za kuamini kwamba mtu alitenda kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama na kwamba mtu huyo anatarajiwa kuhojiwa ama na Mwendesha Mashtaka au na viongozi wa Nchi kutokana na ombi lililotolewa kufuatana na Sehemu 9, mtu huyo atakuwa pia na haki zifuatazo, kabla ya kuhojiwa :

   (a) Kujulishwa kwamba, kuna sababu za kuamini kwamba alitenda kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ;

   (b) Kunyamaza, bila ya kimya hicho kuwa ndio cha kufanya maamuzi kama amekiri kosa au hana hatia ;

   (c) Kupata msaada wa wakili aliyechaguliwa na mtu mwenyewe au, kama hana wakili, apatiwe wakili anayeteuliwa na Mahakama pale ambapo maslahi ya haki yanahitaji hivyo, na bila malipo kutoka kwa mtu huyo kwa hali kama hiyo kama mtu huyo, hana uwezo wa kulipa ; na

(d) Kuhojiwa mbele ya wakili, isipokuwa kama mtu huyo amekataa kwa hiari yake haki yake ya kuwa na wakili.

Ibara 56
Wajibu wa Chumba cha Utangulizi kuhusiana na fursa ya pekee ya kufanya upelelezi

1. (a) Wakati Mwendesha Mashtaka anapoona kwamba upelelezi unampa fursa ya kipekee ambayo haiwezi kupatikana mara nyingine, ya kukusanya maelezo au taarifa, au kupima, kukusanya au kujaribu ushahidi kwa madhumuni ya kesi, Mwendesha Mashtaka atakiarifu Chumba cha Utangulizi.

(b) Katika hali kama hiyo, Chumba cha Utangulizi kinaweza, kutokana na ombi la Mwendesha Mashtaka, kuchukua hatua zinazofaa kwa kuhakikisha ufanisi na ukamilifu wa taratibu na, hususan, kwa kulinda haki za upande wa utetezi.

Copyright © STIC 2010

c) Isipokuwa tu kama Chumba cha Utangulizi kitaamua vinginevyo, Mwendesha Mashtaka atatoa habari zinazohitajika kwa mtu aliyekamatwa au mtu aliyefika mbele ya Mahakama kutokana na samansi kuhusiana na upelelezi uliotajwa katika aya ndogo (a), ili aweze kusikilizwa kuhusu suala hilo.

2. Hatua zinazotajwa na aya 1(b), zinaweza kuwa ni pamoja na :

(a) Kutoa mapendekezo au maagizo kuhusu taratibu zitakazofuatwa ;

(b) Kuagiza ziwekwe kumbukumbu za taratibu za kuendesha kesi ;

(c) Kuteua mtaalamu kwa kusaidia ;

(d) Kuidhinisha wakili wa mtu aliyekamatwa, au aliyefika mbele ya Mahakama kwa kuitikia wito wa samansi, kushiriki au pale ambapo mtu hakukamatwa au kufika mbele ya Mahakama au hakupatiwa wakili, kuteua wakili

mwingine kushiriki na kuwakilisha maslahi ya upande wa utetezi ;

(e) Kuteua mmoja wa wajumbe wake au, kama kuna haja, jaji mwingine atakayepatikana wa Tawi la Utangulizi au la Kesi kutazama na kutoa mapendekezo au maagizo kuhusu kukusanya na kuhifadhi ushahidi na kuwahoji watu ;

(f) Kuchukua hatua nyingine kama itakavyohitajika kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi ushahidi.

3. (a) Pale ambapo Mwendesha Mashtaka atakuwa hakuomba zichukuliwe hatua zinazotajwa na ibara hii lakini Chumba cha Utangulizi kinaona kwamba hatua hizo zinahitajika kwa ajili ya kuhifadhi ushahidi ambao kinauona kuwa ni muhimu kwa upande wa utetezi wakati wa kesi, Chumba kitashauriana na Mwendesha Mashtaka ili kujua kama kuna sababu nzuri kwa Mwendesha Mashtaka kushindwa kuomba hatua hizo zichukuliwe. Ikiwa baada ya kushauriana, Chumba cha Utangulizi kitaona kwamba kushindwa kwa Mwendesha Mashtaka kuomba hatua hizo zichukuliwe hakuna sababu, kinaweza kuchukua hatua hizo kwa uamuzi wake wenyewe.

Copyright © STIC 2010

(b) Mwendesha Mashtaka anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Chumba cha Utangulizi wa kuchukua hatua kwa uamuzi wake wenyewe, chini ya aya hii. Rufaa hii itasikilizwa kwa haraka.

4. Kukubalika kwa ushahidi uliohifadhiwa au kukusanywa kwa madhumuni ya kesi kufuatana na ibara hii, au kwa kumbukumbu ya ushahidi huo katika kesi, kutatawaliwa na ibara 69, na kupewa uzito utakaoamuliwa na Chumba cha Kesi.

Ibara 57
Shughuli na madaraka ya Chumba cha Utangulizi

1. Isipokuwa tu kama Mkataba huu utaelezewa vinginevyo, Chumba cha Utangulizi kitaendesha shughuli zake kwa mujibu wa vipengele vya ibara hii.

2. (a) Maagizo au maamuzi ya Chumba cha Utangulizi vilivyotolewa chini ya ibara 15, 18, 19, 54 aya 2, 61, aya 7, na 72 lazima vikubaliwe kwa wingi wa majaji wake.

(b) Kwa hali nyingine zozote, jaji mmoja wa Chumba cha Utangulizi anaweza kutekeleza shughuli zilizotajwa katika Makataba huu, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi au kwa wingi wa Chumba cha Utangulizi.

3. Zaidi ya shughuli zake nyingine kufuatana na Mkataba huu, Chumba cha Utangulizi kinaweza :

(a) Kwa ombi la Mwendesha Mashtaka, kutoa maagizo kama hayo na hati kama zitakavyohitajika kwa madhumuni ya upelelezi ;

(b) Kwa ombi la mtu aliyekamatwa au aliyefika mbele ya Mahakama kwa kuitikia samansi chini ya ibara 58, kutoa maagizo kama hayo, ikiwa ni pamoja na hatua zilizoelezwa katika ibara 56, au kutafuta ushirikiano kufuatana na Sehemu 9, kama itakavyokuwa lazima ili kumsaidia mtu huyo kutayarisha utetezi wake ;

(c) Kukiwa na haja, kuhakikisha kuwepo kinga na kuheshimu faragha ya waathiriwa na mashahidi, kutunza ushahidi, kuhami watu wa watu waliokamatwa au waliofika mbele ya Mahakama kwa kuitikia samansi, na kwa kulinda habari za usalama wa taifa ;

(d) Kumwidhinisha Mwendesha Mashtaka kuchukua hatua mahsusi za upelelezi katika eneo la Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama bila ya kupata ushirikiano wa Nchi hiyo chini ya Sehemu 9 ikiwa, kila itakapowezekana kwa kuzingatia maoni ya Nchi husika, Chumba cha Utangulizi kimeamua katika hali hiyo kuwa Nchi hiyo inaonyesha waziwazi kuwa haiwezi kutekeleza ombi la kutoa ushirikiano kutokana na kukosekana kwa mamlaka yoyote au mfumo wowote wa kimahakama unaoweza kulitekeleza ombi hilo la ushirikiano chini ya Sehemu 9 ;

Copyright © STIC 2010

(e) Pale hati ya kukamata au samansi itakapokuwa imetolewa chini ya Ibara 58, na kwa kuzingatia uzito wa ushahidi na haki za pande husika kama inavyoelezwa katika Mkataba huu na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, kutafuta ushirikiano wa Nchi kufuatana na ibara 93 aya 1 (k), kuchukua hatua za tahadhari kwa madhumuni ya kunyang'anywa mali, hususan kwa maslahi ya mwisho ya waathiriwa.

Ibara 58
Kutolewa hati ya kukamata au samansi na Chumba cha Utangulizi

1. Wakati wowote ule, baada ya kuanza upelelezi, Chumba cha Utangulizi kitatoa, kutokana na ombi la Mwendesha Mashtaka, hati ya kukamata mtu, baada ya kulichunguza ombi hilo na ushahidi au taarifa nyingine zilizotolewa na Mwendesha Mashtaka, ikiwa kimeridhika kwamba :

   (a) Kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba mtu huyo alitenda kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ; na

   (b) Kukamatwa kwa mtu huyo kunaonekana kuwa ni lazima :

      (i) Kuhakikisha kwamba atahudhuria kwenye kesi ;

      (ii) Kuhakikisha kwamba hazuii au hahatarishi upelelezi au taratibu za Mahakama ; au

      (iii) Pale inapowezekana, kumzuia mtu huyo asiendelee kutenda kosa hilo la jinai au kosa la jinai linalohusiana na hilo ambalo lipo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama na ambalo limetokana na mazingira hayohayo.

2. Ombi la Mwendesha Mashtaka litakuwa na :

   (a) Jina la mhusika na taarifa nyingine zozote za kumtambulisha ;

Copyright © STTC 2010

(b) Marejeo mahsusi ya makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ambayo mtu huyo anashutumiwa kuwa aliyatenda ;

(c) Maelezo mafupi ya mambo yanayodaiwa kuunda makosa hayo ya jinai ;

(d) Muhtasari wa ushahidi na taarifa nyingine yoyote ile vinavyotoa sababu za kutosha za kuamini kwamba mtu huyo alitenda makosa hayo ya jinai ; na

(e) Sababu zinazomfanya Mwendesha Mashtaka aamini kwamba lazima mtu huyo akamatwe.

3. Hati ya kukamata itakuwa na :

(a) Jina la mhusika na taarifa nyingine zozote za kumtambulisha ;

Copyright © STIC 2010

(b) Marejeo mahsusi ya makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ambayo yanahalalisha kukamatwa kwa mtu huyo ; na

(c) Maelezo mafupi ya mambo yanayodaiwa kuunda makosa hayo ya jinai.

4. Hati ya kukamata itaendelea kutumika mpaka Mahakama itakapoagiza vinginevyo.

5. Kufuatana na hati ya kukamata, Mahakama inaweza kuomba kukamatwa kwa muda au kukamatwa na kumwasilisha mtu chini ya Sehemu 9.

6. Mwendesha Mashtaka anaweza kuomba Chumba cha Utangulizi kirekebishe hati ya kukamata kwa kubadilisha au kuongeza makosa ya jinai yaliyoelezwa humo. Chumba cha Utangulizi kitarekebisha hati ya kukamata ikiwa inaridhika kuwa kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba mtu huyo alitenda makosa ya jinai kama yalivyorekebishwa au kuongezwa.

7. Kama njia mbadala ya kutaka hati ya kukamata, Mwendesha Mashtaka anaweza kukiomba Chumba cha Utangulizi kutoa samansi ili mtu huyo afike mbele ya Mahakama. Ikiwa Chumba cha Utangulizi kimeridhika kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba mtu huyo alitenda kosa la jinai analoshutumiwa na kwamba samansi inatosha kuhakikisha kwamba atafika mbele ya Mahakama, kitatoa samansi kwa masharti au bila masharti ya kuzuia uhuru (mwingine usiokuwa wa kuwekwa kizuizini) ikiwa inakubaliwa na sheria za kitaifa kwa mtu huyo kufika mbele ya Mahakama. Samansi itakuwa na :

   (a) Jina la mhusika na taarifa nyingine zozote za kumtambulisha ;

   (b) Tarehe ya kufika mbele ya Mahakama ;

   (c) Marejeo mahsusi ya makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ambayo mtu huyo anashutumiwa kuwa ameyatenda ; na

   (d) Maelezo mafupi ya mambo yanayodaiwa kuunda makosa hayo ya jinai.

   Mtu anayelengwa atakabidhiwa samansi.

Copyright © STIC 2010

Ibara 59
Utaratibu wa kukamata katika Nchi ambamo mtu anazuiliwa

1. Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama iliyopokea ombi la kumkamata mtu kwa muda au kumkamata na kumwasilisha itachukua hatua za haraka za kumkamata mtu huyo, kwa mujibu wa sheria zake na vipengele vya sehemu 9.

2. Mtu aliyekamatwa atafikishwa mara moja mbele ya mamlaka ya kimahakama yenye uwezo katika Nchi ambamo mtu anazuiliwa ambayo itaamua, kwa mujibu wa sheria za Nchi hiyo, kama :

   (a) Hati ya kukamata inamhusu mtu huyo ;

   (b) Mtu huyo alikamatwa kufuatana na utaratibu unaotakiwa ; na

(c) Haki za mtu huyo ziliheshimiwa.

3. Mtu aliyekamatwa atakuwa na haki ya kuomba dhamana kutoka kwa mamlaka ya kisheria ya Nchi iliyomzuia wakati akisubiri kuwasilishwa.

4. Katika kufikia uamuzi wa ombi kama hilo, mamlaka ya kisheria katika Nchi ambamo mtu anazuiliwa itafikiria kama, kulingana na uzito wa makosa ya jinai anayoshutumiwa mtu huyo, kuna haja muhimu na ya kipekee inayohalalisha mtu huyo kupewa dhamana, kama kuna uhakika wa kutosha kuwa Nchi ambamo mtu huyo anazuiliwa inaweza kutekeleza wajibu wake wa kumwasilisha mtu huyo kwenye Mahakama. Mamlaka ya Nchi ambamo mtu huyo anazuiliwa haitakuwa na uhuru wa kuamua ikiwa hati ya kukamata imetolewa vilivyo kwa mujibu wa ibara 58 aya 1 (a) na (b).

5. Chumba cha Utangulizi kitajulishwa kuhusu ombi lolote la dhamana na kitatoa mapendekezo kwa mamlaka ya Nchi ambamo mtu anazuiliwa. Mamlaka inayomzuia mtu itayazingatia kikamilifu mapendekezo kama hayo, ikiwa ni pamoja na mapendekezo yoyote juu ya hatua za kumzuia mtu huyo asitoroke kabla ya kutoa uamuzi wake.

Copyright © STIC 2010

6. Kama mtu huyo anapewa dhamana, Chumba cha Utangulizi kinaweza kuomba ripoti kila baada ya kipindi fulani juu ya hali ya dhamana hiyo.

7. Mara baada ya kuagizwa kuwasilishwa na Nchi ambamo mtu anazuiliwa, mtu huyo atawasilishwa kwenye Mahakama haraka iwezekanavyo.

Ibara 60
Utaratibu wa awali mbele ya Mahakama

1. Baada ya mtu huyo kuwasilishwa kwenye Mahakama au anapofika mbele ya Mahakama, kwa hiari yake, au kwa kuitikia wito wa samansi, Chumba cha Utangulizi itabidi kiridhike kuwa mtu huyo amearifiwa juu ya makosa ya jinai ambayo anashutumiwa kuyatenda, na juu ya haki zake kufuatana na Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na haki ya kuomba dhamana wakati anaposubiri kesi.

2. Mtu anayelengwa na hati ya kukamata anaweza kuomba dhamana wakati anaposubiri kesi. Kama Chumba cha Utangulizi kitaridhika kwamba masharti yaliyomo katika Ibara 58, aya 1, yanatimizwa, mtu huyo atabaki kizuizini. Kama sivyo, Chumba cha Utangulizi kitamwachia kwa masharti au bila masharti.

3. Chumba cha Utangulizi kitapitia upya baada ya kila kipindi fulani, uamuzi wake wa kumwachia au kumweka mtu kizuizini, na kinaweza kufanya hivyo wakati wowote kwa ombi la Mwendesha Mashtaka au la mtu huyo. Katika kupitia upya huko kinaweza kurekebisha uamuzi wake kuhusiana na kuweka kizuizini, kuachia au masharti ya kuachia kikiridhika kwamba mazingira yaliobadilika yanahitaji ifanyike hivyo.

4. Chumba cha Utangulizi kitahakikisha kwamba mtu hawekwi kizuizini kwa muda usiotakiwa kabla ya kesi kwa sababu ya ucheleweshaji wa Mwendesha Mashtaka usiokuwa na sababu. Unapotokea ucheleweshaji kama huo Mahakama itafikiria kumwachia mtu huyo kwa masharti au bila masharti.

Copyright © STIC 2010

5. Ikilazimu, Chumba cha Utangulizi kinaweza kutoa hati ya kukamata mtu aliyeachiwa ili kuhakikisha kufika kwake mbele ya Mahakama.

Ibara 61
Kuthibitisha mashtaka kabla ya kesi

1. Kwa kutegemea vipengele vya aya 2, kwa muda wa kutosha baada ya mtu kuwasilishwa au kujitokeza kwa hiari yake Mahakamani, Chumba cha Utangulizi kitaisikiliza kesi ili kuthibitisha mashtaka ambayo Mwendesha Mashtaka anadhamiria kuyafungulia kesi. Kesi itasikilizwa mbele ya Mwendesha Mashtaka na mtu anayefunguliwa mashtaka pamoja na wakili wake.

2. Chumba cha Utangulizi kinaweza, kutokana na ombi la Mwendesha Mashtaka au kwa hiari yake, kusikiliza kesi bila kuwepo kwa mshtakiwa ili kuthibitisha mashtaka ambayo Mwendesha Mashtaka anadhamiria kuyafungulia kesi ikiwa mtu huyo :

   (a) Alikataa haki yake ya kuwepo mahakani ; au

(b) Alikimbia au haonekani, na hatua zote za lazima zimechukuliwa ili awepo na kwenye Mahakama kumwelezea mashtaka yake na kuwa kesi ya kuthibitisha mashtaka hayo itafanyika.

Katika hali hiyo, mtu kama huyo atawakilishwa na wakili pale ambapo Chumba cha Utangulizi kitaamua kuwa kwa kufanya hivyo ni kwa ajili ya kutafuta haki.

3. Kwa muda wa kutosha kabla ya kusikiliza kesi, mtu huyo :

(a) Atapatiwa nakala ya waraka wenye mashtaka ambayo Mwendesha Mashtaka anadhamiria kumfungulia ; na

(b) Ataarifiwa juu ya ushahidi ambao Mwendesha Mashtaka anadhamiria kuutumia wakati wa kusikilizwa kwa kesi.

Chumba cha Utangulizi kinaweza kuagiza kutolewa habari kwa madhumuni ya usikilizaji wa kesi.

Copyright © STIC 2010

4. Kabla ya kesi kusikilizwa, Mwendesha Mashtaka anaweza kuendelea na upelelezi, na anaweza kufanya marekebisho au kufuta mashtaka yoyote yale. Mtu huyo atapewa notisi ya kutosha kabla ya kusikilizwa kwa marekebisho yoyote yale ya mashtaka au mashtaka yaliyofutwa. Pale mashtaka yatakapofutwa, Mwendesha Mashtaka atakiarifu Chumba cha Utangulizi sababu za mashtaka hayo kufutwa.

5. Wakati wa kusikiliza kesi, Mwendesha Mashtaka lazima atoe sababu madhubuti zitakazothibitisha kila shtaka pamoja na ushahidi wa kutosha utakaotoa sababu za kuamini kuwa mtu huyo alitenda kosa la jinai ambalo anashtakiwa. Mwendesha Mashtaka anaweza kutegemea ushahidi wa nyaraka au wa papo kwa papo na hatakuwa na haja ya kuwaita mashahidi watakaotakiwa kutoa ushahidi katika kesi hiyo.

6. Wakati wa kusikiliza kesi, mtu huyo :

(a) Anaweza kuyakataa mashtaka ;

(b) Anaweza kuupinga ushahidi uliowasilishwa na Mwendesha Mashtaka ; na

(c) Anaweza kutoa ushahidi.

7. Kutokana na usikilizwaji wa kesi, Chumba cha Utangulizi kitaamua ikiwa kuna ushahidi wa kutosha utakaojenga sababu madhubuti za kuamini kuwa mtu huyo ametenda kila kosa la jinai ambalo anashtakiwa. Kufuatana na uamuzi wake, Chumba cha Utangulizi :

(a) Kitayathibitisha mashtaka hayo baada ya kuridhika kuwa kuna ushahidi wa kutosha na kitampeleka mtu huyo kwenye Chumba cha Kesi kwa ajili ya kuendesha kesi juu ya mashtaka kama yalivyothibitishwa ;

(b) Kitakataa kuyathibitisha mashtaka hayo pindi kikiridhika kuwa hakuna ushahidi wa kutosha ;

(c) Kitaahirisha kusikilizwa kwa kesi na kumwomba Mwendesha Mashtaka kufikiria :

(i) Kutoa ushahidi wa ziadi au kufanya upelelezi wa ziada kuhusiana na shtaka maalumu ; au

(ii) Kulifanyia shtaka marekebisho kwa kuwa ushahidi uliowasilishwa unaonekana kuthibitisha kosa tofauti la jinai, lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama.

8. Pale ambapo Chumba cha Utangulizi kinakataa kulithibitisha shtaka, Mwendesha Mashtaka hatazuiwa kutaka shtaka hilo lithibitishwe baadaye ikiwa ombi hilo litaambatanishwa na ushahidi wa ziada.

9. Baada ya mashtaka kuthibitishwa na kabla ya kesi kuanza, Mwendesha Mashtaka anaweza, kwa ruhusa ya Chumba cha Utangulizi, na baada ya kumpa mshtakiwa notisi kuyafanyia mashtaka marekebisho. Ikiwa Mwendesha Mashtaka anaamua kuongeza mashtaka, au kuleta mashtaka mbadala yaliyo makubwa zaidi, lazima mashtaka hayo yasikilizwe na kuthibitishwa chini ya

Copyright © STIC 2010

ibara hii. Baada ya kuanza kesi, Mwendesha Mashtaka anaweza kufuta mashtaka kwa ruhusa ya Chumba cha Kesi.

10. Hati yoyote ya kukamata iliyotolewa hapo awali itakoma kutumika kuhusiana na mashtaka yoyote ambayo hayakuthibitishwa na Chumba cha Utangulizi au yamefutwa na Mwendesha Mashtaka.

11. Mara baada ya mashtaka kuthibitishwa kwa mujibu wa ibara hii, Ofisi ya Rais itaunda Chumba cha Kesi, ambacho, kwa kutegemea aya 9 na ibara 64, aya 4, kitakuwa na wajibu wa kuendesha kesi na kinaweza kufanya shughuli yoyote ya Chumba cha Utangulizi ambayo inahusiana na kesi.

Copyright © STIC 2010

Sehemu VI Kesi

Ibara 62
Mahali pa kesi

Isipokuwa kama imeamuliwa vinginevyo, kesi itafanyiwa kwenye makao makuu ya Mahakama.

Ibara 63
Kesi mbele ya mshtakiwa

1. Mshtakiwa atakuwepo wakati wa kesi.

2. Ikiwa mshtakiwa yupo kwenye Mahakama na anaendelea kuleta vurugu wakati wa kesi, Chumba cha Kesi kinaweza kumwondoa mshtakiwa na kumtengenezea uwezekano wa kusikiliza kesi na kumpa wakili wake maagizo nje ya chumba cha mahakama, kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano, ikihitajika. Hatua kama hizo zitachukuliwa katika hali isiyokuwa ya kawaida tu, baada ya njia nyingine kushindwa na kwa muda unaohitajika tu.

Copyright © STIC 2010

Ibara 64
Shughuli na madaraka ya Chumba cha Kesi

1. Shughuli na madaraka ya Chumba cha Kesi vilivyoelezewa katika ibara hii vitatekelezwa kwa mujibu wa Mkataba huu na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

2. Chumba cha Kesi kitahakikisha kuwa kesi inaendeshwa kwa haki na kwa haraka, na itaendeshwa kwa kuheshimu haki za mshitakiwa na kwa kuzingatia ulinzi wa waathiriwa na mashahidi.

3. Baada ya kukabidhiwa kesi kwa kuiendesha, kwa mujibu wa Mkataba huu, Chumba cha Kesi kilichokabidhiwa kesi hiyo :

   (a) Kitashauriana na pande zinazohusika na kufuata taratibu ambazo ni za lazima katika kuendesha kesi ya haki na kwa haraka ;

   (b) Kitaamua lugha itakayotumika wakati wa kesi ; na

(c) Kwa kutegemea vipengele vingine vyovyote vya Mkataba huu, kitawezesha kupatikana kwa nyaraka na habari ambazo hazikupatikana hapo awali, mapema kabla ya kesi kuanza ili kuwezesha kuwepo kwa matayarisho ya kutosha kwa kesi hiyo.

4. Chumba cha Kesi, ikilazimu, ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi kitayapeleka mambo ya awali kwenye Chumba cha Utangulizi au, kama ni lazima, kwa jaji mwingine wa Tawi la Utangulizi.

5. Baada ya kutoa notisi kwa pande husika, Chumba cha Kesi kinaweza, kikiona inafaa, kuelekeza kwamba mashtaka yaunganishwe au yatenganishwe kuhusiana na mashtaka dhidi ya mshtakiwa zaidi ya mmoja.

6. Katika kufanya shughuli zake kabla ya kesi au wakati wa kesi, Chumba cha Kesi kinaweza, ikilazimu :

(a) Kufanya shughuli zozote za Chumba cha Utangulizi zilizotajwa katika ibara 61, aya 11 ;

Copyright © STIC 2010

(b) Kutaka kuwasilishwa mashahidi na maelezo ya mashahidi na kutolewa kwa nyaraka za ushahidi mwingine kwa madhumuni ya, ikilazimu, kupata msaada wa Nchi kama ilivyoelezwa katika Mkataba huu ;

(c) Kuwezesha kulindwa kwa habari za siri ;

(d) Kuagiza kutolewa ushahidi wa ziada zaidi ya ule uliokusanywa kabla ya kesi au uliotolewa na pande husika wakati wa kesi ;

(e) Kuwezesha kulindwa kwa washtakiwa, mashahidi na waathiriwa ; na

(f) Kuamuru jambo lolote lile muhimu.

7. Kesi itaendeshwa hadharani. Chumba cha Kesi kitaweza kuamua katika hali isiyokuwa ya kawaida, kutaka hatua fulani za kesi ziendeshwe kwa siri kwa madhumuni yaliyoelezewa katika ibara

68 au kulinda habari za siri au nyeti zitakazotolewa wakati wa kutoa ushahidi.

8. (a) Kesi inapoanza, Chumba cha Kesi kitamsomea mshtakiwa mashtaka yaliyothibitishwa hapo awali na Chumba cha Utangulizi. Chumba cha Kesi kitajiridhisha kuwa mshtakiwa ameyaelewa mashtaka. Kitampa mshtakiwa fursa ya kukiri kosa kwa mujibu wa ibara 65, au kukataa kosa.

(b) Wakati wa kesi, jaji anayeendesha kesi atatoa miongozo ya kesi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa kesi inaendeshwa kwa haki na bila upendeleo. Kwa kutegemea maelekezo ya jaji anayeendesha kesi, pande husika zinaweza kutoa ushahidi kwa mujibu wa vipengele vya Mkataba huu.

9. Chumba cha Kesi, miongoni mwa mambo mengine, kitakuwa, na madaraka juu ya maombi ya upande wowote au matakwa yake yenyewe :

Copyright © STIC 2010

(a) Kutoa uamuzi juu ya kukubalika au umuhimu wa ushahidi ; na

(b) Kuchukua hatua zote muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa utulivu wakati wa kusikiliza kesi.

10. Chumba cha Kesi kitahakikisha kuwepo kwa kumbukumbu zote za kesi zenye kuonyesha utaratibu wote wa kesi hiyo, na kwamba kumbukumbu hizo zinawekwa na kutunzwa na Msajili.

Ibara 65
Utaratibu baada ya kukiri kosa

1. Pale mshtakiwa anapokiri kosa kufuatana na ibara 64, aya 8 (a), Chumba cha Kesi kitaamua ikiwa :

(a) Mshtakiwa anaelewa hali na matokeo ya kukiri kosa ;

(b) Mshtakiwa anakiri kosa kwa hiari yake baada ya kushauriana vya kutosha na wakili mtetezi ; na

(c) Kukiri kwa kosa kunaambatana na maelezo ya kesi yaliyomo ndani ya :

(i) Mashtaka yaliyowasilishwa na Mwendesha Mashtaka na aliyokiri mshtakiwa ;

(ii) Hati zozote zitakazowasilishwa na Mwendesha Mashtaka ambazo zinayapa nguvu mashtaka na ambazo mshtakiwa anazikubali ; na

(iii) Ushahidi mwingine wowote, kama vile maelezo ya mashahidi yaliyowasilishwa na Mwendesha Mashtaka au mshtakiwa.

2. Pale Chumba cha Kesi kitakaporidhika kuwa mambo yaliyotajwa katika aya 1 yamethibitishwa, kitafikiria kukiri kwa kosa pamoja na ushahidi mwingine wowote ule wa ziada uliowasilishwa, kuwa vinajenga ukweli unaohitajika ili kuthibitisha kosa la jinai ambalo mshtakiwa amelikiri, na kinaweza kumhukumu mshtakiwa kwa kosa hilo la jinai.

Copyright © STIC 2010

3. Pale ambapo Chumba cha Kesi hakikuridhika kuwa mambo yaliyotajwa katika aya 1 yamethibitishwa, kitachukulia kwamba mshtakiwa hakukiri kosa, na kwa sababu hiyo kitaamuru kuwa kesi iendelee kwa kufuata taratibu za kawaida za kesi zilizoelezewa katika Mkataba huu, na kinaweza kuipeleka kesi kwenye Chumba kingine cha Kesi.

4. Pale ambapo Chumba cha Kesi kinadhani kuwa kinahitaji ukweli zaidi juu ya kesi uwasilishwe kwa ajili ya kupatikana haki, na hasa kwa maslahi ya waathiriwa, Chumba kinaweza :

(a) Kumwomba Mwendesha Mashtaka kuwasilisha ushahidi wa ziada, ikiwa ni pamoja na maelezo ya mashahidi ; au

(b) Kuagiza kwamba kesi iendelee kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa kesi ulioelezewa katika Mkataba huu. Katika hali hiyo, Chumba cha Kesi kitachukulia kwamba mshtakiwa hakukiri kosa, na kinaweza kuipeleka kesi kwenye Chumba kingine cha Kesi.

5. Majadiliano yoyote yale baina ya Mwendesha Mashtaka na upande wa utetezi kuhusu marekebisho ya mashtaka, kukiri kosa, au adhabu itakayotolewa hayatayabana Mahakama.

Ibara 66
Kudhaniwa kutokuwa na hatia

1. Mtu yeyote atadhaniwa kuwa hana hatia mpaka hapo itakapothibitishwa mbele ya Mahakama kuwa ana hatia, kwa mujibu wa sheria inayotumika.

2. Ni wajibu wa Mwendesha Mashtaka kuthibitisha kwamba mshtakiwa ana hatia.

3. Ili kumtia mshtakiwa hatiani, Mahakama lazima iridhike bila ya wasiwasi wowote juu ya kosa la mshtakiwa.

Ibara 67
Haki za mshtakiwa

Copyright © STIC 2010

1. Katika kuamua juu ya shtaka lolote, mshtakiwa atakua na haki ya kusikilizwa hadharani, kwa kuzingatia vipengele vya Mkataba huu, kuwa anasikilizwa kwa haki bila ya upendeleo na kuhakikisha kwa kiwango fulani na kwa usawa kamili yafuatayo :

   (a) Kuarifiwa kinaganaga na kwa haraka hali, sababu na yaliyomo katika mashtaka kwa lugha ambayo mshtakiwa anaielewa vema na kuisema ;

   (b) Kupewa muda wa kutosha pamoja na kuwezeshwa kujitayarisha kwa utetezi na kuwasiliana atakavyo na wakili aliyemchagua kwa hiari yake na anayemwamini ;

   (c) Kufikishwa mahakamani bila ucheleweshaji usiokuwa na sababu ;

   (d) Kwa kutegemea ibara 63, aya 2, kuwepo wakati wa kesi, kujitetea mwenyewe binafsi au kupitia wakili wake ambaye atamchagua yeye mwenyewe, kupewa taarifa, kuarifiwa juu ya haki ya kuwa na wakili ikiwa mshtakiwa hana wakili aliyepatiwa na Mahakama, katika hali ambayo

upatikanaji wa haki unahitaji, na bila ya malipo ikiwa mshtakiwa hana uwezo wa kutosha wa kufanya malipo ;

(e) Kuhoji au kusababisha kuhojiwa mashahidi walio dhidi yake na kupewa haki ya mtu mwingine kuwepo wakati wa kuwahoji mashahidi kwa niaba yake kwa masharti yale yale ya mashahidi walio dhidi yake. Mshtakiwa ataruhusiwa vile vile kuwasilisha utetezi na ushahidi mwingine unaokubalika chini ya Mkataba huu ;

(f) Kupatiwa msaada wa mkalimani hodari na tafsiri nyingine zilizo za lazima bila ya malipo ili kukidhi mahitaji ya kupatikana kwa haki, ikiwa utaratibu wowote ule wa Mahakama au nyaraka zitakazowasilishwa kwenye Mahakama hazipo katika lugha ambayo mshtakiwa anaielewa vizuri na kuisema ;

(g) Kutolazimishwa kutoa maelezo au kukiri kosa na kubakia kimya, bila ukimya huo kuchukuliwa katika kuamua kuwa na kosa au kutokuwa na kosa ;

Copyright © STIC 2010

(h) Kutoa maelezo ya maandishi au ya mdomo katika utetezi wake bila kiapo ; na

(i) Kutobebeshwa mzigo wa kutoa uthibitisho au jukumu lolote la kukanusha.

2. Zaidi ya mengine yoyote yale yaliyoelezewa katika Mkataba huu, Mwendesha Mashtaka, kwa haraka iwezekanavyo, atauarifu upande wa utetezi, ushahidi uliopo upande wa Mwendesha Mashtaka, ambao anaamini kuwa unaonyesha dalili za mshtakiwa kutokuwa na hatia au kupunguza hatia ya mshtakiwa, au utakaoathiri hadhi ya ushahidi wa upande wa mashtaka. Inapotokea shaka kuhusiana na utekelezwaji wa aya hii, Mahakama itaamua.

Ibara 68
Kuwahami waathiriwa na mashahidi na kushiriki kwao kwenye kesi

1. Mahakama itachukua hatua zinazofaa ili kuhami usalama, hali ya kimwili na ya kisaikolojia, heshima na faragha ya waathiriwa na mashahidi. Katika kufanya hivyo, Mahakama itazingatia mambo yote muhimu, ikiwa ni pamoja na umri, jinsia kama ilivyoelezewa katika ibara 7, aya 3, na afya, na hali ya kosa la jinai, na hasa, lakini si hilo tu, pale kosa la jinai linapohusu ukatili wa kijinsia, au ukatili dhidi ya watoto. Mwendesha Mashtaka atachukua hatua kama hizo hasa wakati wa upelelezi na wakati wa kuendesha kesi ya makosa kama hayo ya jinai. Hatua hizo hazitamkandamiza au kwenda kunyume na haki za mshtakiwa na kuendeshwa kesi kwa haki na bila ya upendeleo.

2. Ikiwa ni kinyume na misingi ya kawaida ya kuendesha kesi hadharani kama inavyoelezewa katika ibara 67, Vyumba vya Mahakama vinaweza, ili kuwahami waathiriwa na mashahidi au mshtakiwa, kuendesha utaratibu wowote ule wa kesi kwa siri au kuwasilisha ushahidi kwa kutumia njia ya eletroniki au njia yoyote ile maalumu. Hatua kama hizo zitatekelezwa hasa kwa mwathiriwa wa ukatili wa kijinsia au mtoto ambaye ni mwathiriwa au shahidi, ila kama imeagizwa vinginevyo na Mahakama kwa kuzingatia hali zote, hasa maoni ya mwathiriwa au shahidi.

3. Pale ambapo maslahi binafsi ya waathiriwa yanaguswa, Mahakama itaruhusu maoni na wasiwasi wao viwasilishwe na kufikiriwa wakati wa hatua za utaratibu wa kesi, ambao Mahakama itaona unafaa na kwa namna ambayo haitamkandamiza au kwenda kinyume na haki za mshtakiwa na kesi inayoendeshwa kwa haki na bila ya upendeleo. Maoni na wasiwasi kama huo vinaweza kuwasilishwa na wawakilishi wa kisheria wa waathiriwa pale ambapo Mahakama itaona inafaa, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

4. Kitengo cha Waathiriwa na Mashahidi kinaweza kumshauri Mwendesha Mashtaka na Mahakama juu ya njia zinazofaa za kuhami, mipango ya usalama, ushauri na msaada, kama ilivyoelezewa katika ibara 43, aya 6.

Copyright © STIC 2010

5. Pale ambapo kutangazwa kwa ushahidi au habari kufuatana na wa Mkataba huu, kutapelekea kuwepo hatari kubwa ya usalama wa shahidi na familia yake, Mwendesha Mashtaka anaweza, kwa madhumuni ya utaratibu wowote ule uliofuatwa kabla ya kuanza kwa kesi, kuzuia ushahidi au habari hiyo, na badala yake kuwasilisha muhtasari wake. Hatua kama hizo zitatekelezwa kwa namna ambayo haitamkandamiza au kwenda kinyume na haki za mshtakiwa na kuendeshwa kesi kwa haki na bila ya upendeleo.

6. Nchi inaweza kupeleka maombi ya kutaka zichukuliwe hatua za lazima kuhusiana na kuwahami watumishi wake au makachero wake na kulinda habari za siri au nyeti.

Ibara 69
Ushahidi

Copyright © STIC 2010

1. Kabla ya kutoa maelezo, kila shahidi, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, atakula kiapo juu ya ukweli wa ushahidi utakaotolewa na shahidi huyo.

2. Maelezo ya shahidi katika kesi lazima yatolewe na shahidi mwenyewe isipokuwa kwa namna ya hatua zilizoelezewa katika ibara 68 au katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi. Mahakama inaweza kumruhusu vilevile shahidi kutoa maelezo ya mdomo au yaliyonaswa kwa kanda kwa njia ya video au kwa teknolojia ya sauti, pamoja na kuwasilisha nyaraka au maelezo yaliyoandikwa, kwa kutegemea Mkataba huu na kulingana na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi. Hatua hizi hazitamkandamiza wala kwenda kinyume na haki za mshtakiwa.

3. Pande husika zinaweza kuwasilisha ushahidi unaohusiana na kesi, kwa mujibu wa ibara 64. Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuomba kuwasilishwa kwa ushahidi wote ambao inahisi ni wa lazima katika kutafuta ukweli.

4. Mahakama inaweza kuamua juu ya kuhusika au kukubalika kwa ushahidi wowote kwa kutilia maanani, miongoni mwa mambo mengine, thamani ya mchango wa ushahidi huo katika kesi na madhara yoyote ambayo ushahidi huo unaweza kuyasababisha katika kesi inayoendeshwa kwa haki au kwa tathmini ya haki ya

maelezo ya shahidi, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

5. Mahakama itaheshimu na kutekeleza kanuni za kutunza siri kama ilivyo katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

6. Mahakama haitataka uthibitisho wa mambo yanayojulikana na kila mtu lakini inaweza kuyaweka kwenye taarifa za kimahakama.

7. Ushahidi uliopatikana kwa njia za ukiukwaji wa Mkataba huu au haki za binadamu zinazotambulika kimataifa, hautakubaliwa ikiwa :

   (a) Ukiukwaji huo unasababisha kuwepo shaka juu ya ukweli wa ushahidi huo ; au

   (b) Kukubalika kwa ushahidi huo kutakuwa ni kinyume na kwa kiwango kikubwa, utaathiri hadhi ya mwenendo wa kesi.

Copyright © STIC 2010

8. Katika kuamua juu ya kuhusika au kukubalika kwa ushahidi uliokusanywa na Nchi, Mahakama haitaamua kutumia sheria za Nchi hiyo.

Ibara 70
Makosa dhidi ya utoaji wa haki

1. Mahakama itakua na uwezo wa kisheria kwa makosa yafuatayo dhidi ya utoaji wake wa haki pindi makosa hayo yakitendwa kwa makusudi :

   (a) Kutoa maelezo ya uongo kwa mtu aliyekula kiapo kwa mujibu wa ibara 69, aya 1, kusema ukweli ;

   (b) Kutoa ushahidi ambao upande husika unajua kuwa ni wa uwongo au ni wa kughushi ;

   (c) Kumshawishi shahidi kwa kumhonga, kumzuia au kumwingilia shahidi asihudhurie au kutoa maelezo, kulipiza kisasi dhidi ya shahidi kwa kutoa maelezo au

kuharibu ushahidi, kuvuruga au kuingilia kazi ya kukusanya ushahidi ;

(d) Kumzuia, kumtisha au kumshawishi kwa kumhonga ofisa wa Mahakama, kwa madhumuni ya kumlazimisha au kumshawishi ofisa huyo asitekeleze au asitekeleze vizuri wajibu wake ;

(e) Kulipiza kisasi dhidi ya ofisa wa Mahakama kutokana na kazi aliyoifanya ofisa huyo au iliyofanywa na ofisa mwingine ;

(f) Kuomba au kupokea rushwa akiwa kama ofisa wa Mahakama kuhusiana na kazi zake rasmi.

2. Misingi na taratibu zinazotawala shughuli za kisheria za Mahakama kwa makosa ya jinai yaliyokuwa chini ya ibara hii, zitakuwa zile zilizotajwa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi. Masharti ya kutoa ushirikiano wa kimataifa kwa Mahakama kuhusiana na taratibu zake zilizotajwa katika ibara hii zitatawaliwa na sheria za ndani za Nchi iliyoombwa.

Copyright © STIC 2010

3. Mtu anapopatikana na hatia, Mahakama inaweza kutoa hukumu ya kifungo kisichozidi miaka mitano, au faini kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, au yote mawili.

4. (a) Kila Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itazipanua sheria zake za makosa ya jinai zinazotoa adhabu dhidi ya hadhi ya upelelezi wake au utaratibu wake wa kisheria na kuwa ni makosa dhidi ya utoaji wa haki uliotajwa katika ibara hii ikiwa umefanyika katika eneo la Nchi yake au na raia wake ;

(b) Kwa ombi la Mahakama, kila itakapoonekana inafaa, Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itaiwasilisha kesi hiyo kwa mamlaka zake zenye uwezo kwa madhumuni ya kufungua mashtaka. Mamlaka hizo zitazishughulikia kesi hizo kwa bidii na kutoa nyenzo za kutosha ili ziweze kuendeshwa kwa ufanisi.

Ibara 71
Adhabu kwa utovu wa nidhamu kwenye Mahakama

1. Mahakama inaweza kuwaadhibu watu walio katika Mahakama watakaoonyesha utovu wa nidhamu ikiwa ni pamoja na kuvuruga utaratibu wake au kukataa kwa makusudi kutii maelekezo, kwa adhabu nyingine ambayo si kifungo, kama vile kuwatoa kwa muda au moja kwa moja kutoka kwenye chumba cha Mahakama, kuwapiga faini au adhabu nyingine kama hizo zilizoelezewa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

2. Taratibu zinazotawala utoaji wa adhabu zilizotajwa katika aya 1 zitakuwa ni zile zilizotajwa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Ibara 72
Kulinda habari zinazohusiana na usalama wa taifa

Copyright © STIC 2010

1. Ibara hii inahusu pale ambapo kutolewa habari au nyaraka za Nchi, kwa maoni ya Nchi hiyo, kutaathiri maslahi ya usalama wake wa taifa. Kesi hizo ni pamoja na zile zilizo chini ya ibara 56, aya 2 na 3, ibara 61, aya 3, ibara 64, aya 3, ibara 67, aya 2, ibara 68, aya 6, ibara 87, aya 6, na ibara 93, pamoja na kesi nyingine zitakazojitokeza katika hatua yoyote ile ya utaratibu utakaohitaji kutolewa habari kama hizo.

2. Ibara hii itahusu pia pale ambapo mtu aliyeombwa kutoa habari au ushahidi amekataa kufanya hivyo au amelipeleka ombi hilo kwenye Nchi husika kwa sababu kuzitoa habari hizo kutaathiri maslahi ya usalama wa taifa wa Nchi na Nchi husika inathibitisha kuwa kwa maoni yake, kutolewa kwa habari hizo kutaathiri maslahi ya usalama wake wa taifa.

3. Hakuna chochote kilichomo katika ibara hii kitakachoathiri mahitaji ya kutunza siri yanayohusiana na Ibara 54, aya 3 (e) na (f), au utekelezwaji wa Ibara 73.

4. Kama Nchi itabaini kwamba habari au nyaraka za Nchi hiyo zina, au zinaweza kutangazwa katika hatua yoyote ile ya utaratibu, na inaamini kuwa kutangazwa huko kutaathiri maslahi ya usalama

wake wa taifa, Nchi hiyo itakuwa na haki ya kuingilia kati ili kupata usuluhishi wa suala hilo kwa mujibu wa Ibara hii.

5. Ikiwa kwa maoni ya Nchi kutolewa kwa habari hizo kutaathiri maslahi ya usalama wake wa taifa, Nchi hiyo itachukua hatua zote zinazofaa, na itafanya hivyo kwa kushirikiana na Mwendesha Mashtaka, upande wa utetezi au Chumba cha Utangulizi au Chumba cha Kesi, kama itakavyohitajika, katika kutafuta njia za kulitatua suala hilo kwa njia ya ushirikiano. Hatua hizo ni pamoja na :

   (a) Kurekebisha au kulifafanua zaidi ombi ;

   (b) Uamuzi wa Mahakama kuhusu umuhimu wa habari za ushahidi unaotakiwa, au uamuzi ikiwa ushahidi huo, japo ni muhimu, unaweza kupatikana au umepatikana kutoka katika chanzo ambacho si Nchi iliyoombwa ;

   (c) Kupata habari au ushahidi kutoka katika chanzo tofauti au kwa namna tofauti ; au

   (d) Makubaliano juu ya masharti kuhusu namna msaada huo unavyoweza kutolewa ikiwa ni pamoja na, miongoni mwa mambo mengine, kutoa mihtasari au uhariri, kupunguza kiwango cha kutoa habari hizo, kutumia habari hizo katika kikao cha siri au kusikilizwa na upande moja tu, au njia nyingine za kulinda habari na ushahidi huo zinazokubalika ndani ya Mkataba huu na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

6. Mara baada ya kuchukuliwa hatua zote zinazofaa kulitatua suala hilo kwa njia ya ushirikiano, na ikiwa Nchi bado inadhani hakuna njia yoyote au masharti yoyote yatakayoifanya Nchi hiyo kutoa habari au nyaraka hizo bila kuathiri maslahi ya usalama wake wa taifa, Nchi hiyo itamwarifu hivyo Mwendesha Mashtaka au Mahakama juu ya sababu maalumu za uamuzi wake, ila kama maelezo maalumu ya sababu hizo nayo pia yataathiri maslahi ya usalama wa taifa wa Nchi hiyo.

Copyright © STIC 2010

7. Baada ya hapo, ikiwa Mahakama itaamua kuwa ushahidi huo unahusu na ni wa lazima katika kutoa hukumu ya kutenda kosa au kutotenda kosa mshtakiwa, Mahakama inaweza kufanya mambo yafuatayo :

(a) Pale ambapo panatakiwa zitolewe habari au nyaraka kufuatana na ombi la kushirikiana lililo chini ya Ibara 9 au hali iliyoelezewa katika aya 2, na kwamba Nchi imetumia kipengele cha sababu ya kukataa iliyoelezewa katika ibara 93, aya 4 :

(i) Mahakama inaweza, kabla ya kufikia uamuzi wowote uliotajwa katika aya 7, (a) (ii), kuomba mashauriano zaidi kwa madhumuni ya kufikiria malalamiko ya Nchi husika, ambayo yatajumuisha, kama inavyofaa, usikilizwaji kwa siri na usikilizwaji wa upande mmoja ;

(ii) Ikiwa Mahakama imeridhika kwamba kwa kutumia kipengele cha sababu ya kukataa chini ya Ibara 93, aya 4, kwa hali ya kesi hiyo, Nchi iliyoombwa haifanyi wajibu wake kama ilivyo katika Mkataba huu, Mahakama inaweza kulishughulikia suala hilo kwa mujibu wa Ibara 87, aya 7, ikionyesha wazi sababu za uamuzi wake ; na

(iii) Mahakama inaweza kufanya uamuzi katika kesi ya mshtakiwa, juu ya kuwepo au kutokuwepo ukweli, kama itakavyofaa kulingana na hali halisi ; au

(b) Katika hali nyingine zozote :

(i) Kuamuru kutolewa ; au

(ii) Itakapotaka zisitolewe, kufanya uamuzi wa kesi ya mshtakiwa juu ya kuwepo au kutokuwepo ukweli, kama itakavyokuwa inafaa kulingana na hali halisi.

Copyright © SLIC 2010

Ibara 73
Habari au nyaraka kutoka kwa mtu wa tatu

Ikiwa Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inaombwa na Mahakama kutoa habari au nyaraka zilizo chini ya mamlaka yake, inazozimiliki au inazozidhibiti, ambazo imepewa kwa kuaminiwa na Nchi, shirika baina ya serikali mbalimbali, au shirika la kimataifa, itaomba idhini kutoka kwa mtoaji wa asili kutoa nyaraka au habari hizo. Ikiwa mtoaji wa asili wa habari hizo ni Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, ama itakubali kuzitoa habari na nyaraka hizo, au kutatua suala la kuzitoa na Mahakama kwa kutegemea vipengele vya ibara 72. Ikiwa mtoaji wa asili wa habari au nyaraka hizo si Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama na imekataa kutoa habari au nyaraka hizo, Nchi iliyoombwa itaiarifu Mahakama kuwa haiwezi kutoa habari au nyaraka hizo kwa sababu ya kulazimika kwake kutunza siri kulikokuwepo baina yake na mtoaji wa asili.

Copyright © STIC 2010

Ibara 74
Mahitaji ya kufikia uamuzi

1. Majaji wote wa Chumba cha Kesi watakuwepo katika kila hatua ya kesi na kwa kipindi chote cha majadiliano. Ofisi ya Rais inaweza, kufuatana na kesi moja moja kumkabidhi, kwa kadri wanavyoweza kupatikana, jaji mbadala, mmoja au zaidi ya mmoja kuwepo katika kila hatua ya kesi na kuchukua nafasi ya mjumbe wa Chumba cha Kesi ikiwa mjumbe huyo hawezi kuhudhuria.

2. Uamuzi wa Chumba cha Kesi utatokana na tathmini ya ushahidi na utaratibu wote. Uamuzi huo hautapindukia kiwango cha ukweli na hali iliyoelezewa katika mashtaka au marekebisho ya mashtaka. Mahakama inaweza kufanya uamuzi wake kulingana na ushahidi uliowasilishwa na kujadiliwa kwenye Mahakama wakati wa kesi tu.

3. Majaji watajitahidi kufikia uamuzi wao kwa kukubaliana kwa kauli moja. Wakishindwa kufanya hivyo uamuzi utatolewa kwa wingi wa kura.

4. Majadiliano ya majaji wa Chumba cha Kesi yatakuwa ya siri.

5. Uamuzi utakuwa kwa maandishi na utakuwa na taarifa yenye hoja za yale ambayo yameonekana na majaji wa Chumba cha Kesi juu ya ushahidi na uamuzi. Chumba cha Kesi kitatoa uamuzi mmoja. Pale ambapo hawakukubaliana kwa kauli moja, uamuzi wa Chumba cha Kesi utakuwa na maoni ya walio wengi na walio wachache. Uamuzi au muhtasari wa uamuzi huo, utatolewa kwenye kesi ya wazi.

Ibara 75
Malipo kwa waathiriwa

1. Mahakama itatengeneza utaratibu unaohusiana na malipo, kwa au kuhusiana na waathiriwa, ikiwa ni pamoja na kuwarudishia mali zao, fidia na kurudia katika hali ya maisha yao ya kawaida. Kwa misingi hiyo, Mahakama inaweza, katika uamuzi wake ama kwa kuombwa au kwa uwezo wake kwa hali isiyokuwa ya kawaida, kuamua kiwango na ukubwa wa uharibifu wowote ule, hasara na kujeruhiwa, au kuhusiana na waathiriwa, na itaelezea kuhusu misingi ya kufanya uamuzi huo.

Copyright © STIC 2010

2. Mahakama inaweza kuamuru moja kwa moja dhidi ya mtu aliyepatikana na hatia ikielezea malipo yanayofaa kwa au kuhusiana na waathiriwa, ikiwa ni pamoja na kuwarudishia mali zao, fidia na kurudia katika hali ya maisha yao ya kawaida. Pale inapofaa, Mahakama inaweza kuamuru kwamba malipo yafanyike kupitia Mfuko wa Dhamana ulioelezewa katika ibara 79.

3. Kabla ya kuamuru, chini ya ibara hii, Mahakama inaweza kukaribisha na itazingatia malalamiko kutoka kwa au kwa niaba ya mtu aliyepatikana na hatia, waathiriwa, watu au Nchi zinazofuatilia suala hilo.

4. Katika kutumia madaraka yake chini ya ibara hii, Mahakama inaweza, baada ya kumpata mtu na hatia kwa kosa la jinai, kufuatia uwezo wa kisheria wa Mahakama, kuamua ikiwa, ili kutekeleza maagizo itakayoyatoa chini ya ibara hii, kuna haja ya kuchukua hatua zilizo chini ya ibara 93, aya 1.

5. Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itatekeleza uamuzi wake chini ya ibara hii kama kwamba vipengele vya ibara 109 vinaihusu ibara hii.

6. Hakuna kitu chochote katika ibara hii ambacho kitatafsiriwa kuwa kinakandamiza haki za waathiriwa chini ya sheria ya kitaifa au ya kimataifa.

Ibara 76
Kutoa adhabu

1. Inapotolewa adhabu, Chumba cha Kesi kitafikiria adhabu muafaka itakayotolewa na itatilia maanani ushahidi uliowasilishwa na maelezo yaliyotolewa wakati wa kesi ambayo yanahusiana na adhabu iliyotolewa.

2. Isipokuwa pale ambapo ibara 65 inahusika na kabla ya kumaliza kesi, Chumba cha Kesi kwa utashi wake na kwa ombi la Mwendesha Mashtaka au mshtakiwa, kinaweza kusikiliza zaidi kesi au kusikiliza ushahidi wowote ule wa ziada au maelezo yanayohusiana na adhabu, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

3. Pale ambapo aya 2 inatumika, malalamiko yoyote yale chini ya ibara 75 yatasikilizwa pale kesi itakaposikilizwa zaidi kama ilivyo katika aya 2 na, ikilazimu, wakati wowote ule ambao kesi itasikilizwa zaidi.

4. Adhabu itatamkwa hadharani na, pale inapowezekana, mbele ya mshtakiwa.

Copyright © STIC 2010

Sehemu VII Adhabu

Ibara 77
Adhabu zinazoweza kutolewa

1. Kwa kutegemea Ibara 110, Mahakama inaweza kutoa moja ya adhabu zifuatazo dhidi ya mtu aliyepatikana na hatia kwa kosa la jinai lililotajwa katika ibara 5 ya Mkataba huu :

   (a) Adhabu ya kifungo kwa muda wa miaka iliyoainishwa, ambayo haitazidi miaka 30 ; au

   (b) Adhabu ya kifungo cha maisha kilichohalalishwa na ukubwa wa kosa la jinai na hali binafsi ya mtu aliyepatikana na hatia.

2. Zaidi ya adhabu ya kifungo, Mahakama inaweza kuamuru :

   (a) Kupiga faini kulingana na kigezo kilichoelezewa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi ;

   (b) Kunyan'ganya mapato, mali na rasilimali zilizopatikana moja kwa moja au kwa kificho kutokana na kosa hilo la jinai, bila ya kuathiri haki za mtu wa tatu mwenye kuaminika.

Copyright © STIC 2010

Ibara 78
Kuamua adhabu

1. Katika kuamua adhabu, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, Mahakama itatilia maanani mambo kama vile ukubwa wa kosa la jinai na hali binafsi ya mtu aliyepatikana na hatia.

2. Katika kutoa adhabu ya kifungo, Mahakama itaupunguza, kama upo, muda ambao mshtakiwa amekuwa kizuizini kwa amri ya Mahakama. Mahakama inaweza kupunguza muda wote ule ambao mshtakiwa amekuwa kizuizini kuhusiana na kosa la jinai alilolifanya.

3. Ikiwa mtu amepatikana na hatia kwa kosa la jinai zaidi ya moja, Mahakama itatamka adhabu kwa kila kosa la jinai na adhabu ya

jumla itakayoainisha muda wa jumla wa kutumikia kifungo. Muda huo hautakuwa chini ya muda mrefu zaidi wa adhabu iliyotajwa na hautazidi kifungo cha miaka 30 au cha maisha kulingana na ibara 77, 1 (b).

Ibara 79
Mfuko wa Dhamana

1. Mfuko wa Dhamana utaanzishwa kwa uamuzi wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama kwa maslahi ya waathiriwa wa makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, na familia za waathiriwa hao.

2. Mahakama inaweza kuamuru pesa na mali nyingine zilizokusanywa kwa njia ya faini au kwa kunyang'anya zihawilishwe, kwa amri ya Mahakama, kwenda kwenye Mfuko wa Dhamana.

3. Mfuko wa Dhamana utaendeshwa kwa mujibu wa vigezo vitakavyoamriwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

Copyright © STIC 2010

Ibara 80
Kutozuia kutumika kwa adhabu na sheria za kitaifa

Hakuna chochote katika Sehemu hii kinachoathiri Nchi kutumia adhabu zilizoelezwa katika sheria zao za kitaifa, wala sheria za Nchi ambazo hazitoi adhabu zilizoelezewa katika sehemu hii.

Sehemu VIII Rufaa na marudio

Ibara 81
Rufaa dhidi ya uamuzi wa kuachia au kutia hatiani au dhidi ya hukumu

1. Uamuzi ulio chini ya ibara 74 unaweza kukatiwa rufaa kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi kama ifuatavyo :

   (a) Mwendesha Mashtaka anaweza kukata rufaa kwa yoyote ya sababu zifuatazo :

      (i) Kosa la kiutaratibu ;

      (ii) Kosa la ukweli ; au

      (iii) Kosa la kisheria ;

Copyright © STIC 2010

   (b) Mtu aliyepatikana na hatia, au Mwendesha Mashtaka kwa niaba ya mtu huyo anaweza kukata rufaa kwa yoyote ya sababu zifuatazo :

      (i) Kosa la kiutaratibu ;

      (ii) Kosa la ukweli ;

      (iii) Kosa la kisheria ; au

      (iv) Sababu nyingine yoyote itakayoweza kuathiri hali ya haki au kuaminika kwa taratibu au uamuzi.

2. (a) Adhabu inaweza kukatiwa rufaa, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, na Mwendesha Mashtaka au na mtu aliyepatikana na hatia, kwa sababu ya kutokuwepo uwiano kati ya kosa la jinai na adhabu ;

   (b) Ikiwa wakati wa kukata rufaa dhidi ya adhabu iliyotolewa, Mahakama inaona kwamba kuna sababu zitakazoifanya hukumu iwekwe pembeni, yote kwa jumla au sehemu ya hukumu hiyo, inaweza kuwaita Mwendesha Mashtaka na

mtu aliyepatikana na hatia ili kutoa sababu chini ya ibara 81, aya 1 (a) au (b), na inaweza kutoa uamuzi wa kutia hatiani chini ya ibara 83 ;

(c) Utaratibu huo huo unatumika pale Mahakama, inapokuwepo rufaa dhidi ya hukumu tu, inadhani kwamba kuna sababu za kuipunguza adhabu chini ya aya 2 (a).

3. (a) Isipokuwa kama Chumba cha Kesi kitaamua vinginevyo, mtu aliyepatikana na hatia atabaki kizuizini akisubiri rufaa ;

(b) Pale ambapo muda ambao amewekwa kizuizini mtu aliyepatikana na hatia unazidi muda wa adhabu ya kifungo iliyotolewa, mtu huyo ataachiliwa, isipokuwa kama Mwendesha Mashtaka anakata rufaa vile vile, kuachiliwa kwa mtu huyo kutategemea masharti yaliyo chini ya aya (c) hapo chini ;

Copyright © STIC 2010

(c) Akiachiliwa, mshtakiwa atatolewa mara moja, kwa kutegemea yafuatayo :

(i) Katika hali isiyokuwa ya kawaida, na kwa kuzingatia miongoni mwa mambo mengine wasiwasi wa mtu huyo kutoroka, ukubwa wa kosa la jinai ambalo mtu huyo ameshtakiwa, na uwezekano wa rufaa hiyo kufanikiwa, Chumba cha Kesi, kwa ombi la Mwendesha Mashtaka, kinaweza kuendelea kumweka mtu huyo kizuizini kikisubiri rufaa ;

(ii) Uamuzi utakaotolewa na Chumba cha Kesi chini ya aya ndogo (c) (i) unaweza kakatiwa rufaa kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

4. Kwa kutegemea vipengele vya aya 3 (a) na (b), utekelezaji wa hukumu utazuiliwa kwa muda katika kipindi kilichoruhusiwa kwa ajili ya kukata rufaa na kwa muda ambao rufaa itakuwa inasikilizwa.

Ibara 82
Rufaa dhidi ya maamuzi mengine

1. Upande wowote ule unaweza kukata rufaa dhidi ya maamuzi yoyote yale kati ya maamuzi yafuatayo kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi :

   (a) Uamuzi kuhusiana na uwezo wa kisheria na kukubalika ;

   (b) Uamuzi wa kukubali au kukataa kumwachia mtu anayepelelezwa au anayeshtakiwa ;

   (c) Uamuzi wa Chumba cha Utangulizi kuchukua hatua kwa utashi wake chini ya ibara 56 (3) ;

   (d) Uamuzi unaolihusu jambo litakaloathiri kwa kiwango kikubwa hali ya kutoa haki au uendeshwaji haraka wa taratibu au matokeo ya kesi ambayo kwa maoni ya Chumba cha Utangulizi au Chumba cha Kesi, utatuzi wa haraka wa Chumba cha Kesi unaweza kuharakisha taratibu za kesi kwa namna yenye maslahi.

Copyright © STIC 2010

2. Uamuzi wa Chumba cha Utangulizi chini ya ibara 57, aya 3 (d) unaweza kukatiwa rufaa na Nchi husika au na Mwendesha Mashtaka, kwa ruhusa ya Chumba cha Utangulizi. Rufaa hiyo itasikilizwa kwa haraka.

3. Rufaa kama ilivyo haitakuwa na nguvu ya kuizuia kesi ila kama Chumba cha Rufaa kitaagiza hivyo, baada ya kuombwa, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

4. Mwakilishi wa kisheria wa waathiriwa, mtu aliyepatikana na hatia au mmiliki mwenye kuaminika wa mali iliyohusiswha na agizo lililo chini ya ibara 75 anaweza kukata rufaa dhidi ya agizo hilo la malipo kama ilivyoelezewa kwenye Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Ibara 83
Taratibu za kukata rufaa

1. Kwa madhumuni ya taratibu zilizo chini ya ibara 81 na katika ibara hii, Chumba cha Rufaa kitakuwa na madaraka yote ya Chumba cha Kesi.

2. Ikiwa Chumba cha Rufaa kitabaini kuwa taratibu zilizokatiwa rufaa hazikuwa za haki kwa namna ambayo imeathiri kuaminika kwa uamuzi na hukumu, au uamuzi au hukumu iliyokatiwa rufaa umeathiriwa kimaslahi kwa kosa la ukweli au sheria au kosa la utaratibu, kinaweza :

   (a) Kubadili au kurekebisha uamuzi au hukumu ; au

   (b) Kuamuru kufunguliwa kesi mpya kwenye Chumba tofauti cha kesi.

   Kwa madhumuni haya, Chumba cha Rufaa kinaweza kulirudisha jambo linalohusu ukweli kwenye Chumba cha Kesi cha awali ili kuamua jambo hilo na kutoa ripoti ifaavyo, au kinaweza kuitisha ushahidi ili kuamua jambo hilo. Pale ambapo uamuzi au hukumu imekatiwa rufaa na mtu aliyepatikana na hatia tu, au na Mwendesha Mashtaka kwa niaba ya mtu huyo, hauwezi kufanyiwa marekebisho yatakayomletea madhara.

3. Ikiwa katika kukata rufaa dhidi ya hukumu Chumba cha Rufaa kitabaini kwamba adhabu hailingani na kosa la jinai, kinaweza kubadilisha adhabu hiyo kwa mujibu wa Sehemu 7.

4. Hukumu ya Chumba cha Rufaa itafikiwa kwa wingi wa majaji na itatolewa kwenye mahakama ya wazi. Hukumu hiyo itaelezea sababu ilizozitegemea. Pale ambapo majaji hawatakubaliana kwa kauli moja, hukumu ya Chumba cha Rufaa itakuwa na maoni ya majaji wengi na wachache, lakini jaji anaweza kutoa maoni yake binafsi au tofauti kuhusu suala la kisheria.

5. Chumba cha Rufaa kinaweza kutoa hukumu yake bila ya kuwepo mtu aliyekutwa hana hatia au kupatikana na hatia.

Copyright © STIC 2010

Ibara 84
Marudio ya kutiwa hatiani au adhabu

1. Mtu aliyepatikana na hatia au, baada ya kufa, mwenzi, watoto, wazazi au mtu aliyekuwa hai wakati wa kifo cha mshtakiwa na aliyepewa maagizo ya maandishi kutoka kwa mshtakiwa kuleta madai hayo, au Mwendesha Mashtaka kwa niaba ya mtu huyo, anaweza kukiomba Chumba cha Rufaa kiipitie upya hukumu ya mwisho ya kutiwa kwake hatiani au adhabu, kwa sababu :

   (a) Umegunduliwa ushahidi mpya ambao :

      (i) Haukupatikana wakati wa kesi na kutopatikana huko hakukusababishwa kwa namna yoyote na upande unaofanya maombi hayo ; na

      (ii) Una umuhimu wa kutosha kiasi ambacho kama ungalithibitishwa wakati wa kesi, kungelikuwepo na uwezekano wa kusababisha kutolewa hukumu tofauti ;

   (b) Imegundulika upya kuwa ushahidi mkubwa uliotiliwa maanani wakati wa kesi na ndio ambao utiaji hatiani uliutegemea, ulikuwa ni wa uongo, wa kughushi au wa udanganyifu ;

   (c) Jaji mmoja au zaidi ambaye ameshiriki katika kumtia mtu hatiani au kuthibitisha mashtaka amefanya, katika hali hiyo, kitendo cha ukiukaji mkubwa wa nidhamu au uvunjaji mkubwa wa maadili ya kazi wenye uzito wa kuhalalisha kuondolewa kazini kwa jaji au majaji hao chini ya ibara 46.

2. Chumba cha Rufaa kitalitupilia mbali ombi ikiwa kinadhani kwamba ombi hilo halina msingi wowote. Ikiwa kitaamua kwamba ombi hilo ni lenye kustahili kama kitakavyoona inafaa :

   (a) Kitaitisha tena Chumba cha Kesi cha awali ;

   (b) Kitaunda Chumba kipya cha kesi ; au

Copyright © STTC 2010

(c) Kitabaki na madaraka ya kisheria juu ya jambo hilo ili baada ya kuzisikiliza tena pande husika, kwa namna ilivyoelezewa kwenye Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, ili kufikia uamuzi kama hukumu hiyo irudiwe.

Ibara 85
Fidia kwa mtu aliyekamatwa au aliyepatikana na hatia

1. Mtu yeyote ambaye amewahi kukamatwa au kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria atakuwa na haki ya lazima ya kulipwa fidia.

2. Ikiwa mtu, kufuatana na uamuzi wa mwisho, amepatikana na hatia kwa kosa la jinai, na baadaye kupatikana kwake na hatia kukarudiwa kwa sababu ukweli mpya uliogunduliwa umeonyesha waziwazi kuwa kumekuwepo na ukiukwaji wa haki, mtu aliyeadhibiwa kutokana na kupatikana huko na hatia, atalipwa fidia kwa mujibu wa sheria, ila kama itathibitishwa kuwa kutopatikana huko kwa wakati kwa ukweli uliokuwa haujulikani kumesababishwa kwa jumla au kwa kiasi fulani na yeye mwenyewe.

Copyright © STTC 2010

3. Katika hali isiyo ya kawaida, pale Mahakama inapopata ukweli usiokuwa na shaka unaoonyesha kuwa pamekuwepo na ukiukwaji wa haki mkubwa na ulio wazi, inaweza kwa uwezo wake kutoa fidia kwa mtu aliyeachiliwa kutoka kizuizini kufuatia uamuzi wa mwisho wa kumwachia au kusitisha utaratibu mzima wa kesi kwa sababu hiyo, kufuatana na vigezo vilivyotolewa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Sehemu IX Ushirikiano wa kimataifa na msaada wa kisheria

Ibara 86
Wajibu wa jumla wa kushirikiana

Kwa mujibu wa vipengele vya Mkataba huu, Nchi zinazounda Mahakama zitashirikiana kikamilifu na Mahakama katika kufanya upelelezi na kuyafungulia mashtaka makosa ya jinai yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama.

Ibara 87
Maombi ya ushirikiano : vipengele vya jumla

1. (a) Mahakama itakuwa na mamlaka ya kutaka ushirikiano wa Nchi zinazounda Mahakama. Maombi ya kutaka ushirikiano huo yatapelekwa kwa njia ya kidiplomasia au kwa njia nyingine yoyote ile itakayokubalika na Nchi nyingine yoyote baada ya kuridhia, kukubali, kuidhinisha au kujiunga na Mkataba huu.

Copyright © SIIC 2010

Mabadiliko ya baadaye juu ya njia yoyote iliyochaguliwa yatafanywa na kila Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

(b) Pale itakapoonekana inafaa, bila ya kuathiri vipengele vya aya ndogo (a), maombi yanaweza kupitishiwa kwenye Shirika la Polisi la Kimataifa la Jinai au shirika la kikanda linalofaa.

2. Maombi ya kushirikiana na nyaraka nyingine zozote zile zinazotilia mkazo maombi hayo zitakuwa katika au zitaambatanishwa na tafsiri kwa lugha rasmi ya Nchi iliyoombwa au moja ya lugha za kazi za Mahakama kulingana na chaguo la Nchi baada ya kuridhia, kukubali, kuidhinisha au kujiunga. Mabadiliko ya baadaye ya chaguo hilo yatafanywa kulingana na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

3. Nchi iliyoombwa italifanya ombi hilo la ushirikiano na nyaraka nyingine zozote zinazotilia mkazo ombi hilo kuwa ni vya siri, ila

kama kuvitangaza vitu hivyo ni lazima kwa ajili ya utekelezaji wa ombi hilo.

4. Kuhusiana na ombi la msaada lililowasilishwa chini ya sehemu hii, Mahakama inaweza kuchukua hatua hizo ikiwa ni pamoja na hatua za kuzilinda habari, kama itakavyolazimu, ili kuhakikisha usalama au hali bora ya kimwili au ya kisaikolojia ya waathiriwa wowote wale, wale wanaotarajiwa kuwa mashahidi na familia zao. Mahakama inaweza kuomba kuwa habari yoyote ile inayotolewa chini ya sehemu hii itatolewe na kushughulikiwa kwa namna ambayo italinda usalama, hali bora ya kimwili na ya kisaikolojia ya waathiriwa wowote wale, wale wanaotarajiwa kuwa mashahidi na familia zao.

5. (a) Mahakama inaweza kuiomba Nchi yoyote ile ambayo si mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itoe msaada chini ya sehemu hii kufuatana na mipango ya muda, kwa mkataba na Nchi hiyo au kwa namna nyingine yoyote ile inayofaa.

Copyright © STIC 2010

(b) Pale ambapo Nchi isiyo mojawapo ya Nchi zile zinazounda Mahakama ina makubaliano ya muda au mkataba na Mahakama, inashindwa kushirikiana kutokana na ombi hilo kulingana na utaratibu au mkataba wowote ule, Mahakama inaweza kuliarifu hivyo Baraza la Nchi zinazounda Mahakama au, pale ambapo jambo hilo limewasilishwa kwenye Mahakama na Baraza la Usalama, kuliarifu Baraza la Usalama.

6. Mahakama inaweza kuliomba shirika lolote lile baina ya serikali mbalimbali kutoa habari au nyaraka. Mahakama inaweza kuomba vilevile namna nyingine za ushirikiano na msaada ambao unaweza kukubaliana na shirika hilo na ambao upo chini ya mamlaka au madaraka yake.

7. Pale ambapo Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inashindwa kutekeleza ombi la Mahakama la kutoa ushirikiano kinyume na vipengele vya Mkataba huu, na kwa hivyo kuizuia Mahakama kufanya shughuli zake na kutumia madaraka yake yaliyo chini ya Mkataba huu, Mahakama inaweza kulitambua jambo hilo na kulipeleka kwenye Baraza la Nchi zinazounda

Mahakama au, pale ambapo jambo hilo limewasilishwa na Baraza la Usalama, kulipeleka kwenya Baraza la Usalama.

Ibara 88
Kuwepo kwa taratibu zilizo chini ya sheria za kitaifa

Nchi zinazounda Mahakama zitahakikisha kuwepo kwa taratibu zilizo chini ya sheria za kitaifa za Nchi zao kuhusiana na aina zote za ushirikiano zilizoelezewa katika Sehemu hii.

Ibara 89
Kuwawasilisha watu kwenye Mahakama

1. Mahakama inaweza kutoa ombi la kukamatwa na kuwasilishwa kwa mtu, pamoja na vitu vinavyotilia mkazo ombi hilo vilivyoelezewa katika ibara 91, kwa Nchi yoyote ile yenye eneo ambalo mtu huyo anaweza kupatikana na itaomba ushirikiano wa Nchi hiyo katika kumkamata na kumwasilisha. Nchi zinazounda Mahakama, kwa mujibu wa vipengele vya sehemu hii na utaratibu ulio chini ya sheria zao za kitaifa, zitakubali ombi la kumkamata na kumwasilisha mtu huyo.

2. Pale ambapo mtu anayetakiwa awasilishwe anaweka pingamizi kwenye mahakama ya kitaifa kwa misingi ya ne bis in idem, kama ilivyo katika ibara 20, Nchi iliyoombwa itashauriana na Mahakama kwa haraka ili kuamua ikiwa pamekuwepo na uamuzi unaofaa juu ya kukubalika. Ikiwa kesi hiyo imekubalika, Nchi iliyoombwa itaendelea na utekelezaji wa ombi hilo. Ikiwa uamuzi wa kukubalika unasubiriwa, Nchi iliyoombwa inaweza kuahirisha utekelezaji wa ombi la kumwasilisha mtu huyo hadi hapo Mahakama itakapofanya uamuzi juu ya kukubalika.

3. (a) Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, kwa mujibu wa sheria zake za utaratibu za kitaifa, itaruhusu kusafirishwa kwa kupitia katika eneo lake mtu anayetakiwa kuwasilishwa kwenye Mahakama na Nchi nyingine, isipokuwa kama kupitia katika Nchi hiyo kutazuia au kuchelewesha kuwasilishwa kwake.

Copyright © STIC 2010

(b) Ombi la Mahakama la kumpitisha katika Nchi litawasilishwa kwa mujibu wa ibara 87. Ombi la kumpitisha katika Nchi litakuwa na :

(i) Wasifu wa mtu anayesafirishwa ;

(ii) Maelezo mafupi kuhusiana na kesi na uainishaji wake wa kisheria ; na

(iii) Hati ya kukamata na kuwasilisha ;

(c) Mtu anayesafirishwa atawekwa kizuizini wakati akiwa anasafirishwa ;

(d) Hakitahitajika kibali ikiwa mtu huyo anasafirishwa kwenye ndege na ndege hiyo haitatua kwenye eneo la Nchi ambayo mtu huyo anapitia ;

(e) Ikiwa ndege inayomsafirisha mtu huyo italazimika kutua bila ya kupangiwa katika eneo la Nchi anayopitishwa, Nchi hiyo itataka liwepo ombi la Mahakama kwa mtu huyo kupitia katika Nchi hiyo kama ilivyo katika aya ndogo (b). Nchi ambayo mtu huyo anapitia itamweka kizuizini mtu anayesafirishwa mpaka litakapopokelewa ombi kuwa mtu huyo apitie katika Nchi hiyo na amepitia katika Nchi hiyo, ili mradi tu kuwekwa kizuizini huko kwa madhumuni ya aya ndogo hii hakutakuwa kwa zaidi ya saa 96 kutoka wakati utuaji huo wa ndege usiopangwa umefanyika ila kama ombi hilo linapokelewa ndani ya muda huo.

4. Ikiwa mtu anayetafutwa ana kesi dhidi yake au anatumikia kifungo katika Nchi inayoombwa, kwa kosa la jinai ambalo ni tofauti na lile ambalo anatakiwa awasilishwe kwenye Mahakama, Nchi inayoombwa, baada ya kufanya uamuzi wake wa kukubali ombi, itashauriana na Mahakama.

Ibara 90
Maombi shindani

1. Nchi mojawapo kati ya zile zinazounda Mahakama inayopokea ombi la Mahakama kumwasilisha mtu chini ya ibara 89, ikiwa

Copyright © STIC 2010

inapokea vilevile ombi kutoka Nchi nyingine la kumrudisha mtu huyohuyo kwa kosa lilelile ambalo ndiyo msingi unayoifanya Mahakama iombe kuwasilishwa kwake, Nchi hiyo itaiarifu Mahakama na Nchi inayoomba juu ya jambo hilo.

2. Pale ambapo Nchi inayoomba ni mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, Nchi inayoombwa itatoa kipaumbele kwa ombi la Mahakama ikiwa :

(a) Mahakama imeamua, kufuatana na ibara 18 au 19, kuwa kesi inayohitaji kuwa mtu huyo awasilishwe inakubalika na uamuzi huo unatilia maanani upelelezi au mashtaka yaliyoendeshwa na Nchi inayoomba kuhusiana na ombi lake la kumrudisha mtu huyo ; au

(b) Mahakama inafanya uamuzi ulioelezewa katika aya ndogo (a) kufuatana na taarifa kutoka kwa Nchi iliyoombwa chini ya aya 1.

Copyright © STIC 2010

3. Pale ambapo uamuzi chini ya aya 2 (a) haukufanyika, Nchi iliyoombwa inaweza, kwa hiari yake, wakati ikisubiri uamuzi wa Mahakama chini ya aya 2 (b) kuendelea na kushughulikia ombi la kurudishwa mtu kutoka Nchi inayoomba lakini haitamrudisha mtu huyo mpaka Mahakama iamue kuwa kesi hiyo haikubaliki. Uamuzi wa Mahakama utafanywa kwa haraka.

4. Ikiwa Nchi inayoomba si mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, Nchi iliyoombwa ikiwa haina wajibu wa kimataifa wa kumrudisha mtu huyo kwenye Nchi iliyoomba, itatoa kipaumbele kwa ombi la Mahakama la kumwasilisha, ikiwa Mahakama imeamua kwamba kesi hiyo inakubalika.

5. Ikiwa Mahakama haikuamua kuwa kesi iliyo chini ya aya 4 inakubalika, Nchi iliyoombwa, inaweza kwa hiari yake, kuendelea kulishughulikia ombi la kumrudisha mtu huyo kutoka kwenye Nchi inayoomba.

6. Pale ambapo aya 4 inahusika, isipokuwa kama Nchi iliyoombwa iko chini ya wajibu wa kimataifa kumrudisha mtu kwenye Nchi iliyoomba ambayo si mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, Nchi iliyoombwa itaamua ikiwa imwasilishe mtu huyo kwenye

Mahakama au imrudishe kwenye Nchi iliyoomba. Katika kufanya uamuzi wake, Nchi iliyoomba itayafikiria mambo yote muhimu, ikiwa ni pamoja na, lakini hayaishii hapo :

(a) Tarehe za maombi hayo ;

(b) Maslahi ya Nchi inayoomba ikiwa ni pamoja, pale inapohusika, kama kosa la jinai limetendeka katika Nchi yake, na uraia wa waathiriwa, na wa mtu anayetafutwa ; na

(c) Uwezekano wa kuwasilishwa hapo baadaye kati ya Mahakama na Nchi inayoomba.

7. Pale ambapo Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inayopokea ombi la Mahakama la kumwasilisha mtu inapokea vilevile ombi kutoka Nchi nyingine yoyote la kumrudisha mtu huyohuyo kwa kosa la jinai ambalo silo lile Mahakama inalotaka awasilishwe :

Copyright © STIC 2010

(a) Nchi iliyoombwa, ikiwa haina jukumu la kimataifa la kumrudisha mtu huyo kwenye Nchi inayoomba, itatoa kipaumbele kwa ombi la Mahakama ;

(b) Nchi inayoombwa, ikiwa ina jukumu la kimataifa la kumrudisha mtu huyo kwenye Nchi inayoomba, itaamua ama kumwasilisha mtu huyo kwenye Mahakama, au kumrudisha mtu huyo kwenye Nchi inayoomba. Katika kufanya uamuzi wake, Nchi iliyoombwa, itayafikiria mambo yote muhimu ikiwa ni pamoja na yale yaliyotajwa katika aya 6, lakini siyo hayo tu, bali itafikiria zaidi hali na ukubwa wa kosa husika.

Pale ambapo imetolewa taarifa chini ya ibara hii, Mahakama imeamua kuwa kesi haikubaliki, na baadaye kurudishwa kwa mtu huyo kwenye Nchi iliyoomba kunakataliwa, Nchi iliyoombwa itaiarifu Mahakama juu ya uamuzi wake.

Ibara 91
Yaliyomo kwenye ombi la kukamata na kuwasilisha

1. Ombi la kukamata na kuwasilisha litafanywa kwa maandishi. Katika hali ya dharura, ombi linaweza kufanywa kwa njia yoyote ile inayoweza kuwasilisha tataarifa ya maandishi, ilimradi tu ombi hilo litathibitishwa kwa kupitia njia zilizoelezewa katika ibara 87, aya 1 (a).

2. Kwa ombi la kumkamata na kumwasilisha mtu ambaye hati ya kukamata imetolewa na Chumba cha Utangulizi chini ya ibara 58, ombi hilo litakuwa au litatiliwa mkazo na :

    (a) Habari zinazomwelezea mtu anayetafutwa, zinazotosha ili kumtambua mtu huyo, na habari kuhusu mahali ambapo mtu huyo anaweza kuwepo ;

    (b) Nakala ya hati ya kukamata ; na

    (c) Nyaraka hizo, taarifa au habari kama ilivyolazimu zikidhi mahitaji ya mchakato mzima wa kumwasilisha mtu huyo katika Nchi iliyoombwa, ila mahitaji hayo yasiwe mengi sana kuliko yale yanayohitajika kwa maombi ya kumrudisha mtu kufuatana na mikataba au taratibu kati ya Nchi iliyoombwa na Nchi nyingine, na ikiwezekana ziwe chache, ikitiliwa maanani hali halisi ya Mahakama.

3. Kwa ombi la kumkamata au kumrudisha mtu ambaye amekwisha kupatikana na hatia, ombi hilo litakuwa na, au litatiliwa mkazo na ;

    (a) Nakala ya hati yoyote ile ya kumkamata mtu huyo ;

    (b) Nakala ya hukumu ya kumtia hatiani ;

    (c) Habari zinazoonyesha kama mtu anayetafutwa ndiye yule anayetajwa katika hukumu ya kumtia hatiani ; na

    (d) Ikiwa mtu anayetafutwa ameshahukumiwa, nakala ya adhabu iliyotolewa, na kwa adhabu ya kifungo, taarifa juu ya muda ambao mtu huyo ameshatumikia kifungo na muda uliobakia.

Copyright © STIC 2010

4. Kwa ombi la Mahakama, Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itashauriana na Mahakama, ama kwa jumla au kuhusiana na jambo maalumu, kuhusu mahitaji yoyote yale chini ya sheria zake za kitaifa ambazo zinaweza kutumika chini ya aya 2 (c). Wakati wa mashauriano, Nchi hiyo mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itaishauri Mahakama juu ya mahitaji maalumu ya sheria zake za kitaifa.

Ibara 92
Kukamatwa kwa muda

1. Katika hali ya dharura, Mahakama inaweza kuomba mtu anayetafutwa akamatwe kwa muda huku ikingojea ombi la kuwasilishwa kwake pamoja na hati za kutaka mtu huyo akamatwe kama inavyoelekezwa katika ibara 91.

2. Ombi la kukamata mtu kwa muda litafanyika kwa njia yoyote inayoweza kuwasilisha kumbukumbu ya maandishi na litakuwa na :

   (a) Habari za kutosha zinazomwelezea mtu anayetafutwa, habari ambazo zitawezesha kumtambua mtu huyo, na habari kuhusu pale ambapo mtu huyo anaweza kuwepo ;

   (b) Maelezo mafupi ya makosa ya jinai yanayosababisha kumkamata na mambo yanayoweza kuwa ni makosa ya jinai, ikiwa ni pamoja na, pale inapowezekana, tarehe na eneo lilipotendeka kosa hilo ;

   (c) Maelezo juu ya kuwepo hati ya kukamata au hukumu ya kumtia hatiani mtu anayetafutwa ; na

   (d) Maelezo kuwa ombi la kutaka kuwasilishwa mtu anayetafutwa litafuata baadaye.

3. Mtu ambaye amekamatwa kwa muda anaweza kuachiwa endapo nchi inayoombwa kumwasilisha haikupokea ombi la kumwasilisha na nyaraka zenye kuthibitisha ombi hilo kama ilivyo katika ibara 91 katika muda ulioelezewa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi. Hata hivyo mtu huyo anaweza kujisalimisha kabla ya kumalizika kwa muda huo endapo sheria ya Nchi inayoombwa inaruhusu

Copyright © STIC 2010

kufanya hivyo. Katika hali kama hiyo, Nchi inayoombwa itamwasilisha mtu huyo katika Mahakama haraka iwezekanvyo.

4. Ile kuwa mtu anayetafutwa ametolewa kizuizini kwa kufuatana na aya 3, hakutoathiri kukamatwa kwa mtu huyo hapo baadaye na kumwasilisha mtu huyo ikiwa ombi la kumwasilisha na nyaraka za kuthibitisha ombi hilo zinawasilishwa baadaye.

Ibara 93
Aina nyingine za ushirikiano

1. Kwa mujibu wa vipengele vya sheria hii na kwa mujibu wa sheria za kitaifa, Nchi zinazounda Mahakama zitakubaliana na maombi ya Mahakama kutoa msaada ufuatao kuhusiana na upelelezi au mashtaka :

   (a) Kumtambua na kuelezea mahali ambapo mtu huyo yupo au mahali zilipo mali zake ;

   (b) Kuchukua ushahidi, ikiwa ni pamoja na maelezo yaliyotolewa kwa kiapo na, kutoa ushahidi, ikiwa ni pamoja na maoni ya wataalamu na ripoti zilizo muhimu kwa Mahakama ;

   (c) Kuhojiwa kwa mtu yeyote anayepelelezwa au kushtakiwa ;

   (d) Kutuma nyaraka, ikiwa ni pamoja na nyaraka za kimahakama ;

   (e) Kuwezesha kujitokeza kwenye Mahakama kwa hiari watu watakaokuwa mashahidi au wataalamu ;

   (f) Kuhamisha watu kwa muda kama ilivyo katika aya 7 ;

   (g) Kukagua maeneo husika ikiwa ni pamoja na kufukua na kukagua maeneo ya makaburi ;

   (h) Kupekua na kukamata ;

   (i) Kuwasilisha kumbukumbu na nyaraka ikiwa ni pamoja na kumbukumbu na nyaraka rasmi ;

Copyright © STIC 2010

(j) Ulinzi wa waathiriwa na mashahidi pamoja na hifadhi ya ushahidi ;

(k) Kutambua, kufuatilia, kuzuia au kukamata mapato, mali na rasilimali ya vitu vinavyoambatana na uhalifu, kwa madhumuni ya kunyang'anywa hapo baadaye bila kuathiri haki za mtu wa tatu anayestahiki ; na

(l) Aina yoyote nyingine ya msaada ambao haukatazwi na sheria za Nchi iliyoombwa, kwa madhumuni ya kuwezesha kufanyika kwa upelelezi na kufungua mashtaka ya uhalifu yaliyo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama.

2. Mahakama itakuwa na uwezo wa kumhakikishia shahidi au mtaalamu anayefika mbele ya Mahakama kwamba yeye hatashtakiwa, hatawekwa kizuizini au kuzuiliwa uhuru wake binafsi na Mahakama kwa namna yoyote ile kutokana na tendo alilotenda au ambalo hakulitenda kabla ya kuondoka kwa mtu huyo kwenye Nchi iliyoombwa.

Copyright © STIC 2010

3. Endapo utekelezaji wa aina fulani ya msaada ulioelezwa katika ombi lililowasilishwa chini ya aya 1 unakatazwa katika Nchi iliyoombwa kwa mujibu wa misingi ya jumla ya kisheria iliyopo, Nchi iliyoombwa itashauriana na Mahakama mara moja ili kutatua suala hilo. Katika mashauriano hayo itabidi ifikiriwe kama msaada huo unaweza kutolewa kwa namna nyingine au kwa masharti fulani. Ikiwa suala hilo haliwezi kutatuliwa baada ya mashauriano hayo Mahakama italifanyia marekebisho ombi hilo kama inavyostahili.

4. Kwa kwa mujibu wa ibara 72, Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inaweza kukataa sehemu au ombi zima la kutoa msaada ikiwa ombi hilo linahusu kutolewa kwa nyaraka au kutoa siri ya ushahidi unaohusiana na usalama wake wa taifa.

5. Kabla ya kukataa ombi la kutoa msaada chini ya aya 1 (1), Nchi iliyoombwa itaangalia kama msaada huo unaweza kutolewa kufuatana na masharti fulani, au kama unaweza kutolewa baadaye au kwa namna nyingine mbadala, ikiwa Mahakama au Mwendesha Mashtaka atakubali msaada huo kwa kutegemea

masharti yaliyowekwa. Mahakama au Mwendesha Mashtaka watayazingatia masharti hayo.

6. Endapo ombi la kutoa msaada linakataliwa, Nchi iliyoombwa itatakiwa kuijulisha Mahakama au Mwendesha Mashtaka mara moja sababu za kukataa ombi hilo.

7. (a) Mahakama inaweza kuomba uhamisho wa muda wa mtu aliye kizuizini kwa madhumuni ya utambulisho au ya kupata maelezo au aina nyingine ya msaada. Mtu huyo anaweza kuhamishwa kama masharti yafuatayo yanatimizwa :

(i) Mtu huyo anatoa kwa hiari ridhaa yake ya kukubali uhamisho huo ; na

(ii) Nchi iliyoombwa inakubaliana na uhamisho huo kwa mujibu wa masharti ambayo Nchi iliyombwa na Mahakama zimekubaliana.

(b) Mtu anayehamishwa atabaki kizuizini. Lengo la kuhamishwa likishatimizwa, Mahakama inapaswa kumrudisha mtu huyo, bila kuchelewa, katika Nchi iliyoombwa.

Copyright © STIC 2010

8. (a) Mahakama itahakikisha kutunzwa kwa siri ya nyaraka na habari, isipokuwa kama zitahitajika kwa upelelezi na uendeshaji wa kesi kama ilivyoelezwa katika ombi.

(b) Pindi ikilazimu, Nchi iliyoombwa inaweza kuwasilisha kwa wendesha Mashtaka nyaraka au habari kwa njia ya siri. Mwendesha mshtaka anaweza kutumia nyaraka na habari hizo kwa madhumuni ya kujenga ushahidi mpya tu.

(c) Nchi iliyoombwa inaweza, kwa hiari yake au kwa kuombwa na Mwendesha Mashtaka, kuridhia kufichuliwa kwa nyaraka au habari hizo. Hapo tena zinaweza kutumiwa kuwa ni ushahidi kulingana na vipengele vya Sehemu 5 na 6 na kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

9. (a) (i) Pindi Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ikipokea ombi jingine ambalo silo lile la kumwasilisha au kumrudisha mtu, kutoka kwenye Mahakama na kutoka katika Nchi nyingine katika utekelezaji wake wa jukumu lake la kimataifa, Nchi hiyo itajaribu, kwa kushauriana na Mahakama na hiyo Nchi nyingine, kukubali maombi yote mawili, ikilazimu kwa kuahirisha au kwa kuweka masharti kwa ombi mojawapo.

(ii) Jambo hilo likishindikana maombi yanayoshindana yatasuluhishwa kwa mujibu wa kanuni zilizoorodheshwa katika ibara 90.

(b) Pale ambapo ombi la Mahakama linahusu habari, mali au watu ambao wapo chini ya mamlaka ya Nchi ya tatu au shirika la kimataifa, kwa uwezo wa mkataba wa kimataifa Nchi zilizoombwa zitaijulisha hivyo Mahakama na Mahakama itaelekeza ombi lake kwa Nchi ya tatu au shirika la kimataifa.

Copyright © STTC 2010

10. (a) Pindi itakapoombwa Mahakama inaweza kushirikiana na kutoa msaada kwa Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ambayo inaendesha upelelezi juu ya kesi inayohusiana na mwenendo wa kosa la jinai lililo ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama au kosa kubwa la jinai kwa mujibu wa sheria za kitaifa za Nchi iliyoombwa.

(b) (i) Msaada utakaotolewa kwa mujibu wa aya ndogo (a) utakuwa ni pamoja na :

a. Kuwasilisha maelezo, nyaraka au ushahidi mwingine wowote ule uliopatikana wakati wa upelelezi au wakati wa kesi inayoendeshwa na Mahakama ; na

b. Kumhoji mtu yeyote yule aliye kizuizini kwa amri ya Mahakama ;

(ii) Kuhusiana na msaada ulio chini ya aya ndogo (b) (i) a :

a. Ikiwa nyaraka hizo au ushahidi wa namna nyingine vinapatikana kwa msaada wa Nchi, upelekaji wa vitu hivyo utahitaji idhini ya Nchi hiyo ;

b. Ikiwa maelezo, nyaraka au ushahidi wa namna nyingine vimetolewa na shahidi au mtaalamu, upelekaji huo utakuwa kwa kutegemea vipengele vya ibara 68.

(c) Chini ya masharti yaliyotolewa katika aya hii, Mahakama inaweza kukubali ombi la kutoa msaada chini ya aya hii kutoka katika Nchi ambayo si moja wapo ya Nchi zinazounda Mahakama.

Ibara 94
Kuahirisha utekelezaji wa ombi kuhusiana na upelelezi au mashtaka yanayoendelea

Copyright © STIC 2010

1. Ikiwa utekelezaji wa mara moja wa ombi utaingiliana na upelelezi au mashtaka yanayoendelea ya kesi ambayo haihusiani na ombi husika, Nchi inayoombwa inaweza kuahirisha utekelezaji wa ombi hilo kwa muda ambao itakubaliana na Mahakama. Hata hivyo, kuahirishwa huko hakutakuwa kwa muda mrefu kuliko ule unaohitajika ili kukamilisha upelelezi au mashtaka husika katika Nchi iliyoombwa. Kabla ya kuamua kuahirisha, Nchi iliyoombwa inatakiwa ifikirie kama msaada ulioombwa unaweza ukatolewa mara moja kwa kutegemea hali fulani.

2. Ikiwa utachukuliwa uamuzi wa kuahirisha kufuatana na aya 1, Mwendesha Mashtaka anaweza kutafuta njia za kuhifadhi ushahidi kwa mujibu wa ibara 93, aya 1 (j).

Ibara 95
Kuahirisha utekelezaji wa ombi kuhusiana na pingamizi la kukubalika

Wakati kuna pingamizi la kukubalika linalofikiriwa na Mahakama kufuatana na ibara 18 au 19, Nchi iliyoombwa inaweza kuahirisha utekelezaji wa ombi hilo chini ya sehemu hii wakati ikisubiri uamuzi wa Mahakama, isipokuwa kama Mahakama imeagiza kwamba Mwendesha

Mashtaka anaweza kuendelea kukusanya ushahidi wa namna hiyo kufuatana na ibara 18 au 19.

Ibara 96
Yaliyomo katika ombi la misaada ya aina nyingine chini ya ibara 93

1. Ombi la misaada ya aina nyingine linalotajwa katika ibara 93 linapaswa kutolewa kwa maandishi. Katika hali za dharura, ombi linaweza kutolewa kwa njia nyingine yoyote inayoweza kuwasilisha kumbukumbu ya maandishi, ilimradi tu ombi hilo linathibitishwa kufuatana na masharti ya ibara 87, aya 1, (a).

2. Ombi linapaswa, ikihitajika, kuwa na au kutegemezwa na vifuatavyo :

   (a) Taarifa fupi juu ya madhumuni ya ombi na msaada unaoombwa, ikiwa ni pamoja na msingi wa kisheria na sababu za ombi ;

   (b) Maelezo ya habari kwa urefu iwezekanavyo kuhusu mahali alipo mtu au utambulisho wake au mahali anapoweza kupatikana au kutambuliwa ili msaada unaoombwa utolewe ;

   (c) Taarifa fupi ya matendo muhimu yanayosisitiza ombi hilo ;

   (d) Sababu na maelezo ya kinaganaga ya utaratibu wowote wa kufuatwa au mahitaji mengine ;

   (e) Habari yoyote itakayotakiwa chini ya sheria ya Nchi iliyoombwa ili kutekeleza ombi hilo ; na

   (f) Habari nyingine yoyote muhimu itakayowezesha kupatikana kwa msaada unaoombwa.

3. Kwa ombi la Mahakama, Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, itashauriana na Mahakama ama kwa jumla, au kuhusiana na jambo maalumu, juu ya sheria zake za kitaifa ambazo zinaweza kutumika chini ya aya 2, (e). Wakati wa mashauriano,

Copyright © STIC 2010

Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itaishauri Mahakama juu ya mahitaji maalumu ya sheria zake za kitaifa.

4. Vipengele vya ibara hii, pale vinapoweza kutumika, vitahusiana vilevile na ombi la msaada kwa Mahakama.

Ibara 97
Mashauriano

Pale Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inapopokea ombi lililo chini ya Sehemu hii na kama ombi hilo linaainisha matatizo yanayoweza kukwamisha au kuzuia utekelezaji wa ombi hilo, Nchi hiyo itapaswa kushauriana na Mahakama bila ya kuchelewa ili kutatua matatizo hayo. Matatizo hayo yatakuwa ni pamoja na mambo mengine kama :

(a) Habari zisizotosheleza katika kutekeleza ombi ;

(b) Kuhusiana na ombi la kuwasilisha mtu, ukweli kuwa juu ya jitihada zote zilizofanywa, mtu anayetafutwa haeleweki mahali alipo, au kwamba upelelezi uliofanywa umedhihirisha kuwa mtu aliye katika Nchi iliyoombwa siye yule aliyetajwa katika hati ya kukamata ; au

Copyright © SFIC 2010

(c) Ukweli kwamba utekelezaji wa ombi hilo kama lilivyo utailazimisha Nchi iliyoombwa kuvunja mkataba ambao tayari upo kati yake na nchi nyingine.

Ibara 98
Ushirikiano kuhusiana na kumwondolea mtu kinga ya kisheria na kuridhia kumwasilisha

1. Mahakama haitaendelea na ombi la kutaka mtu awasilishwe au la msaada wowote ambalo litaitaka Nchi inayoombwa kutenda kinyume na wajibu wake chini ya sheria za kimataifa, kuhusiana na serikali yenyewe au kinga ya kidiplomasia ya mtu au ya mali ya Nchi ya tatu ; isipokuwa kama Mahakama itaweza kwanza kupata ushirikiano wa Nchi hiyo ya tatu juu ya kuondoa kinga ya kidiplomasia.

2. Mahakama haitaendelea na ombi la kutaka mtu awasilishwe, ombi ambalo litaitaka Nchi inayoombwa kutenda kinyume na wajibu

wake chini ya mikataba ya kimataifa inayotaka ipatikane idhini ya Nchi anayoombwa kumwasilisha mtu kwenye Mahakama ; isipokuwa kama Mahakama imepata kwanza ushirikiano wa Nchi iliyoombwa kumwasilisha mtu kwenye Mahakama kwa kutoa idhini ya mtu huyo kuwasilishwa.

Ibara 99
Utekelezaji wa maombi yaliyotolewa chini ya ibara 93 na 96

1. Ombi la msaada litatekelezwa kwa mujibu wa utaratibu wa sheria za Nchi iliyoombwa, isipokuwa kama sheria hizo haziruhusu, kwa namna itakavyoelezewa katika ombi, ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu zozote zilizoelezewa katika ombi hilo au kumruhusu mtu aliyetajwa katika ombi hilo awepo na asaidie katika mchakato wa utekelezaji .

2. Katika hali ya dharura, nyaraka au ushahidi uliotolewa kufuatana na ombi utapelekwa haraka kufuatia ombi la Mahakama.

3. Majibu kutoka Nchi iliyoombwa yatawasilishwa katika lugha na muundo wake wa asili.

4. Bila kuathiri ibara nyingine katika Sehemu hii, pale inapolazimu kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa ombi ambalo linaweza kutekelezwa bila ya kuchukua hatua za kulazimisha hasa, ikiwa ni pamoja na mahojiano au kuchukua ushahidi kutoka kwa mtu kwa hiari yake, ikiwa ni pamoja na kufanya hivyo bila ya kuwepo mwakilishi wa Nchi iliyoombwa ambayo ni mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ; kama ni lazima kwa ombi hilo kutekelezwa, na kukagua bila kufanyiwa marekebisho eneo la wazi au sehemu nyingine ya wazi, Mwendesha Mashtaka anaweza kutekeleza ombi hilo moja kwa moja katika eneo la Nchi husika kwa namna ifuatayo :

    (a) Ikiwa Nchi iliyoombwa ambayo ni mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ndiyo inatuhumiwa kuwa ndipo kosa la jinai lilipotendeka, na imekubaliwa na Mahakama kufuatana na ibara 18 au 19, Mwendesha Mashtaka atatekeleza moja kwa moja ombi hilo baada ya kufanya mashauriano yote yanayowezekana na Nchi iliyoombwa ambayo ni moja ya zile zinazounda Mahakama ;

Copyright © STIC 2010

(b) Katika hali nyingine, Mwendesha Mashtaka anaweza kutekeleza ombi hilo baada ya kufanya mashauriano na Nchi iliyoombwa ambayo ni mojawapo ya zile zinazounda Mahakama na kwa kutegemea masharti yoyote yanayokubalika au wasiwasi ulioelezewa na Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama. Pale Nchi iliyoombwa ambayo ni mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itaainisha matatizo yanayohusiana na utekelezaji wa ombi kufuatana na aya hii ndogo ; itashauriana na Mahakama bila ya kuchelewa ili kutatua jambo hilo.

5. Vipengele vinavyomruhusu mtu aliyekwisha kusikilizwa au aliyekwisha kuchunguzwa na Mahakama chini ya ibara 72 kuomba vipingamizi vyenye nia ya kumzuia kutoa habari za siri zinazohusiana na usalama wa taifa vitahusika vilevile na utekelezaji wa maombi ya msaada chini ya ibara hii.

Copyright © STIC 2010

Ibara 100
Gharama

1. Gharama za kawaida kwa ajili ya utekelezaji wa maombi katika Nchi iliyoombwa zitalipwa na Nchi hiyo, isipokuwa gharama zifuatazo ambazo zitalipwa na Mahakama :

(a) Gharama zinazohusiana na usafiri na usalama wa mashahidi na wataalamu au uhamishaji wa watu walio kizuizini chini ya ibara 93 ;

(b) Gharama za kutafsiri, ukalimani na kunakili ;

(c) Gharama za usafiri na za kujikimu za majaji, Mwendesha Mashtaka, Naibu Mwendesha Mashtaka, Msajili, Naibu Msajili na mtumishi yeyote wa chombo chochote cha Mahakama ;

(d) Gharama za maombi yoyote ya kitaalamu au ripoti iliyoombwa na Mahakama ;

(e) Gharama zinazohusiana na kumsafirisha mtu anayewasilishwa katika Mahakama na Nchi inayomshikilia ; na

(f) Baada ya mashauriano, gharama zozote ambazo si za kawaida zitakazotokana na utekelezaji wa ombi.

2. Vipengele vya aya 1, kama itakavyoonekana inafaa, vitahusu maombi kutoka kwa Nchi ambayo ni mojawapo ya zinazounda Mahakama. Kwa hali hiyo, Mahakama italipia gharama za kawaida za utekelezaji.

Ibara 101
Kanuni ya shtaka maalumu

1. Mtu aliyewasilishwa kwenye Mahakama chini ya Mkataba huu hatashtakiwa, hataadhibiwa au kuwekwa kizuizini kwa kosa lolote alilolifanya kabla ya kuwasilishwa kwake, bali kwa mwenendo ambao ndio msingi wa makosa ya jinai yaliyosababisha kuwasilishwa kwa mtu huyo.

Copyright © STTC 2010

2. Mahakama inaweza kuomba kuondolewa kwa mahitaji yaliyomo katika aya 1 kutoka kwa Nchi inayomwasilisha mtu kwenye Mahakama, na ikilazimu, Mahakama itatoa habari za ziada kwa mujibu wa ibara 91. Nchi zinazounda Mahakama zitakuwa na mamlaka ya kuruhusu Mahakama kutotumia masharti hayo na inapaswa kujitahidi kufanya hivyo.

Ibara 102
Matumizi ya istilahi

Kwa madhumuni ya Mkataba huu :

(a) Neno «kuwasilisha» linamaanisha Nchi kukabidhi mtu kwenye Mahakama, kufuatana na Mkataba huu.

(b) Neno « kurejesha mkosaji/mtuhumiwa » linamaanisha Nchi kukabidhi mtu kwa Nchi nyingine kama ilivyo katika mkataba, makubaliano au sheria za taifa.

Sehemu X Utekelezaji

Ibara 103
Wajibu wa Nchi katika utekelezaji wa adhabu za kifungo

1. (a) Adhabu ya kifungo itatumikiwa katika Nchi itakayoteuliwa na Mahakama kutoka katika orodha ya Nchi zilizoijulisha Mahakama nia yao ya kukubali kuwapokea watu waliohukumiwa.

   (b) Wakati wa kuijulisha Mahakama nia yake ya kukubali watu waliohukumiwa, Nchi inaweza kuweka masharti ya kukubali kwake kama ilivyokubaliwa na Mahakama na kwa mujibu wa Sehemu hii.

   (c) Nchi iliyoteuliwa na Mahakama katika hali maalumu itaiarifu Mahakama mara moja kama inakubali uteuzi wa Mahakama.

2. (a) Nchi ya utekelezaji itaiarifu Mahakama hali yoyote, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa masharti yoyote yaliyokubaliwa chini ya aya 1 ambayo yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa makubaliano au kiwango cha kifungo. Mahakama itapewa angalau notisi ya siku 45 juu ya hali yoyote itakayojitokeza ambayo ilijulikana au inayotabirika. Katika kipindi hicho, Nchi ya utekelezaji haitachukua hatua yoyote itakayoathiri wajibu wake chini ya ibara 110.

   (b) Pale ambapo Mahakama haiwezi kukubaliana na hali zilizotajwa katika aya ndogo (a), itapaswa kuiarifu Nchi ya utekelezaji na kuendelea kwa mujibu wa ibara 104, aya 1.

3. Katika kutumia hiari yake ya kuteua chini ya aya 1, Mahakama itapaswa kuzingatia yafuatayo :

   (a) Kanuni kwamba Nchi zinazounda Mahakama zitapaswa kugawana majukumu ya utekelezaji wa adhabu ya kifungo kwa mujibu wa kanuni za mgawanyo sawa, kama ilivyo katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi ;

Copyright © STIC 2010

(b) Utekelezaji wa viwango vya mikataba ya kimataifa inayokubalika kwa kiasi kikubwa inayotawala utendeaji wa wafungwa ;

(c) Maoni ya mtu aliyehukumiwa ;

(d) Uraia wa mtu aliyehukumiwa ;

(e) Mambo mengine yanayohusiana na hali ambamo kosa la jinai lilitendeka au mtu aliyehukumiwa, au utekelezaji madhubuti wa adhabu, kama itakavyoonekana inafaa katika kuteua Nchi ya utekelezaji.

4. Ikiwa hakuna Nchi iliyoteuliwa chini ya aya 1, adhabu ya kifungo itatumikiwa katika gereza litakalotolewa na Nchi mwenyeji, kwa mujibu wa masharti yaliyomo katika mkataba wa makao makuu yanayotajwa na ibara 3, aya 2. Katika hali kama hiyo, gharama za utekelezaji wa adhabu ya kifungo zitalipwa na Mahakama.

Copyright © STIC 2010

Ibara 104
Mabadiliko katika uteuzi wa Nchi ya utekelezaji

1. Mahakama inaweza, wakati wowote ule, kuamua kumhamishia mtu aliyehukumiwa kwenye gereza la Nchi nyingine.

2. Mtu aliyehukumiwa anaweza, wakati wowote ule, kuomba Mahakama ahamishwe kutoka katika Nchi ya utekelezaji.

Ibara 105
Utekelezaji wa adhabu

1. Bila kuathiri masharti ambayo Nchi imeyaweka kwa mujibu wa ibara 103, aya 1 (b) adhabu ya kifungo ni lazima izingatiwe na Nchi zinazounda Mahakama, ambazo haziwezi kamwe kuibadilisha.

2. Ni Mahakama pekee ndiyo yenye haki ya kuamua juu ya ombi lolote lile la rufaa na la marudio. Nchi ya utekelezaji haitazuia kufanyika kwa ombi la aina hiyo linalofanywa na mtu aliyehukumiwa.

Ibara 106
Usimamizi wa utekelezaji wa adhabu na wa hali ya kifungo

1. Utekelezaji wa adhabu ya kifungo utasimamiwa na Mahakama na utalingana na viwango vya mikataba ya kimataifa inayokubalika kwa kiasi kikubwa ; inayotawala utendeaji wa wafungwa.

2. Hali ya kifungo itatawaliwa na sheria za Nchi ya utekelezaji na italingana na viwango vya mikataba ya kimataifa inayokubalika kwa kiasi kikubwa ; inayotawala utendeaji wa wafungwa ; hali hiyo haiwezi kamwe kuwa nzuri zaidi au mbaya zaidi kuliko ile ya wafungwa waliopatikana na hatia kwa makosa kama hayo katika Nchi ya utekelezaji.

3. Mawasiliano kati ya mtu aliyehukumiwa na Mahakama yatakuwa huru na ya siri.

Copyright © STIC 2010

Ibara 107
Kuhamisha mtu aliyehukumiwa baada ya kumaliza adhabu yake

1. Baada ya kumaliza adhabu yake, mtu asiyekuwa raia wa Nchi ya utekelezaji, anaweza, kwa mujibu wa sheria za Nchi ya utekelezaji, kuhamishiwa katika Nchi nyingine inayotakiwa kumpokea au katika Nchi nyingine inayokubali kumpokea, kwa kutilia maanani matakwa yoyote ya mtu anayehamishiwa katika Nchi hiyo, isipokuwa kama Nchi ya utekelezaji itamwamuru mtu huyo abakiye katika Nchi hiyo.

2. Kama hakuna Nchi iliyokuwa tayari kulipa gharama za kumhamisha mtu huyo kwenda Nchi nyingine kufuatana na aya 1, gharama hizo zitalipwa na Mahakama.

3. Kwa kutegemea vipengele vya ibara 108, Nchi ya utekelezaji inaweza vilevile, kwa mujibu wa sheria zake za kitaifa, kumrejesha au kumwasilisha mtu huyo kwenye Nchi iliyoomba mtu huyo arejeshwe au awasilishwe kwa ajili ya kufikishwa kwenye Mahakama au kutumikia adhabu.

Ibara 108
Kikomo cha mashtaka au adhabu ya makosa mengine

1. Mtu aliyehukumiwa ambaye anatumikia kifungo katika Nchi ya utekelezaji hatashtakiwa au kuadhibiwa au kurejeshwa nchi ya tatu kwa mwenendo wowote aliokuwa nao kabla ya mtu huyo kuwasilishwa kwenye Nchi ya utekelezaji, isipokuwa tu kama mashtaka hayo, adhabu au kurejeshwa huko kumeidhinishwa na Mahakama kutokana na ombi la nchi ya utekelezaji.

2. Mahakama itaamua jambo hilo baada ya kusikiliza maoni ya mtu aliyehukumiwa.

3. Aya 1 itasita kutumika endapo mtu aliyehukumiwa atabaki kwa hiari yake katika Nchi ya utekelezaji kwa muda wa zaidi ya siku 30 baada ya kumaliza kutumikia adhabu aliyopewa na Mahakama, au akirudi tena katika nchi hiyo baada ya kuondoka.

Copyright © STIC 2010

Ibara 109
Utekelezaji wa hatua ya kupiga faini au kunyang'anywa mali

1. Nchi zinazounda Mahakama zitatekeleza adhabu ya kupiga faini na hatua ya kunyang'anya mali vilivyoamriwa na Mahakama kulingana na sura 7, bila kuathiri haki za mtu wa tatu mwaminifu, na kulingana na utaratibu wa sheria zao za kitaifa.

2. Ikiwa Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama haiwezi kutekeleza amri ya kunyang'anya mali, itachukua hatua ya kupata tena thamani ya mapato, mali au raslimali ambavyo Mahakama iliamua vinyang'anywe, bila kuathiri haki ya mtu wa tatu mwaminifu.

3. Mali, au mapato ya mauzo ya mali isiyohamishika au pale inapofaa mauzo ya mali nyingine itakayopatikana na Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itahamishiwa kwenye Mahakama.

Ibara 110
Mahakama kufanya marudio ya hukumu kuhusiana na upunguzaji wa adhabu

1. Nchi ya utekelezaji haitamwachia mtu huru kabla ya kumaliza muda wa adhabu iliyotolewa na Mahakama.

2. Ni Mahakama tu ndiyo yenye haki ya kuamua juu ya upunguzaji wowote ule wa adhabu, na itaamua jambo hilo baada ya kumsikiliza mtu huyo.

3. Ikiwa mtu ametumikia theluthi mbili ya adhabu yake au miaka 25 kwa yule anayetumikia kifungo cha maisha, Mahakama itafanya marudio ya adhabu hiyo ili kuamua kama kuna haja ya kuipunguza. Marudio kama hayo hayatafanyika kabla ya muda huo.

Copyright © STIC 2010

4. Katika marudio yake chini ya ibara 3, Mahakama inaweza kuipunguza adhabu pindi ikitambua kwamba lipo jambo moja au zaidi ya mambo yafuatayo :

    (a) Mtu kuonyesha mapema kuendelea kuwa tayari kushirikiana na Mahakama katika upelelezi na mashtaka ;

    (b) Msaada wa hiari wa mtu katika kuwezesha utekelezaji wa hukumu na amri ya Mahakama katika hali nyingine, na hasa kwa kutoa msaada wa kuonyesha mali zilipo kulingana na amri ya kupiga faini, kunyang'anya mali au malipo yanayoweza kutumiwa kwa manufaa ya waathiriwa ; au

    (c) Mambo mengine yanayoonyesha dhahiri mabadiliko makubwa ya hali yenye kutosheleza kuhalalisha kupunguzwa kwa adhabu kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

5. Ikiwa Mahakama itaamua katika marudio yake ya awali chini ya aya 3 kuwa si sahihi kupunguza adhabu, italirudia tena baadaye suala la kupunguza adhabu kwa vipindi kama hivyo na kwa kutumia vigezo kama hivyo vinavyoelezwa katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

Ibara 111
Kutoroka

Kama mtu aliyepatikana na hatia anatoroka gerezani na kukimbia kutoka Nchi ya utekelezaji, nchi hiyo baada ya kushauriana na Mahakama inaweza kuomba kurejeshwa kwa mtu huyo kutoka katika nchi ambayo mtu huyo yupo kufuatana na taratibu zilizopo baina ya pande mbili au zaidi, au inaweza kuomba kuwa Mahakama itafute uwezekano wa mtu huyo kurudishwa kwa mujibu wa Sehemu 9. Mahakama inaweza kuagiza kuwa mtu huyo awasilishwe au arudishwe katika Nchi ambayo alikuwa akitumikia adhabu au katika Nchi nyingine itakayoteuliwa na Mahakama.

Copyright © STIC 2010

Sehemu XI Baraza la Nchi zinazounda Mahakama

Ibara 112
Baraza la Nchi zinazounda Mahakama

1. Baraza la Nchi zinazounda Mahakama chini ya Mkataba huu linaundwa. Kila Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itakuwa na mwakilishi mmoja katika Baraza hilo, ambaye ataweza kufuatana na wawakilishi mbadala na washauri. Nchi nyingine zilizosaini Mkataba huu au makubaliano ya mwisho zinaweza kuwa watazamaji katika Baraza.

2. Baraza :

   (a) Litajadili na kukubali, kama inavyofaa mapendekezo ya Tume ya Maandalizi ;

   (b) Litasimamia uendeshaji unaohusu utawala wa Ofisi ya Rais, Mwendesha Mashtaka na Msajili ;

   (c) Litajadili ripoti na shughuli za Ofisi iliyoundwa chini ya aya 3 na kuchukua hatua zinazofaa kuhusiana na hilo ;

   (d) Litajadili na kupitisha bajeti ya Mahakama ;

   (e) Litaamua kama libadilishe idadi ya majaji kwa mujibu wa ibara 36 ;

   (f) Litajadili suala lolote linalohusiana na kutotoa ushirikiano kufuatana na ibara 87, aya 5 na 7 ;

   (g) Litafanya shughuli yoyote kulingana na Mkataba huu au Kanuni za Utaratibu na Ushahidi.

3. (a) Baraza litakuwa na Ofisi itakayokuwa na Rais, Makamu wa Rais wawili na wajumbe 18 watakaochaguliwa na Baraza kwa kipindi cha miaka mitatu.

   (b) Ofisi itakuwa na utaratibu wa uwakilishi, utakaotilia maanani, hasa mgawanyo sawa wa kijiografia na

Copyright © STIC 2010

uwakilishi wa kutosha wa mifumo mikuu ya kisheria duniani.

(c) Ofisi itakutana mara nyingi iwezekanavyo lakini angalau mara moja kwa mwaka. Italisaidia Baraza katika utekelezaji wa majukumu yake.

4. Baraza linaweza kuunda mashirika tanzu kama itakavyohitajika, ikiwa ni pamoja na utaratibu huru wa usimamizi kwa ajili ya ukaguzi, kufanya tathmini na upelelezi wa Mahakama, ili kuboresha ufanisi na uchumi wake.

5. Rais wa Mahakama, Mwendesha Mashtaka na Msajili au wawakilishi wao wanaweza kushiriki, kama itavyoonekana inafaa, katika mikutano ya Baraza na ya Ofisi.

6. Baraza litakutana kwenye makao makuu ya Mahakama au ya Umoja wa Mataifa mara moja kwa mwaka na, ikihitajika, litafanya mikutano maalumu. Isipokuwa tu kama imeelezwa vingine katika Mkataba huu, Mikutano maalumu itaitishwa na Ofisi kwa utashi wake au kwa maombi ya theluthi moja ya Nchi zinazounda Mahakama.

Copyright © STIC 2010

7. Kila Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama itakuwa na kura moja. Zitafanywa kila juhudi ili kufikia uamuzi kwa makubaliano ya pamoja katika Baraza na katika Ofisi. Ikiwa makubaliano ya pamoja hayataweza kufikiwa, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo katika Mkataba huu :

(a) Maamuzi ya mambo muhimu lazima yapitishwe kwa theluthi mbili ya wingi wa kura za wale waliohudhuria na kupiga kura ilimradi tu wingi ulio dhahiri wa Nchi zinazounda Mahakama ndiyo utakaofanya akidi ya kupiga kura ;

(b) Maamuzi kuhusu masuala ya utaratibu yatachukuliwa kwa wingi sahili wa Nchi zinazounda Mahakama zitakazohudhuria na kupiga kura.

8. Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ambayo imechelewa kulipa michango yake ya fedha kwa ajili ya gharama

za Mahakama haitakuwa na kura katika Baraza wala katika Ofisi ikiwa kiasi cha malimbikizo kinalingana au kinazidi kiasi cha michango yake inayopaswa kulipa kwa miaka miwili iliyopita. Hata hivyo, Baraza linaweza kuiruhusu Nchi hiyo kupiga kura katika Baraza na katika Ofisi likiridhika kuwa kushindwa kwake kulipa kunatokana na hali iliyo nje ya uwezo wa Nchi hiyo.

9. Baraza litapitisha kanuni zake za utaratibu.

10. Lugha rasmi na lugha za kazi za Baraza zitakuwa zile zinazotumika katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Copyright © STIC 2010

Sehemu XII Mambo ya fedha

Ibara 113
Kanuni za fedha

Isipokuwa kama inaelezwa vinginevyo mambo yote ya fedha yanayohusiana na fedha za mikutano ya Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, ikiwa ni pamoja na Ofisi yake na mashirika tanzu, yatatawaliwa na Mkataba huu, na Kanuni za Fedha na kanuni zilizopitishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

Ibara 114
Ulipaji wa gharama

Gharama za Mahakama, za Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, ikiwa ni pamoja na za Ofisi zake na za mashirika tanzu zitalipwa kutoka kwenye Mfuko wa fedha za Mahakama.

Copyright © STIC 2010

Ibara 115
Fedha za Mahakama na za Baraza la Nchi zinazounda Mahakama

Gharama za Mahakama, za Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, za Ofisi na za mashirika tanzu kama ilivyo katika bajeti ya Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, zitapatikana kutoka vyanzo vifuatavyo :

(a) Michango iliyokadiriwa ya Nchi zinazounda Mahakama ;

(b) Fedha zinazotolewa na Umoja wa Mataifa, baada ya kuidhinishwa na Baraza Kuu, hususan kuhusiana na gharama zilizotumiwa kwa rufaa za Baraza la Usalama.

Ibara 116
Michango ya hiari

Bila kuathiri ibara 115, Mahakama inaweza kupokea na kutumia, kama fedha za ziada, michango ya hiari kutoka katika serikali, mashirika ya kimataifa, watu binafsi, makampuni na vyombo vingine, kulingana na vigezo muhimu vilivyopitishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama.

Ibara 117
Ukadiriaji wa michango

Michango ya Nchi zinazounda Mahakama itakadiriwa kwa mujibu wa viwango vya ukadiriaji vilivyokubaliwa, kulingana na viwango vilivyokubaliwa na Umoja wa Mataifa kwa ajili ya bajeti yake ya kawaida, na kufanyiwa marekebisho kwa mujibu wa misingi inayotumiwa katika kukadiria viwango hivyo.

Ibara 118
Ukaguzi wa mahesabu ya mwaka

Kumbukumbu, vitabu na mahesabu ya Mahakama, ikiwa ni pamoja na taarifa zake za fedha za mwaka vitakaguliwa kila mwaka na mkaguzi wa kujitegemea.

Copyright © STIC 2010

Sehemu XIII Vifungu vya mwisho

Ibara 119
Usuluhishi wa migogoro

1. Mgogoro wowote ule unaohusiana na shughuli za kimahakama za Mahakama utasuluhishwa kwa uamuzi wa Mahakama.

2. Mgogoro mwingine wowote ule baina ya Nchi mbili au zaidi zinazounda Mahakama unaohusiana na ufafanuzi au utekelezaji wa Mkataba huu ambao haukusuluhishwa kwa njia ya majadiliano katika kipindi cha miezi mitatu toka kuanza kwake utapelekwa kwenye Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Baraza lenyewe linaweza kuamua kuusuluhisha mgogoro huo au linaweza kutoa mapendekezo juu ya njia nyingine za usuluhishi wa mgogoro huo, ikiwa ni pamoja na kuupeleka kwenye Mahakama ya haki ya Kimataifa kulingana na Mkataba wa mahakama hiyo.

Copyright © STIC 2010

Ibara 120
Tamko linalolenga kutoa au kubadili matokeo ya kisheria

Mkataba huu hautaruhusu tamko lolote lile linayolenga kutoa au kubadili matokeo ya kisheria ya vipengele vyake.

Ibara 121
Marekebisho

1. Baada ya miaka saba kupita tangu Mkataba huu uanze kutumika, Nchi yoyote mojawapo ya zile zinazounda Mahakama inaweza kupendekeza yafanywe marekebisho kwa Mkataba huu. Hati ya marekebisho yoyote yanayopendekezwa itawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ambaye ataisambaza haraka kwa Nchi zote zinazounda Mahakama.

2. Mara baada ya miezi mitatu kupita kuanzia tarehe ya kutoa taarifa, Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, katika kikao chake kinachofuata, kwa wingi wa kura za wale watakaohudhuria na kupiga kura, litaamua ikiwa litakubali pendekezo hilo. Baraza linaweza kushughulikia pendekezo hilo moja kwa moja au kuitisha

Mkutano wa Mapitio ikiwa jambo husika linahitaji kufanyiwa hivyo.

3. Ikiwa itashindikana kuyapitisha marekebisho kwa kauli moja katika mkutano wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, au kwenye Mkutano wa Mapitio patahitajika theluthi mbili ya wingi wa kura za Nchi zinazounda Mahakama.

4. Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika aya 5, marekebisho yataanza kutumika katika Nchi zote zinazounda Mahakama baada ya hati za kuridhia au kukubali kuwasilishwa na saba ya nane ya nchi hizo kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

5. Marekebisho yoyote ya ibara 5, 6, 7 na 8 za Mkataba huu yataanza kutumika katika Nchi zote zinazounda Mahakama ambazo zimeyakubali marekebisho hayo mwaka mmoja baada ya kuwasilisha hati zao za kuridhia au za kukubali. Kuhusiana na Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ambayo haikuyakubali marekebisho hayo, Mahakama haitatumia uwezo wake wa kisheria kwa kosa la jinai linalohusu marekebisho hayo ikiwa kosa hilo limefanywa na raia wa Nchi hiyo au katika eneo la Nchi hiyo.

6. Kama marekebisho yamekubaliwa na saba ya nane ya Nchi zinazounda Mahakama kulingana na aya 4, Nchi yoyote mojawapo ya zile zinazounda Mahakama ambayo haikuyakubali marekebisho hayo inaweza kujitoa kwenye Mkataba huu mara moja bila ya kujali ibara 127, aya 1 lakini kwa kuzingatia ibara 127, aya 2, kwa kutoa notisi katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja baada ya marekebisho hayo kuanza kutumika.

7. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atasambaza kwa Nchi zote zinazounda Mahakama marekebisho yaliyopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Nchi zinazounda Mahakama au kwenye mkutano wa marudio.

Copyright © STIC 2010

Ibara 122
Marekebisho ya vipengele vya kiasasi

1. Marekebisho ya vipengele vya Mkataba huu ambavyo ni mahsusi vya kiasasi, ambavyo ni ibara 35, 36, aya 8 na 9, ibara 37, ibara 38,

ibara 39 aya 1 (sentensi mbili za mwanzo), 2 na 4, ibara 42, aya 4 hadi 9, ibara 43, aya 2 na 3, na ibara 44, 46, 47 na 49 vinaweza kupendekezwa wakati wowote na Nchi mojawapo yoyote ya zile zinazounda Mahakama bila kujali ibara 121, aya 1. Hati ya marekebisho yoyote yanayopendekezwa itawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa au kwa mtu yeyote aliyeteuliwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, ambaye ataisambaza mara moja kwa Nchi zote zinazounda Mahakama na wengineo wanaoshiriki katika Baraza.

2. Marekebisho yaliyo chini ya ibara hii ambayo hayakukubalika kwa kauli moja yatapitishwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama au na Mkutano wa Mapitio kwa theluthi mbili ya wingi wa kura za Nchi zinazounda Mahakama. Marekebisho hayo yataanza kutumika katika Nchi zote zinazounda Mahakama miezi sita baada ya kupitishwa na Baraza, au kama itakavyokuwa, na Mkutano wa Mapitio.

Copyright © STIC 2010

Ibara 123
Mapitio ya Mkataba

1. Miaka saba baada ya Mkataba huu kuanza kutumika, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ataitisha Mkutano wa Mapitio ili kujadili marekibisho yoyote ya Mkataba huu. Mapitio hayo yatakuwa ni pamoja na, lakini si lazima hayo tu, orodha ya makosa ya jinai yaliyomo katika ibara 5. Mkutano huo utakuwa wazi kwa wote wanaoshiriki katika Baraza la Nchi zinazounda Mahakama na kwa masharti yale yale.

2. Wakati wowote ule baada ya hapo, kwa ombi la mojawapo ya Nchi zinazounda Mahakama na kwa madhumuni yaliyotajwa katika aya 1, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, baada ya kupata idhini kutoka Nchi nyingi kati ya zile zinazounda Mahakama, ataitisha Mkutano wa Mapitio.

3. Vipengele vya ibara 121, aya 3 hadi 7, vitatumiwa katika kupitisha na kuanza kutumika kwa marekebisho yoyote yale ya Mkataba yaliyojadiliwa katika Mkutano wa Mapitio.

Ibara 124
Vipengele vya mpito

Bila kujali ibara 12, aya 1 na 2, baada ya kuridhia Mkataba huu, Nchi inaweza kutangaza kuwa kwa kipindi cha miaka saba baada ya kuanza kutumika kwa Mkataba huu, haitambui uwezo wa kisheria wa Mahakama kuhusiana na kategoria za makosa ya jinai yaliyotajwa katika ibara 8 ikiwa kosa hilo la jinai linadaiwa kutendwa na raia wake au ndani ya eneo la Nchi hiyo. Tamko linalotokana na ibara hii linaweza kuondolewa wakati wowote. Vipengele vya ibara hii vitapitiwa upya katika Mkutano wa Mapitio utakaoitishwa kwa mujibu wa ibara 123, aya 1.

Ibara 125
Saini, ridhaa, kukubali, idhini au kujiunga

1. Mkataba huu utaweza kutiwa saini na Nchi yoyote mjini Roma, kwenye Makao Makuu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo tarehe 17 Julai 1998. Baada ya hapo, utaweza kutiwa saini mjini Roma katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Italia hadi tarehe 17 Oktoba 1998 na baada ya hapo Mkataba huu unaweza kutiwa saini mjini New York kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa hadi tarehe 31 Disemba 2000.

Copyright © STIC 2010

2. Mkataba huu unaweza kuridhiwa, kukubaliwa au kuidhinishwa na Nchi zilizousaini. Hati za kuuridhia, kuukubali au kuuidhinisha zitawekwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja ya Mataifa.

3. Nchi zote zinaweza kujiunga na Mkataba huu. Hati za kujiunga zitawekwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Ibara 126
Kuanza kutumika

1. Mkataba huu utaanza kutumika siku ya kwanza ya mwezi baada kupita siku sitini kufuatia tarehe ya kuwekwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa hati ya sitini ya kuridhia, kukubali, kuidhinisha au kujiunga.

2. Kwa kila Nchi iliyoridhia, iliyokubali, iliyoidhinisha au iliyojiunga na Mkataba huu baada ya kuwekwa kwa hati ya sitini ya kuridhia,

kukubali, kuidhinisha au kujiunga, Mkataba huu utaanza kutumika siku ya kwanza ya mwezi baada ya siku ya sitini inayofuatia kuwekwa na Nchi hiyo hati yake ya kuridhia, kukubali, kuidhinisha au kujiunga.

Ibara 127
Kujitoa

1. Nchi mojawapo ya zile zinazounda Mahakama, inaweza kujitoa katika Mkataba huu kwa kuwasilisha notisi ya maandishi kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Kujitoa huko kutakuwa rasmi mwaka mmoja baada ya tarehe ya kupokea notisi, isipokuwa kama notisi hiyo inatoa tarehe ya baadaye.

2. Nchi haitaondolewa majukumu yake, ikiwa ni pamoja na majukumu ya fedha zilizolimbikizwa, yanayotokana na Mkataba huu wakati Nchi hiyo ilipokuwa mojawapo ya zile zinazounda Mahakama kutokana na kujitoa kwake. Kujitoa huko hakutaathiri ushirikiano wake wowote na Mahakama kuhusiana na upelelezi wa makosa ya jinai na kesi ambavyo Nchi iliyojitoa ilikuwa na wajibu wa kutoa ushirikiano, na vilivyoanza kabla ya tarehe ambayo kujitoa kwa Nchi hiyo kumekuwa rasmi, wala kujitoa huko hakutaathiri kwa namna yoyote majadiliano yoyote ya Mahakama ambayo tayari yalikuwepo kabla ya tarehe ya kujitoa kwa Nchi hiyo kuwa rasmi.

Copyright © STIC 2010

Ibara 128
Makala halisi

Makala halisi ya Mkataba huu, ambao makala halisi zipo vilevile kwa Kiarabu, Kichina, Kingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania itawekwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ambaye atatuma nakala zake zilizothibithishwa Nchi zote.

Kwa kushuhudia haya, wale waliotia saini zao hapa chini, ambao wameruhusiwa na serikali zao, wamesaini Mkataba huu.

Umetayarishwa Roma, siku hii ya 17 Julai 1998.

Copyright © STIC 2010

Copyright © STIC 2010